

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Thelathini na Tano – Tarehe 24 Mei, 2019

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae. Katibu!

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA MADINI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Katibu!

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Maswali Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi Mbunge wa Mlalalo c kwa niaba yake Mheshimiwa Mary Chatanda.

Na. 287

Kuugawa Mkoa wa Tanga

MHE. MARY P. CHATANDA (K.n.y MHE. RASHID A. SHANGAZI) aliuliza:-

Mkoa wa Tanga ndio Mkoa wenyewe halmashauri nyingi zaidi kwa sasa ukiwa na jumla ya halmashauri kumi na moja:-

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuugawa mkoa huo ili kurahisisha shughuli za utawala na maendeleo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA - MHE. MWITA M. WAITARA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi Mbunge wa Mlalo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwa Mkoa wa Tanga ndio mkoa wenyewe halmashauri nyingi zaidi kwa sasa ukiwa na jumla ya halmashauri 11. Hata hivyo, kipaumbele cha Serikali kwa sasa ni kuimarisha maeneo ya utawala yaliyopo yaliyoanzishwa katika miaka ya hivi karibuni kwa miundombinu na huduma mbalimbali ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi kabla ya kuanzisha maeneo mengine mapya. Hivyo, naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira wakati Serikali ikitekeleza azma ya kuimarisha maeneo yake yaliyopo ambayo yana upungufu wa miundombinu na huduma mbalimbali muhimu kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wetu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ally Keissy swali la nyongeza.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nchi yetu kwa sasa ina miundombinu mizuri kuliko enzi za ukoloni au enzi zilizopita. Je, Serikali inaonaje kwa muda huu kupunguza idadi ya wilaya, idadi ya majimbo ya mikoa ili Serikali ipate pesa, i-save pesa kwa ajili ya kupunguza idadi ya mikoa, idadi ya majimbo na idadi ya wilaya?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, tumemsikia Mheshimiwa Ally Keissy kwa maoni yake na mtazamo wake lakini maeneo haya kiutawala yakiwepo majimbo ya uchaguzi ya Waheshimiwa Wabunge hawa wapendwa, wilaya, mikoa na maeneo mengine ya kata na vijiji yanaanzishwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa utakapofika wakati wa kuona kwamba kwa hilo wazo la Mheshimiwa Keissy ni muhimu kufanyiwa kazi tutalifanya kazi. Kwa sasa msimamo ni kwamba tutaendelea kuimarisha maeneo yaliyopo kujenga miundombinu, kupeleka huduma mbalimbali za kijamii ili watu wote waweze kupata maisha ambayo ni bora zaidi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Oran Njeza swalii la nyongeza.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana ningependa kuuliza swalii la nyongeza mji mdogo wa Mbalizi ulipewa mamlaka miaka 15 iliyopita na sasa hivi ina wakazi zaidi ya 100,000 na pia uwanja wa kimataifa wa Songwe uko katika eneo hilo. Sasa ni lini Mji mdogo wa Mbalizi utapewa hadhi ya kuwa Halmashauri ya Mji wa Mbalizi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba kwa sasa tunaendelea kuimarisha maeneo ya kiutawala yaliyoanzishwa. Wanapozungumzia kuanzisha halmashauri maana yake unaongezea miundombinu unahitaji huduma ya ukubwa zaidi na watendaji watakuwepo na majengo yataongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuvumilia tuimarishe kwanza hii miji midog iliyopo halmashauri zetu na katika nchi hii kuna mikoa mingi pia bado haina majengo ya kutosha ya kuwa mikoa na watendaji wengine. Tuna upungufu wa miundombinu katika halmashauri zetu pia Waheshimiwa Wabunge wenyewe bado wanadai ofisi za Wabunge hazijajengwa. Kwa hiyo, nadhani ukiangalia mahitaji yaliyopo na kuongeza eneo la utawala nadhani tupeane muda kidogo tutekeleze haya yaliyopo tukamilishe tutazingatia baadaye maoni yake, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ezekiel Maige swali la nyongeza

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi kwa kiasi kikubwa swali langu linafanana na Mheshimiwa Njeza kumekuwepo *confusion* ya kuongeza maeneo na kupandisha hadhi. Mko wa Shinyanga tulishamaliza mchakato wa kupendekeza mji wa Kahama uwe manispaa na sifa zote tunakidhi na kigezo kikubwa kimekuwa ni suala la mapato ambayo halmashauri ya Manispaa ya Kahama ina uwezo wa kujindesha kwa hiyo si changamoto kwa Serikali. Pia Mji wa Isaka na tulishafikisha wizarani je, ni lini Wizara kwa mtazamo maalum inaweza ikaruhusu Halmashauri ya Mji wa Isaka pamoja na Halmashauri ya Manispaa ya Kahama itanza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze Naibu wangu kwa ufanuzi mzuri sana. Katika swali hili lakini tunafahamu kwamba nishukuru Mheshimiwa Maige kwa *concern* yake; tuna maeneo makubwa matatu kwanza, kuna Halmashauri ya Mji wa Geita, Kahama, pamoja na Halmashauri ya Mji wa Kibaha ambao sasa iko katika suala la kufanya tathmini ya kuhakikisha kuzipandisha katika hadhi ya manispaa. Kwa hiyo lakini kuna utaratibu sasa hivi ambao tunaendelea kuufanya kwanza kutoanzisha maeneo mapya lakini hilo suala zima la hadhi tutalifanyia kazi pale jambo litakapoiva vizuri mtapata mrejesho Waheshimiwa Wabunge.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tuendelee na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakangata, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 288

Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Rukwa

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA aliuliza:-

Je, ni lini Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Rukwa itaanza kujengwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Rukwa unao Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Sumbawanga inayotoa huduma

za rufaa kwa halmashauri nne za mkoa huo hadi sasa. Hata hivyo hospitali hiyo inayo changamoto ya ufinyu wa nafasi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mipyä ya kutolea huduma za afya ili kukidhi mahitaji ya wananchi. Kutokana na changamoto hiyo Ofisi ya Mkoa wa Rukwa imeshapata eneo jipya la ukubwa wa hekari 100 lilitopo Milanzi ndani ya Manispaa ya Sumbawanga litakalotumika kwa ajili ya ujenzi wa hospitali mipyä ya rufaa ya mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi huu utaanza baada ya kumalizika ujenzi wa hospitali za rufaa katika mikoa mipyä ya Katavi, Songwe, Njombe, Simiyu na Geita.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bupe Mwakangata swalii nyongeza.

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza naipongeza Serikali kwa kutujengea hospitali za wilaya tatu katika Mkoa wa Rukwa, lakini katika hiso wilaya tatu bado wilaya moja ya Sumbawanga mjini haijapatiwa hospitali ya wilaya. Je, ni lini sasa itajengewa hospitali ya wilaya?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili ni lini Serikali sasa itapeleka fedha za ukarabati hospitali hii ya mkoa ambayo inatumika kwa sasa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Bupe Mwakangata kwa kazi nzuri ambayo anafanya katika kufuatilia upatikanaji wa huduma za afya katika Mkoa wa Rukwa hasa huduma ya afya ya mama na mtoto naamini wanawake wa Mkoa wa Rukwa wamemuona na wameiona kazi yake nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ni lini tutajenga hospitali ya wilaya katika wilaya moja ambayo hajapata hospitali, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kama alivyoeleza tumeanza hospitali 67 mwaka huu katika bajeti ziko hospitali 28 kwa hiyo, tuombe tu uvumilivu kwa wananchi ambao hawajapata hospitali moja ya wilaya, Serikali ya Awamu ya Tano ni Serikali ya vitendo ni Serikali ya kutekeleza kwa hiyo tutajenga hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini naomba nitoe angalizo kwa sababu pia tunataka kujenga hospitali mpya ya Mkoa wa Rukwa. Kwa hiyo, ningeomba subira tukimaliza ujenzi wa mikoa mitano mipyaa kutekeleza ilani hii ya uchaguzi 2015/2020. Kwa hiyo, ile hospitali ya mkoa sasa tutaikabidhi kwa hospitali ya manispaa ya Sumbawanga kama tulivyofanya kwa Shinyanga na Singida ndio tutafanya hivyo, tukimaliza hospitali mpya hizi zillizokuwa zinatumika za mikao zitakabidhiwa katika manispaa. Sasa ni lini tutapeleka fedha ya ukarabati tumepeata fedha takribani shilingi bilioni 14 kutoka mfuko wa Dunia wa kupambana na UKIMWI, TB na Malaria kwa hiyo tutapeleka Mkoa wa Rukwa kwa ajili ya kuboresha huduma za magonjwa ya dharura na ajali pia kuboresha huduma za ICU wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum pamoja na huduma za mama na mtoto.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Susan Lyimo swali la nyongeza.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi, ugonjwa wa Kansa unakuwa kwa kasi kubwa sana na Hospitali ya Rufaa ya KCMC imekuwa ikihudumia wagonjwa hao lakini tatizo kubwa sana na kilio kikubwa cha watu wa pale KCMC ni *bankerkwa* ajili ya kuweka mashine ya *Radiotherapy* kwa ajili ya mionzi ya watu wenye matatizo ya kansa. Je, ni lini sasa Serikali itatatua tatizo hilo hasa ikizingatiwa hata katika bajeti ya maendeleo mwaka huu fedha hizo hazijatengwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE

NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Suzan Lyimo kwa swali lake la nyongeza na kwa kweli amekuwa akifuatilia suala hili la upatikanaji wa *bankers* kwa ajili ya utoaji wa matibabu ya mionzi, *radiotherapy* katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini KCMC. Ni lini watu wa Kanda ya Ziwa ni mashahidi tunaenda hatua kwa hatua. Tumeanza kuweka huduma za mionzi katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa Bungando na sasa hivi karibia asilimia 95 ya wagonjwa wa Kanda ya Ziwa wanapata huduma za matibabu ya saratani *chemotherapy* na *radiotherapy* katika Hospitali ya Rufaa ya Bugando.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni lini tunaenda hatua kwa hatua tunahitaji takribani bilioni 9 na juzi nilikaa na timu yangu nikawaeleza tunaenda vizuri kwa upande wa Hospitali za Rufaa za Kanda na changamoto kubwa ya kanda ya KCMC kwa kweli nakubaliana na wewe ni *bankers*. Tukiweka *bankers* tutakuwa tumekamilisha kweli bajeti ya mwaka huu hatujaweka lakini kama unavyofahamu tunapata fedha kutoka vyanzo vingine mwenyewe pia ni mdau wa kanda ya Kaskazini. Kwa hiyo, tutahakikisha, Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kama najipendelea lakini tutahakikisha kwamba tunaweka *bankers* katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso swali la nyongeza.

MHE. SELEMAN M. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza Mkoa wa Katavi ni mkoa ambao hauna hospitali ya mkoa na unategemea sana Hospitali ya Manispaa ya Mpanda kwa ajili ya kutoa huduma kiasi kwamba wagonjwa wamekuwa wengi na kuifanya ile hospitali kuzidiwa. Je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka fedha kwa ajili ujenzi wa hospitali ya mkoa ili iweze kuendana na muda kwa wakati?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Moshi Kakoso kwa swali lake la nyongeza kuhusu ujenzi wa hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi. Na kama nilivyojibu katika swali la msingi kipaumbele chetu kama Serikali ni kukamilisha ujenzi wa Hospitali za Rufaa za mikoa katika mikoa mipyä ikiwemo Mkoa wa Katavi. Mheshimiwa Kakoso tayari timu yangu ilishafika Katavi mwezi uliopita na hivi leo nikitoka hapa naenda ofisini kwa ajili ya kusaini mikataba ya ujenzi wa hospitali ya Rufaa ya Katavi. Lakini tutaanza na majengo manne ya kipaumbele, tutaanza jengo la wagonjwa wa nje *OPD* tumelitengea takribani shilingi bilioni 3 tutajenga jengo kwa ajili ya huduma ya uzazi na watoto wachanga *maternity block* tumetenga 3.3 bilion, tutaweka jengo la *ICU* na *Theatre* na jengo la nne la kipaumbele ni jengo kwa ajili ya huduma za radiolojia na mionzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwatoe hofu wananchi wa Katavi kama tulivyoahidi kwenye llani ya Uchaguzi ya CCM Mheshimiwa Kakoso usiwe na shaka 2020 utasimama kifua mbele baada ya kuwa tumetekeleza llani ya Uchaguzi ya CCM kwa kujenga Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi. Kwa hiyo, takribani kuna kama bilioni 9 tumezitenga kwa ajili ya Katavi mwaka huu wa fedha 2019/2020.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tuendelee na swali linalofuata Mheshimiwa Sonia Jumaa Magogo Mbunge wa Viti Maalum sasa aulizwe swali lake.

Na. 289

Sheria Zinazomkandamiza Wanawake na Watoto

MHE. SONIA J. MAGOGO aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kubadilisha au kurekebisha sheria ambazo zinaonekana kuitwa na wakati au kuchochaea ukandamizaji kwa wa mama na mtoto?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sonia Jumaa Magogo Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikifanya tathmini na kuwasilisha baadhi ya sheria zenyе upungufu ili Bunge lako tukufu likiona inafaa kuzibadili au kufanya marekebisho ya sheria hizo. Serikali imefanya marekebisho ya baadhi ya sheria na kupitia Bunge hili marekebisho mbalimbali yamefanyika naomba kutoa mifano michache. Sheria ya makosa ya Jinai Sura ya 16 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002 kifungu cha 130(1)(2)(e) kinatoa adhabu ya kifungo cha miaka 30 jela au kifungo cha maisha kwa kosa la kujiamiana na mtoto wa chini ya umri wa miaka 18.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali imefanya marekebisho ya Sheria ya Elimu ya mwaka 1978 Sura ya 353 kifungu cha 60A(1)(2) na (3), inayotoa adhabu ya kifungo cha miaka 30 jela kwa mtu ye yote atakayempa mwanafunzi mimba. Marekebisho haya yanalenga kulinda haki ya mtoto wa kike kupata elimu, vilevile Serikali ilitunga Sheria ya Msaada wa Kisheria Na. 1 ya mwaka 2017 ambayo inasaidia upatikanaji wa msaada wa kisheria bure kwa wanawake na watoto wasio na uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na marekebisho ya sheria hizo zinazolenga kulinda haki na ustawi wa wanawake na watoto, Serikali imeandaa mpango kazi jumuishi wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto wa 2017/2018 - 2021/2022. Mpango huu wa kisekta unatekelezwa na wizara 11 chini ya uratibu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na wadau wengine wa wanawake na watoto.

Mpango huu una eneo mahususi linaloshughulika na utekelezaji wa sheria zinazohusu wanawake na watoto.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sonia Magogo swalii la nyongeza.

MHE. SONIA J. MAGOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Afya nina maswali mawili ya nyongeza. Mahakama kuu ilitamka kuwa vifungu vya Sheria ya Ndoa ambavyo vinaruhusu ndoa za utotoni havistahili kutumika hivyo vifanyiwe marekebisho ndani ya mwaka mmoja na kuweka umri wa miaka 18 kuwa ndio umri wa chini wa mtoto kuweza kuolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini Serikali kuitia Mwanasheria Mkuu illikata rufaa juu ya shauri hilo. Je, Serikali haioni kwa kukata rufaa inaendelea kukubali athari zinazompata mtoto kiafya na pia kuondoa haki ya fursa za kimaendeleo kwa mtoto?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, wanawake wengi wamekuwa wakipata shida sana pindi wanapotengana na wenza wao ama kupoteza wenza wao hasa wa vijijini na hii ni kutokana na kutokujua sheria mbalimbali na kupelekea watoto wengi kukosa haki zao za msingi kama afya, malazi, chakula na elimu.

Je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kutoa elimu kwa wanawake hawa kuanzia ngazi ya vijiili kuweza kuwasaidia watoto hawa kupata elimu kuanzia ngazi ya chini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Sonia Magogo kwa maswali yake mawili ya nyongeza. Suala la marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 maelezo yalishatolewa ndani ya Bunge lako

tukufu na Waziri wa Katiba na Sheria, kwa hiyo nisingependa kurudia maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kwa sababu suala hili sasa hivi liko chini ya Waziri wa Katiba na Sheria na ye ye ameahidi ndani ya Bunge lako tukufu kwamba linafanyiwa kazi. Suala la kutoa elimu kwa kina mama na watoto ambao wanapata matatizo au changamoto au haki zao mara wanapotengana na waume zao, kwa kweli niyashukuru sana Mashirika yasiyo ya Kiserikali yamekuwa yakifanya kazi kwa karibu sana na Serikali katika kutoa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya haki za wanawake na watoto katika ndoa na mara ambapo kunakuwa ndoa imevunjika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kama nilivyoeleza katika majibu yangu ya msingi tumepitisha Sheria ya *Legal Aid Act, No. 1* ya Mwaka 2017, na lengo letu kwa kweli ni kuhakikisha sasa wanawake hasa wa vijijini wanapata huduma za msaada wa kisheria pale ambapo kunakuwa na changamoto ndani ya ndoa. Mheshimiwa Sonia nikiri kwamba tutaongeza jitihada za kuelimisha jamii katika ngazi zote hasa katika ngazi ya vijijini ili kuhakikisha kwamba wanawake wanatambua haki zao. Pia tutawaelimisha na wanaume kwa sababu mwisho wa siku ili tuweze kupata mafanikio mazuri lazima tuwaelimishe na kuwashamasisha wanaume kuheshimu na kutambua haki za wanawake na watoto ndani ya ndoa na nje ya ndoa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, swali la nyongeza.

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kumekuwa na vitendo vingi vya unyanyasaji na hasa kwa watoto wadogo ambavyo haviripotiwi kabisa na akina mama kwa sababu ya kuogopa wakati mwingine usalama wao, lakini wengine pia kwa sababu ya kutojua haki zao za Kisheria. Sijui Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha akina mama wanapata elimu hiyo ili watoto wanapopata matatizo

ya kudhalilishwa waweze kuwa na ujasiri wa kuripoti vitendo hivyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, majibu.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini kwa swali lake la nyongeza kuhusu uwepo wa vitendo vyta ukatili dhidi ya watoto. Swali lake kwa ujumla anasema tuna mkakati gani wa kutoa elimu, nimetoa maelezo wakati najibu swali la Mheshimiwa Sonia Magogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kubwa tutaendelea na jitihada za kutoa elimu kwa jamii kuitia vyombo vyta habari hata ukiangalia TV, ukisikiliza radio na vipeperushi mbalimbali, tumekuwa tukichapisha juu ya suala hili la vitendo vyta ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Mkakati mwingine Mheshimiwa Mwakasaka ambao tunautumia, tuna namba ya simu bure 116 ambayo inatoa fursa kwa mtu ye yeyote na nitumie fursa hii kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba mwananchi ye yeyote ambaye ana tatizo la vitendo vyta ukatili dhidi ya watoto mnaweza mkajaribu hata sasa hivi kupiga namba 116 itapokelewa na taarifa dhidi ya vitendo hivyo inafika katika mahala, vyombo vyta Serikali na kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuameanzisha Madawati ya Jinsia na Watoto katika Jeshi la Polisi. Tuna madawati zaidi ya 350 ambayo kazi yake pia ni kutaka kutoa uhuru kwa wanawake na watoto kwenda kutoa taarifa juu ya vitendo vyta ukatili dhidi ya wanawake na watoto bila vikwazo vyovyyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema suala hili kwa kweli tutaendelea kulifanya kazi, nikiwa kama Waziri ninahusika na masuala ya haki na ustawi wa mtoto. Kwa kweli kuna ongezeko kubwa la vitendo vyta ukatili dhidi ya watoto, ubakaji na ulawiti umeendelea kuongezeka katika jitihada

zetu. Kwa hiyo, tuanze sisi ndani ya familia, kwa sababu vitendo hivi vinatokea pia katika familia husika, watu wa karibu ndiyo wanajihusisha kwa kiasi kikubwa na vitendo hivi vya ukatili dhidi ya watoto.

NAIBU SPIKA: Meshimiwa Joseph Roman Selasini, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kwanza nimpongeze Waziri kwa jitihada hizi za kuelimisha jamii kuhusu unyanyasaji wa watoto, lakini ni ukweli watoto wananyanyaswa kwa kiasi kikubwa sana. Watoto wa kiume wanalawitiwa, watoto wa kike wanaingiliwa na wengine wanaingiliwa kinyume na maumbile, sasa hii inatokana na ukimya wa sisi wazazi kwa jumla.

Sasa ni lini Serikali itaaniszha mkakati wa makusudi kabisa wa kutembelea haya mashule na kukaa na wazazi ili kuwaeleza jambo hili wazazi waondoe aibu na waongee na watoto wao kwa uwazi kabisa kuhusu jambo hili? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, majibu.

WAZIRI WA AFYA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Selasini kwa swali lake zuri la nyongeza hasa kwa kukiри kwamba jukumu la kwanza linaanza na sisi wazazi walezi. Tarehe 16 Juni, 2019 ambayo ni siku ya Mtoto wa Afrika, Serikali itazindua *agenda* ya Kitaifa kuhusu wajibu wa wazazi na walezi kwenye ulinzi na usalama wa mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ajenda hiyo lengo lake kubwa ni kutaka kwanza kuweka wajibu wa kwanza kwa mzazi mlezi kutimiza wajibu wake katika malezi, matunzo na usalama wa mtoto. Lakini kwamba pia kama alivyoeleza, hiyo ajenda pia itatuka sasa tuendelee kwenda katika shule mbalimbali za msingi na ndani ya Wizara tunafikiria katika

kila shule ya msingi na Serikali kuweka dawati la ulinzi na usalama wa mtoto. Kwa sababu pale mtoto amepata tatizo angalau anajua nitakimbia kwa mwalimu fulani ambaye naweza kujieleza kwa uhuru na kwa faragha na masuala yangu yakasikilizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe rai kwa wazazi wenzangu na mimi ni mzazi, pamoja na kazi kubwa tunayoifanya ya kutafuta shilingi lazima tutimize wajibu wetu kwa watoto wetu. Wazazi anaweza ikapita wiki mbili, wiki tatu hamuuilizi hata mtoto unaendeleaje, nimkuwa nikisema kila siku. Mimi namkagua binti yangu, lazima tufanye huo utaratibu hawa watoto wa miaka mitatu, minne, mitano angalau muingeshe hata mara moja kwa wiki utajua ana changamoto gani, ana matatizo gani, lakini tukiwa *busy* na kutafuta fedha kwa kweli watoto wanaharibika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naliongea hili kwa uchungu, kuna mtoto analawitiwa miezi mitatu mzazi hajui, unajiliza hivi huyu mtoto kweli ana wazazi na walezi. Kwa hiyo, nimshukuru sana Baba Mchungaji na tunaomba viongozi wa dini watusaidie, katika mahubiri yenu hebu tuhubiri tunaenda wapi kama kizazi, kama jamii ya Watanzania. Kwanini vitendo vya ubakaji na ulawiti dhidi ya watoto wa kike na wa kiume vinaendelea kuongezeka. Sheria peke yake hatuwezi kumaliza suala hili, lazima tutimize wajibu wetu kama wazazi na walezi kuhusu matunzo na usalama wa watoto wetu, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kwa makusudi kabisa nimewaruhusu wanaume ndo waulize maswali ya nyongeza kwa sababu huko kwenye jamii siyo kwamba wanapendelewa wanawake, lakini vitendo vingi vya namna hii vinafanywa na wanaume. Kwa hiyo, kinamama swalii hili mlisamehe kidogo kwa siku ya leo kina baba wametuwalishaa.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge wa Babati Mjini sasa aulize swalii lake. (*Makofii*)

Na. 290

Swali la Singu Estate Babati

MHE. PAULINE P. GEKUL aliuliza:-

Je, ni lini Shamba la Singu *Estate* litarudishwa kwa wananchi wa Kata ya Sigino kama alivyoahidi Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati alipofanya ziara katika Jimbo la Babati Mjini mwaka 2017?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)
aliuju:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge wa Babati Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shamba la Singu namba 679 lenye Hati namba 11837 ambalo ukubwa wake ni hekta 1,260 sawa na ekari 3,080 lipo kilomita tano kutoka Mji wa Babati Mkoani Manyara linamiliiki na Kampuni ya *Agric. Evolution (T) Co. Ltd.* Mnamo mwaka 2004 Mji wa Babati ulipandishwa hadhi na kuwa Halmashauri ya Mji, hatua iliyopelekea kubadilika kwa Sheria za uendeshaji wa Mamlaka hiyo na pia kuanzisha mchakato wa kubadilishwa kwa shamba hili kutoka matumizi ya kilimo na kuwa na matumizi mbalimbali ya kimji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria zilizotumika katika mchakato wa kubadilisha matumizi ya shamba la Singu zilimlazimu mmiliki wa shamba hilo kurejesha hati ya umiliki wa shamba ili liweze kubadilishwa kuwa na matumizi mbalimbali ya ardhi ya jumla. Baada ya hati hiyo kurejeshwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iliridhia mabadiliko hayo na kupitisha rasmi mpango wa kina wa matumizi ya ardhi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, makubaliano yaliyofanyika kati ya mwenye shamba, Halmashauri ya Mji na wananchi wa kijiji cha Singu ni kama ifuatavyo; kijiji kipatiwe ekari 50 kwa ajili ya huduma za jamii kama vile shule, zahanati na kadhalika ili ziwanufaishe wananchi wa Singu. Wananchi waliokuwa wamejenga ndani ya eneo la ekari 200 kwenye shamba hilo wasitolewe bali wapimiwe na kumilikishwa viwanja katika maeneo waliyojenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara aliyoifanya katika Kijiji cha Singu mwezi Agosti mwaka 2017, wananchi na uongozi wa kijiji kwa ujumla wao waliweza kuridhia uendelezaji wa eneo hilo kimji ili waweze kunufaika na huduma zitakazopatikana na kwamba wananchi wa Singu watapewa kipaumbele katika ugawaji wa viwanja hivyo. Kuanzia mwaka 2017 hadi sasa mambo yafuatayo yamefanyika;

- (i) Umeandaliwa mpango kabambe wa mji kwa miaka 20 ijayo ambapo Singu ilipangwa kama mji wa pembezoni;
- (ii) Umeandaliwa upangaji wa kina;
- (iii) Upimaji wa viwanja umefanyika;
- (iv) Utengenezaji wa barabara katika eneo la mradi umefanyika na;
- (v) Juhudi za usuluuhishi wa mgogoro kati ya Mwekezaji na wananchi wa Singu zimefanyika kupitia uongozi wa mkoa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na muafaka kupatikana na wananchi kupewa zaidi ya ekari 800 na kumilikishwa maeneo yao kisheria.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Pauline Gekul, swali la nyongeza.

PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru, sijui niseme nini katika hili swali, lakini naomba niseme mambo manne, la kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri

wataalam wako wamekupa majibu ya mwaka jana kuna mambo mengine mapya mazuri yamefanyika naomba tu niyoseme. La kwanza wananchi wamepimiwa maeneo yako, wameachiwa nyumba zao kila mtu nyumba yake amepimiwa; lakini la pili wananchi wamepewa zaidi ya ekari 829; lakini la tatu, wananchi walikuwa wanadai fidia ya umeme wa KV 400 wamelipwa fidia zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Ardhi Mheshimiwa Lukuvi alifika tarehe 06 Machi, mwaka huu akamaliza mgogoro huu ambao nimekuwa nikusema kwa miaka tisa (9). Naomba niipongeze Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kulimaliza hili, Mheshimiwa Waziri Mkuu nikupongeze, Mheshimiwa Waziri Lukuvi na timu yako na nkipongeze Chama cha Mapinduzi kwa kumaliza tatizo hili. Siyo kila jambo uulize swali, kwa mara ya kwanza leo napongeza Serikali na chama changu wananchi wa Babati tumeridhika, ahsanteni Mungu awabariki. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali la Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 291

Kuundwa tena kwa Bodi ya Korosho

MHE. SIKUDHANI Y.CHIKAMBO aliuliza:-

Serikali ilivunja Bodi ya Korosho na majukumu yake sasa yanatekelezwa na Bodi ya Mazao mchanganyiko:-

Je, ni lini Serikali itachukua hatua ya kuunda tena Bodi ya Korosho na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kama ilivyo kwa mazao mengine?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)

alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Korosho Tanzania imeanzishwa chini ya Kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya Mwaka 2009. Majukumu ya Bodi ya Korosho ni kusimamia na kuratibu uendeshaji wa tasnia ya korosho nchini ikiwa ni pamoja na uzalishaji, usindikaji na biashara ya korosho. Aidha, Serikali kuititia Waziri wa Kilimo kwa mujibu wa Kifungu cha 8 cha Sheria ya Tasnia ya Korosho kutoa maelekezo na mwongozo maalum kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa tasnia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli alitengua uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Bodi ya Korosho na kuivunja Bodi ya Wakurugenzi wa Bodi tarehe 10 Novemba, 2018 kwa kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Korosho ambaye ndiye Mtendaji Mkuu wa Bodi aliondolewa katika nafasi yake tarehe 26 Oktoba, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, si kweli kwamba Serikali ilivunja Bodi ya Korosho na majukumu yake kutekelezwa na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko. Bodi ya Nafaka ilianzishwa kwa Sheria Na. 19 ya Mwaka 2009 na inaendelea kutekeleza majukumu yake ya Kisheria ambayo ni pamoja na kufanya biashara ya kununua na kuuza nafaka na mazao mengine ndani na nje ya nchi ambapo imepewa jukumu maalum la kununua korosho. Mnamo tarehe 15 Aprili, 2019 Waziri wa Kilimo alimteua Kaimu Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Korosho na Wajumbe wa Bodi nane (8) wameshateuliwa kwa kipindi cha miaka mitatu. Bodi hiyo, inakamilisha muundo wake baada ya Mwenyekiti wake kuteuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakamilisha kuunda upya Bodi ya Wakurugenzi wa Bodi ya Korosho Tanzania. Uteuzi wa Wajumbe utatangazwa na Mamlaka za uteuzi muda mfupi ujao kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni zilizopo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sikudhani Y. Chikambo, swali la nyongeza.

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa moja ya majukumu ya Bodi ya Korosho ni kufanya biashara na kusimamia ubora wa korosho. Katika msimu wa 2018/2019 jukumu la kufanya biashara ya korosho lilitfanyika na Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Je, Serikali imejipangaje katika kuhakkisha msimu wa 2019/2020 jukumu hili linafanywa na Bodi ya Korosho?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika msimu wa 2017/2018 Bodi ya Korosho iliingia Mkataba na vikundi mbalimbali kuzalisha miche ya korosho na kupitia Bodi ya Korosho walifanya mikataba na vile vikundi. Mpaka hivi ninaposimama hapa, baadhi ya vikundi havijalipwa fedha zao. Je, ni lini sasa Serikali itawalipa wanavikundi wale ambao walizalisha miche ya korosho na miche ilisambazwa katika mikoa mbalimbali ili wapate fedha zao kama sehemu ya wajasiriamali? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, swali lake la kwanza anataka kujua kwamba jukumu mojawapo la Bodi ya Korosho ni kutaka kufanya biashara ya korosho. Nataka nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya kuwatetea wakulima wa korosho hususan watu wa Tunduru na Mkoa mzima wa Ruvuma na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu lake hili, kwanza nimwambie kwamba majukumu yake kama kwenye jibu langu la msingi nilivyo sema hayajaondolewa kwenye Bodi ya Korosho kwa sababu bodi hizi zina majukumu mawili tofauti. Jukumu la kufanya biashara ni jukumu la Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ambalo sasa anaponunua korosho ni jukumu lao la kimsingi la kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la Bodi ya Korosho ni kusimamia, ni waratibu, ni uratibu wa kusimamia biashara ya korosho na hili jukumu wanaendelea nalo kwamba wale waliobaki ambao menejimenti inaendelea kuratibu na mpaka sasa hivi inaratibu katika ubora wa biashara ya korosho pamoja na biashara nzima ya korosho na maandalizi ya msimu ujao wa korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swalii lake la pili, anataka kufahamu kwamba ni kweli kwamba mwaka 2017, sisi kama Serikali tuko katika programu ya kuendeleza zao la korosho ya miaka mitatu ya kuzalisha miche milioni 10 na kuigawa kwa mikoa mbalimbali inayolima korosho. Ni kweli Serikali tuliingia mkataba kupitia halmashauri mbalimbali na vikundi mbalimbali kwa ajili ya uzalishaji huo wa miche na mpaka sasa kuna baadhi ya mikoa sita tumeshalipa. Baadhi ya mikoa mingine ipo kwa sababu kwamba ulipaji huu utalipwa baada ya kufanya uhakiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ile mikoa yote ambayo imelipwa, ile mikoa imemaliza uhakika na hii mikoa ambayo bado haijalipwa itamaliza uhakiki haraka iwezekanavyo ili kuweza kuwalipa kuendeleza zao letu la korosho.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Augustine Vuma Holle Mbunge wa Kasulu Vijijini sasa aulize swalii lake.

Na. 292

Tatizo la Maji Kata ya Buhoro

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE aliuliza:-

Kata ya Buhoro Wilaya Kasulu ina shida kubwa ya maji:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapa mradi wa visima vikubwa viwili kwenye kijiji cha Shunga ili kuwasaidia akina mama wanaoteseka?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Augustine Vuma Holle Mbunge wa Kasulu Vijiji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa utekelezaji wa miradi ya maji kwa mwaka 2019/2020, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu imekiweka kijiji cha Shunga mionganii mwa vijiji vitakavyofanyiwa usanifu wa miradi wa maji. Aidha, mradi mkubwa wa maji kutoka chanzo chake kilichopo eneo la Jeshi la Mutabila kinalenga kuwapatia maji wananchi wa kijiji cha Shunga. Lengo la Serikali ni kuhakikisha wananchi wake wote wanapatiwa huduma hii muhimu ya maji safi na salama.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Augustine Holle Vuma, swali la nyongeza.

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza swali mpja la nyongeza. Kwa kuwa Jimbo la Kasulu Vijiji hasa Kata za Kalela, Kwaga, Rusesa, Muzye, Bugaga na Kagerankanda zina shida kubwa sana ya maji.

Je, Naibu Waziri yuko tayari kuongozana na mimi kwenda Jimbo la Kasulu Vijijini kabla ya Mwaka huu wa Fedha kuisha ili tuangalie ukubwa wa tatizo na ajionee na hatimaye tuweze kuwa na mkakati wa kumaliza tatizo hili la maji kama sio kupunguza? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya katika Jimbo lake lakini nataka nimhakikishie sisi kama Wizara ya Maji tumeiona hiyo changamoto katika Jimbo lake. Bunge lako tukufu limetuidhinishia zaidi ya milioni 987 katika kuhakikisha tunaenda kutatua tatizo la maji katika Jimbo la Kasulu Vijijini. Na ninataka nimhakikishie kama Naibu Waziri niko tayari kwenda katika Jimbo lake kuangalia namna gani tunaweza tukashirikiana kutatua tatizo la maji. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Phillip Mulugo, swali la nyongeza.

MHE. PHILIP A. MULUGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Songwe ilipokuwa Chunya kabla hatujagawana kulikuwa na mradi mkubwa wa maji kutoka kwenye miradi ya *World Bank* vijiji 10 kila halmashauri. Kijiji cha Chang'ombe ambacho Mheshimiwa Naibu Waziri ulikuja mwaka juzi mimi na wewe tukaenda ukahutubia na mukutano na ukawaahidi wale wananchi kwamba watapata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kulikuwa na tatizo kubwa la mkandarasi aliyekuwa bado kwenye Halmashauri ya Chunya kwamba kulikuwa na ubadhirifu wa fedha kwenye mradi wa Chang'ombe. Sasa mpaka leo hali iko hivyo hivyo na hata mwaka jana nimekuuliza swali ukasema kwamba

utalifanyia kazi. Naomba na leo nisisitize kwamba ni lini unakwenda kumwambia mkandarasi akamilishe kazi pale kijiji cha Chang'ombe Songwe? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mbunge. Kwanza nimpongeze kwa kazi nzuri ambayo nimeiona kwa macho katika Jimbo lake lakini kikubwa sisi kama Wizara ya Maji, jukumu letu ni kuhakikisha Watanzania wanapata huduma hii ya maji na maji ni uhaki na hayana mbadala. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwakweli tulishatoa agizo na kama agizo lazima litekelezeke. Nikuombe Mheshimiwa Mbunge baada ya saa saba tukutane ili tuweze kuchukua hatua katika kuhakikisha wananchi wako wananaufaika na mradi wa maji. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Pascal Haonga, swalii la nyongeza.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, Mbozi katika Kijiji cha Harungu Wilaya ya Mbozi tuna mradi mkubwa wa maji ambaao karibu milioni 600 ya *World Bank* na mradi huu una vituo kama 24 ilikuwa iwe na vituo 24 vya kuchotea maji lakini kwa bahati mbaya sana ule mradi wanasema kwamba umekamilika wakati vituo vinavyotoa maji kati ya 24 ni vituo vinne tu.

Je, Mheshimiwa Waziri, nini tamko lako kuhusu mradi huo ambaao ni wa fedha nyingi lakini vituo vingi havitoi maji na tenki lile linavuja?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kutupa taarifa. Nimuagize tu Mhandisi wa Mkoa wa Songwe

atupatie taarifa kama ulivyosema ili kuhakikisha kwamba tunalichukulia hatua haraka hili jambo. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba yake Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko.

Na. 293

Usambazaji wa Mabomba ya Maji – Mara

MHE. ESTHER N. MATIKO (K.n.y MHE. JOYCE B. SOKOMBI) aliuliza:-

Mkoa wa Mara unakabiliwa na changamoto za maji safi na salama kwa muda mrefu hasa katika Jimbo la Musoma Vijijini, Wilaya ya Bunda, Jimbo la Serengeti, Butiama na Rorya licha ya kwamba Mkoa huo umezungukwa na Ziwa Victoria

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inasambaza mabomba ya maji katika maeneo yenye ukosefu wa maji?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na washirika wa Maendeleo wanatekeleza mradi wa majisafi wa Mugango, Kiabakari na Butiama kwa gharama za dola za Kimarekani milioni 30.69. kwa sasa Serikali inakamilisha taratibu za manunuzi za kumpata mkandarasi na ujenzi unatarajiwaa kuanza katika mwaka huu wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zitakazotekelawa ni pamoja na ujenzi wa chanzo cha maji kutoka Ziwa Victoria, ujenzi wa mtambo wa kutibu maji, ujenzi wa matanki ya kuhifadhi maji, ujenzi wa ofisi ya mamlaka, ujenzi wa vituo vya kuchotea maji na ujenzi wa mabirika ya kunyweshea mifugo. Mradi huu unatarajiwa kujengwa ndani ya kipindi cha miaka miwili hadi kukamilika na utahudumia watu wapatao 164,924 katika Miji ya Mugango, Kiabakari, Butiama pamoja na vijiji 13 vilivyopo katika halmashauri ya Musoma Vijijini pamoja na Butiama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuptitia Wizara ya Maji ina mpango wa muda mrefu kwa wananchi waishio kwenye vijiji arobaini vilivyopo kandokando ya Ziwa Victoria kwenye Mkoa wa Mara ili kuhakikisha wanapata maji safi na salama. Wizara imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na hatua inayofuata ni kukamilisha usanifu wa kina wa miradi ya maji kwa ajili ya vijiji vyote 40.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali imefanya makubaliano na mtaalam mshauri ya kufanya utafiti na usanifu kuangalia uwezekano wa kuwapatia wananchi wengine zaidi huduma hii muhimu ya maji kutoka Ziwa Victoria.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swalilala nyongeza.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu, ameonesha m ikakati iliyopo kwa Butiama, Kiabakari, Mugango na Vijiji 13 vya Musoma Vijijini lakini katika swalilala msingi la Mheshimiwa Sokombi aliweza kuonesha adha ya maji Mkoa wa Mara na akataja na Serengeti. Ningependa kujua mkakati uliopo kwa Wilaya ya Serengeti hasa maeneo ya vijijini ambayo kwakweli wananchi wa pale hawana maji kabisa. Ni mkakati gani Serikali mko nao ikiwemo wa kupeleka visima maeneo ya Serengeti Vijijini, sio pale Serengeti Mji. Mkakati gani upo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili mwezi wa tatu wakati Mheshimiwa Naibu Waziri ukijibu swali langu kuhusiana na adha ya maji Tarime kwa muda mfupi wakati tukisubiria mradi unaotoka ziwa Victoria, niliweza kuulizia vile visima 23 ambavyo Serikali ilisema itakuja kuchimba na *DDCA* alikuwa ameshafanya usanifu wa awali. Ulinihakikishia kwamba sasa tatizo lilikuwa ni hela na ukaagiza *DDCA* waende. Lakini ninavyoongea sasahivi ni takriban mwezi mmoja na nusu unaenda bado *DDCA* hawajafika katika Tarime Mji kuhakikisha kwamba wanatuchimbia vile visima 23 wananchi wa maeneo ya pembezoni waweze kupata maji tukisubiria Mradi wa Ziwa Victoria.

Ni lini sasa wataenda? Maana mpaka sasa hivi *DDCA* hawajaenda. Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Matiko, dada yangu lakini kikubwa ninachotaka kukisema sisi kama Wizara ya Maji tunatambua changamoto, si Serengeti tu kwa maana ya Mkoa wa Mara na ndiyo maana katika Miji 28 ambayo tumeiorodhesha kwa ajili ya kutatua tatizo la maji tumeipa kipaumbele zaidi ya miji mitatu kwa maana ya Tarime, Mugumu ambayo ipo Serengeti lakini pia Rarya katika kuhakikisha tunatattua tatizo la maji. Nataka nikuhakikishie tumekwishesaini mkataba katika kuhakikisha utekelezaji huu unakwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia yale maeneo ambayo yapo kandokando na Ziwa Victoria hususan Vijiini tunafanya usanifu ili kuhakikisha vijiji vile ambavyo viro pembezoni na Ziwa Victoria ili viweze kupata huduma hii ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala zima la uchimbaji visima katika Jimbo lako la Tarime tulikwishaagiza na tumepeewa agizo hilo kuhakikisha kwamba linatekelezeka lakini kuna mabadiliko tu ya kiutendaji katika Wakala wetu

wa Maji na wa Uchimbaji Visima *DDCA* lakini sasa hivi ameshapatikana Mkurugenzi, tunamuagiza kwa mara nyingine aende kuchimba visima vile ili wananchi wale waeze kupata maji. Kuhusu mradi wako wa Salasala pia tumekwishawalipa. Tunamtaka mkandarasi atekeleze m radi ule na wananchi waweze kupata huduma ya maji safi na salama. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, swali la nyongeza.

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuitia Wizara ya Maji imejenga tanki kubwa la maji mjini Bagamoyo lenye takriban uwezo wa lita 6,000,000 lakini kwanza tunaishukuru sana Serikali kwa kutukumbuka kwa jambo hilo adhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ni kwamba faida ya tanki hili bado haijaweza kupatikana na kata nzima ya Kisutu, Kata ya Nianjema, Kata ya Magomeni na hata Kata ya Dunda zote kata hizi zinaendelea kupata tatizo la uhaba au kukosekana kwa maji safi na salama kwa sababu hakuna mtandao wa mabomba ya kusambazia maji hayo safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu, ni lini sasa Serikali kuitia Wizara ya Maji itaweka mtandao wa mabomba ya kusambaza maji katika kata zote hizi Mjini Bagamoyo. Nashukuru. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, amekuwa mfuutiliaji katika kuhakikisha anawasemea wananchi wake wa Bagamoyo ili waweze kupata huduma

hii muhimu sana ya maji na nataka nimhakikishie sisi kama viongozi wa Wizara hatutakuwa tayari kupoteza uhai wa wana Bagamoyo katika kuhakikisha wanapata huduma hii ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara ya Maji kupitia Mamlaka ya Usafi na Usafi wa Mazingira DAWASA tumeona haja kabisa ya kukabiliana na kutatua tatizo la maji kwa Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na mkoa wa Pwani. Lakini tumejenga matenki makubwa sana ya maji ikiwemo Bagamoyo zaidi ya milioni sita yote ni kuhakikisha kwamba tunatatua tatizo la maji. Lakini hii ni Awamu ya I ya ujenzi wa matenki, Awamu ya II ni suala zima za usambazaji. Tupo katika hatua ya kupata kibali katika kuhakikisha tunaanzisha sasa mtandao huu wa maeneo ambayo hayana maji, yanapatiwa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunalifanya hili kwa haraka kibali kipatikane ili wananchi wa maeneo ya Kisitu na maeneo mengine waweze kupata maji safi na salama na yenye kuwatoshaleza. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, swalii la nyongeza.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Naibu Spika, nilifikiri ni mfupi sana kuonekana, nakushukuru sana kwa kuniona. Ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji kwamba kuna mradi unaitwa Malama kule Hanang ambaou ungesaidia maji Masakta, Lambo na Maskaroda na umetengewa shilingi bilioni 1.2 miaka mitatu iliyopita lakini mpaka leo wale watu hawakunufaika na hizo hela zilizotengewa.

Naomba kujua ni lini kitafanyika ili Masakta, Lambo na Maksaroda waweze kupata maji? Nashukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge mama yangu Dkt. Mary Nagu ni mama wa pekee ambaye amekuwa akiwapigania sana wananchi wake katika kuhakikisha wanapata huduma hii muhimu sana ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie kwa kuwa mradi huu umekwihatengewa fedha wa Malama naomba nifanye mawasiliano na Katibu wangu Mkuu ili katika kuhakikisha tuangalie namna gani tunaweza kuuanza ili wananchi wake waweze kupata huduma hii muhimu sana ya maji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, swali la nyongeza.

MHE. HAWA S. MWAI FUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, Bwawa la Igombe katika Manispaa ya Tabora limejaa tope hivyo kusababisha upungufu wa maji katika manispaa hiyo. Aliyekuwa Waziri wa Maji Mheshimiwa Eng. kamwelwe aliahidi kupeleka fedha TOWASA ili kuweza kusaidia kuondoa tope na kufanya kina cha maji kuendelea kuwa kama kilivyokuwa hapo awali. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha hizo ili wananchi wa Tabora tuweze kupata maji kama illivyokuwa zamani. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri lakini nimtoe hofu, ahadi siku zote ni deni, sisi kama Wizara ya Maji tutatekeleza deni lile katika kuhakikisha kwamba tunatatua tatizo la maji. Lakini pia ninataka nimfahamishe kwamba sisi kama Serikali tunatekeleza zaidi ya mradi wa bilioni 600 ambaao tunatoa maji Ziwa Victoria kupeleka Tabora pamoja na Miji ya Igunga na Nzega yote ni katika kuhakikisha tunasaidia Mji wa Tabora uweze kupata huduma ya maji. Lakini kuhusu suala zima la ahadi ya

kupeleka fedha, ahadi iko pale pale tutatekeleza katika kuhakikisha bwawa la Igombe tunatatua tatizo lile.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Fred Atupele Mwakibete, swalii la nyongeza.

MHE. FRED A. MWAKIPETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa niweze kuuliza swalii moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wilaya ya Rungwe ni mionganoni mwa wilaya ambazo zina maji mengi ya kutosha na vyanzo vingi lakini wananchi wetu hawana maji ya kutosha. Je, ni lini Serikali itakamilisha miradi ambayo imeanzisha ya maji hususan miradi ya Mwakaleli I pamoja na miradi ya masoko na Kandete pamoja na Kata za Rwanwa. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu kwa swalii hilo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, kiukweli amekuwa mfuatiliaji hata wewe Naibu Spika, masuala ya masoko na maeneo mengine umekuwa mfuatiliaji na kutuulizwa maswali mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara Mheshimiwa Waziri alinituma, nimekwenda lakini pia Waziri mwenyewe amekwenda na tukawa na kikao cha pamoja na Mheshimiwa Mbunge na sasa hivi kuna kazi ambayo inaendelea kule Masoko. Nataka tumhakikishie sisi kama viongozi tutakuwa wafuatiliaji katika kuhakikisha miradi ile inakamilika kwa wakati na wananchi wake waweze kupata huduma hii muhimu ya maji. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda sasa aulize swalii lake. (*Makofi*)

Na. 294

Survey Ilifanyika Kuhusu Tatizo la Maji – Jimbo la Bunda

MHE. BONIPHACE M. GETERE aliuliza:-

Jimbo la Bunda hususan Kata saba za Mugeta, Mihinyo, Kitale, Nyamuswa, Nyamang'uta, Hunyari na Salama zinakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji ya kunywa; na Serikali ilishalionia hilo na kuwapeleka wataalam wake kufanya *survey* katika kata hizo:-

Je, baada ya *survey*hiyo nini kimeamuliwa na Serikali?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwitwa Getere, Mbunge wa Jimbo la Bunda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutatua tatizo la uhaba wa maji katika kata saba zilizopo Jimbo la Bunda, wataalam kutoka Wizara ya Maji kwa kushirikiana na wataalam kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Bunda walifanya upimaji (*survey*) katika vijiji 23 vilivyopo katika kata hizo. Matokeo ya upimaji yalionyesha ni maeneo 10 tu yenye uwezo wa kuhifadhi maji kati ya mita za ujazo 84,794 hadi 354,604. Maeneo hayo ni ya vijiji vya Tingirima, Salama A, Marembeka, Kambumbu, Bigegu, Mahanga, Mihingo, Nyaburundi, Rakana na Manchimweru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara imeweka mabwawa matano katika mpango ili kuanza utekelezaji wa mabwawa hayo ikiwemo Tingirima na Salama A. Aidha, kwa maeneo ambayo hayakufanikiwa kupata vyanzo hivyo vya mabwawa, Serikali

itaendelea na tafiti za kuangalia uwezekano wa kupata maji chini ya ardhi au kutumia chanzo cha ziwa Victoria.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza niishukuru Wizara ya Maji, Waziri wake, Naibu na Katibu Mkuu wake kufanya juhudhi hizo za kupeleka wataalam kwenye Jimbo hilo la Bunda ambalo lina uhaba mkubwa sana wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa maji yamepatikana katika maeneo 10 ambayo ameshayataja hapa awali na kwa kuwa hizi ahadi zimeanza 2016/2017 mpaka leo 2019. Swali langu la kwanza katika eneo hilo ni kwamba Wizara inazo fedha tayari za kutengeneza mradi wa kuchimba Malambo matano kwa mwaka huu au ni ahadi zile zile za mwaka uliopita? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Mheshimiwa Rais tarehe 6 Septemba, 2018 alifika kwenye Jimbo langu kwenye Kata ya Nyamuswa na akiwa Nyamuswa alipata kero kubwa sana ya maji kutoka kwa akinamama wa Nyamuswa ambao wanakabiliwa na kero kubwa sana ya maji. Aliagiza Waziri wa Maji tarehe 6 Septemba, 2018 kwamba baada ya wiki moja Waziri afike pale ahakikishe kwamba anakaa na wanakijiji wa pale akinamama na wadau wa maji wote kwenye Kata ya Nyamuswa kuhakikisha kwamba maji yanapatikana. Sasa ni miezi tisa, Waziri hajaenda pale lakini sio mbaya.

Je, Naibu Waziri ambaye uko sasa ambaye ni Waziri wewe sasa hivi, uko tayari kwenda Nyamuswa kushughulika na lile agizo la Rais? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, amekuwa mfuatiliaji mkubwa sana hususan katika suala la maji katika Jimbo lake la Bunda lakini nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge. Sisi ni Wizara ya Maji, sio Wizara ya Ukame na hii ni Serikali ya Awamu ya Tano ikiakidi inatekeleza na ikishindwa kutekeleza basi kuna kuwa na sababu mahsusni kabisa katika utekelezaji wake.

Nataka nimhakikishie na ndiyo maana tumetuma wataalam wetu ili kuhakikisha kwamba zile tathmini zilizofanyika ili tuanze utekelezaji ili wananchi wako waweze kupata huduma ya maji. Tunakuomba Mheshimiwa Mbunge utupe ushirikiano wa dhati ili tuhakikishe kwamba wananchi wako yale mabwawa matano tunakwenda kuchimba, ili wananchi waweze kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu kufanya ziara katika jimbo lake kwa Mheshimiwa Mbunge, niko tayari kabla ya Bunge, ili kuhakikisha tunakwenda kutatua tatizo hilo ambalo limeahidiwa. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Kibamba, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Kubenea.

Na. 295

Tatizo la Kukatika kwa Umeme

MHE. SAED A. KUBNEA (K.n.y. MHE. JOHN J. MNYIKA)
aliuliza:-

Bado tatizo la kupungua na kukatika kwa umeme bado linaendelea na baadhi ya maeneo hayajafikishiwa umeme mpaka sasa.

(a) Je, ni kwanini matatizo ya kukatika au kupungua kwa umeme katika Jimbo la Kibamba halijapatiwa ufumbuzi kinyume na Serikali ilivyoahidi?

(b) Je, ni maeneo gani katika Jimbo la Kibamba mpaka sasa TANESCO haijafikisha umeme na lini yatafikiwa?

(c) Je, kuna mkakati gani wa kupunguza gharama za wananchi kuunganisha umeme au kuwarejeshea wanapovuta wenyewe umbali mrefu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Kibamba lenye sehemu (a) (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kukatika kwa umeme katika Jimbo la Kibamba linatokana na zoezi la kuhamisha miundombinu ya umeme ili kupisha upanuzi wa barabara ya Dar es Salaam - Morogoro. Kwa sasa tatizo hilo limeitungua, baada ya zoezi hilo kukamilika kwa asilimia 97 na itakamilika mapema mwezi Juni, 2019. Hali ya upatikanji wa umeme katika Jimbo la Kibamba imeimalika kutokana na kukamilika kwa kazi ya kubadilisha nguzo mbovu na kukata miti kwenye mkuza wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 kutoka Ubungo hadi Kibamba. Villevile kupitia TANESCO imetenga shilingi bilioni 5 kwenye bajeti ya 2018/19 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Mloganzila, Luguruni, chenye uwezo wa MVA 90, kituo hiki kitasambza umeme katika maeneo mbalimbali ya Jimbo la Kibamba, ikiwa ni pamoja na Hospitali ya Mloganzila na hivyo kutatua tatizo la ongezeko la mahitaji ya umeme katika Jimbo la Kibamba.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Kibamba kuna baadhi ya maeneo ya ambayo hayajapatiwa huduma ya umeme ikiwa ni pamoja na maeneo ya Kibesa, Kisopwa, Kipera, King'azi, Msumi na baadhi ya maeneo ya Mpigi na Kwembe. Katika bajeti ya mwaka TANESCO ilienga shilingi

bilioni 3.78 kwa ajili ya kupeleka umeme katika maeneo ya Kwembe kwa Tendwa, Kwembe Kipera, Mbezi Luis, Kibwegere, Msakuzi, Mpigi CCM ya Zamani, Kibamba Delini, Mpiji, Kwembe, Msumi na King'azi. Kazi ya kupeleka umeme katika maeneo haya inaendelea na itakamilika mwezi Septemba, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yaliyosalia ya Kibesa, Kisopwa na Kipera, yatapatiwa umeme kuitia bajeti ya 2019/20.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Mwezi Desemba, 2013, Serikali kuitia *EWURA* ilipunguza gharama za kuunganisha umeme kutoka shilingi 385,682, hadi 272,000 kwa wateja wa njia moja wa mjini, aliye ndani ya mita 30 ikiwa ni punguzo la asilimia 30. Kanuni za Sheria ya Umeme Kifungu 131 ya mwaka 2008 zilitangaza katika gazeti la Serikali Na. 63 la Tarehe 4 Februari, 2011 zinaelekeza *TANESCO* na mteja kukubaliana namna ya kurejeshwa kwa gharama zilizotumika kujenga miundombinu ya umeme kama *TANESCO* haitakuwa na uwezo wa kibajeti kwa wakati huo kumfikishia mteja huduma ya umeme.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Saed Kubenea, swali la nyongeza.

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoka na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa miundombinu ya Dar es Salaam na ukatikaji wa umeme, *TANESCO* imekuwa haitoi taarifa ya kuwepo kwa tatizo la ukatikaji wa umeme katika baadhi ya maeneo ambayo miundombinu hiyo inatekelezwa, jambo ambalo linasabisha kuleta usumbufu mkubwa kwa wananchi wanaotumia umeme, lakini hasa katika maeneo ya umma, ikiwemo hospitali ya Sinza Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba miundombinu ya *TANESCO* haiathiriki ya umeme kutokana na utengenezaji wa barabara zinazotengenezwa katika eneo hilo la Dar es Salaam?

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika baadhi ya maeneo ya Dar es Salaam, ambayo hayapati umeme wa kutosha, ni pamoja na katika Jimbo la Mheshimiwa Mwita Mwaikwabe Waitara, Jimbo la Ukonga, Mheshimiwa Ndugulile Jimbo la Kigamboni, Mheshimiwa Kubenea mwenyewe Jimbo la Ubungo na Majimbi mengine likiwemo la Kibamba.

Sasa Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha Jiji la Dar es Salaam, ambalo ndiyo kitovu cha biashara, linapata umeme wa kutosha na wakati wote bila usumbufu wowote na hasa ukizingatia kwamba, mradi mkubwa wa umeme wa gesi uko Kinyerezi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati majibu!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Mheshimiwa Kubenea ameulizia taarifa, endapo, pindi umeme unapokatikatika. Nataka nimtaarifa Mheshimiwa Kubenea, kwamba Serikali kupitia *TANESCO* tulitoa maelekezo ya kutumia maendeleo ya teknolojia katika kuhakikisha wananchi inawafikia taarifa haraka na maendeleo hayo ni kupitia pia uundwaji wa *ma-group* mbalimbali na katika Mkoa wa Dar es Salaam, Kanda zote zimeundiwa *ma-group* na hata mimi mwenyewe nipo kwenye *group* la Kibamba la utoaji taarifa za huduma ya *TANESCO* na mikoa yeto ina *ma-group* ya *whatsap*.

Mheshimiwa Naibu Spika, na sambamba na hilo pia, hata katika kikao cha maafisa habari nchi nzima kilichofanyika Mwanza, Shirika la Umme *TANESCO* na Wizara ya Nishati ni miongoni mwa taasisi na Wizara zilizofanya vizuri

katika kuwahabarisha wananchi taarifa mbalimbali zinazohusiana na sekta ya nishati. Kwa hiyo, nataka niwape, pengine kama Mheshimiwa Mbunge hajaungwa kwenye haya ma-group nataka nielekeze kwamba Mbunge wa Ubungo sambamba na Wabunge wengine wote waungwe kwenye ma-group na viongozi wote ili iwe kiungo katika kutoa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ameulizia namna ya uboreshaji wa miundombinu ya usafiri wa umeme katika Mkoa wa Dar es Salaam. Nataka nimtaarifu Mheshimiwa Kubenea, katika Mkoa wa Dar es Salaam, kwanza kuna mradi mkubwa wa upanuzi wa Kituo cha Ubungo, kituo hiki kinapokea umeme kutoka mitambo ya Kidatu kwa msongo wa *kilo vote* 220 na inapoza kwenye mashine za *MVA* 125 na inafanya kwamba, *megawatts* 200 kusambaza katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na hilo, kituo hiki kinapokea umeme kutoka mitambo ya *SONGAS megawatts* 189, mitambo ya *Ubungo II megawatts* 129 na Kituo cha Tegeta *megawatts* 45. Mahitaji ya Mkoa wa Dar es Salaam ni *megawatts* 500, lakini Kituo cha Ubungo kina uwezo wa *megawatts* 655. Lakini lazima niseme kwamba mitambo hii inafanyiwa ukarabati, wakati mwingine inafikia ukomo, inatakiwa ibadilishwe vipuli, kwa hiyo, inapotokea hiyo, ndiyo maana changamoto ya kukatikakatika umeme kwa Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya nini? Serikali ya awamu ya tano kupitia *TANESCO* inaendelea na upanuzi wa Kituo cha Ubungo, imeshaaggzia na imefika mashine ya *MVA* 300 ambayo itaongeza *megawatts* 240 kwenye msongo wa kilovoti 132 na kufanya Mkoa wa Dar es Salaam kuwa na upatikanaji mkubwa wa *megawatts* za kutosha kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ameyataja Majimbo ya Ukonga, ametaja Jimbo la Kigamboni, kwamba lina changamoto. Nataka nimtaarifu, Waheshimiwa Wabunge

wa Majimbo haya, akiwemo Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Ndugulile, wamefanya jitihada kubwa ya kufuatilia maeneo ambayo hayana umeme na ndiyo maana Serikali ikabuni mradi wa *Peri-urban* na imetenga bilioni 86 na sasa hivi hatua iliyokuwepo ile mikataba ya wakabdarasi ilishafikishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, niwatoe hofu wakazi wa maeneo ya Ukonga, ambako mimi mwenyewe nimefanya ziara kata sita, ikiwemo Zingiziwa, Buyuni, Kivule, lakini pia maeneo ya Somangila, maeneo ya Pembamnazi, maeneo ya *Kisarawe II*, maeneo ya Msonga, maeneo ya Buyuni, yote hayo yametengewa bajeti na mradi utafanyika na kwa gharama za *REA* elfu 27. Wakazi wa Dar es Salaam wakae mkao wa tayari, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imejipanga kutekeleza miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimia Hongoli, swalii la nyongeza!

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swalii la ngongeza. Tatizo la umeme lililopo Kibamba linafanana kabisa na tatizo la umeme lililopo katika Jimbo la Lupembe Halmashauri ya Wilaya ya Njombe. Tuna vijiji 22 havina umeme, lakini tangu Januari, 2019 mkandarasi wa *REA* amesambaza umeme katika vijiji viwili kwenye vijiji hivyo viwili amesambaza kitongoji kimojakimoja. Kwa hiyo, nini kauli ya Serikali sasa kuhakikisha kwamba hivi vijiji 22 vinapelekewa umeme na kuhakikisha kwamba mkandarasi huyu anasambaza umeme kwa kasi ili vijiji vyote 22 viweze kupata umeme? Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati majibum kwa kifupi!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hongoli atakuwa shahidi, tulifanya ziara pamoa naye katika jimbo lake na nimpongeze kwa kazi nzuri anayoifanya, lakini nataka nimthibitishie mkandarasi JV Mufindi anaendelea na kazi, lakini nataka niwathibitishie Wabunge wote kwa sababu yapo maswali mengi ya Mradi

wa REA, kwamba Mradi wa REA bado mudo upo, inatarajiwa ikamilike Juni, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini kama Wizara Mhesimiwa Waziri wa Nishati ametoa maelekezo, miradi ikamilike ifikapo Septemba, 2019. Naomba nimuahidi Mheshimiwa Mbunge, tutaendelea kumsimamia mkandarsi kwa karibu na ukizingatia sasa hivi wakandarasi karibu wote wameshafanikiwa kupata vifaa vyote vya mradi.

Kwa hiyo, nimtoe hofu tu kwamba vijiji 22 vitakalika na kasha tutaanza tena REA Awamu ya III mzunguko wa pili kwa vijiji vyake vyote vilivyosalia, ili kulifanya jimbo lake ifikapo 2021 yote iwe imemeremeta. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge muda wetu umekwenda tutamalizia swalii la mwisho, Iakini Mheshimiwa Naibu Waziri, umezungumzia mradi wa maeneo ya pembezoni Dar es Salaam, nadhani huo mpango ungeenda maeneo yote kwa sababu la sivyo, Wabunge wote watakuwa wanauliza.

Yale maeneo ambayo yanafanana na kuwa pembezoni mwa miji na watu kutakiwa Kulipa elfu 27, iwe ni hiyo kwenye maeneo yote, kwa sababu la sivyo kila Mbunge ataleta maeneo kwamba kina mji halafu kuna maeneo ya pembezoni. Kwa hiyo, muangalie maeneo yote ya pambezoni nchi nzima iwe ni elfu 27 ili irahisishe utendajikazi wenu lakini pia watu waweze kupata umeme kwenye hayo maeneo. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge tumalizie swalii la mwisho la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Balozi, Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge, sasa aulize swalii lake.

Na. 296

Wahadhiri Kutoka Nje ya Nchi

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA aliuliza:-

Kumekuwa na utaratibu kwa Vyuo Vikuu Tanzania kuajiri Wahadhiri toka nje ya nchi kwa lengo la kukuza tafiti na taaluma katika vyuo hivyo:-

(a) Je, katika miaka 10 iliyopita, ni wahadhiri wangapi wameajiriwa katika Vyuo Vikuu Tanzania?

(b) Je, ni mafanikio gani kitaaluma na kiutafiti yameletwa na wahadhiri hao toka nje ya nchi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, (TAMISEMI) kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKAO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA K.n.y WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJI): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo Vikuu vimekuwa vikijiri wanataaluma kutoka nje kwa malengo ya kuboresha hali ya taaluma na kujiiimarisha katika masuala ya kiutafiti katika nyanja mabalimbali. Ajira ya wataalam wa kigeni hutolewa kwa kibali maalum na kwa mkataba kwa kuzingatia mahitaji ya utalamu yaliyopo katika chuo husika. Katika miaka 10 iliyopita, kati ya mwaka 2008 mpaka 2009, hadi 2018/2019, vyuo vikuu 17 yaani vya umma vinane na binafsi tisa, vilajiri wanataaluma wa kigeni 502. Aidha kutokana na jitihada za Serikali na vyuo vyenyewe kuendeleza wataalm wa ndani, wanataaluma wa kigeni wameendelea kupungua, hali

iliyodhihirishwa na idadi ya wanataaluma wa kigeni waliopo nchini sasa kubaki 151 tu, hadi kufikia mwaka 2018/2019.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio yaliyopatikana baada ya kuajiri wataalamu wageni ni pamoja na kupata wataalamu wa fani ambazo nchi hajajitoshereza, kuanzishwa kwa programu mpya katika vyuo mbalimbali, kusimamia tafiti za kitaaluma mbalimbali katika vyuo vilivyoajiri katika nyanja mbalimbali. Pia imesaidia kuwezesha uanzishwaji wa mashirikiano kati ya vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi na kuwezeshwaa kupatikanaji wa vifaa vya kisasa vya kitafiti vya kufundishia na kujifunzia na vya maabara. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kamala, swali la nyongeza!

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nina maswali mawili ya nyongeza. Utafiti uliofanywa na watafiti katika vyuo vikuu vya Tanzania umebainisha kwamba upungufu wa wahadhili katika vyuo vikuu kwa Tanzania ni asilimia 44, na umebainisha pia kwamba, chuo kama Muhimbili, kuna upungufu wa wahadhili asilimia 65, chuo kama cha Mbeya, kina upungufu wa wahadhili asilimia 54 na utafiti huo umebainisha pia, kati ya hao waliopo pamoja na upungufu huo, asilimia 53 tayari wameshastafu kwa sheria za sasa.

Je, Wizara iko tayari kutafakari upya uamuzi wa kwamba, wahadhili wakifikisha miaka 65 wastaifu na wasiongezewe mkataba?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa taasisi nyingi duniani zilishapandisha umri wa kustaafu, kwa mfano, *Nairobi University* umri wa kustaafu kwa maprofesa ni miaka 70 na baada ya hapo anaweza akaendelea kwa mkataba. Ujerumani hakuna neno kustaafu kwa maprofesa, ukistaafu unapewa cheo cha *Emeritus Professor*, unaendelea kufundisha na kutafiti mpaka pale utakaposema sasa umechoka, na Uingereza wamebadilisha sheria kabisa sheria

ya Bunge, neno kusitaafu katika kufundisha vyuo vikuu limefutwa kabisa, kwa sababu wamegundua akistaafu mmoja leo, inawachukua miaka 40 kuweza kutengeneza mtu kama huyo.

Je, Wizara iko tayari kufikiria na kujifunza kutoka kwa wenzetu? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa maswali hayo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKAO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA (K.n.y WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJI): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, Mheshimiwa Mbunge ametoa utafiti alioufanya na ninaomba niamini kwamba huyu ni Dokta na ni Balozi atakuwa amefanya utafiti wa kutosha, lakini tutaongezea kufanya ili kupata taarifa sahihi sana juu ya jambo hili. Lakini ni kweli kwamba wako wahadhili wengine wengi ambao wanastaafu wakiwa na umri wa kuweza kufanya kazi, hilo jambo ni ko wazi, hili jambo ni ushauri mzuri naomba tuupokee, tufanyie kazi tuone uwezo utakavyoruhusu, tutashauriana na tutaomba Mheshimiwa Mbunge kukutane zaidi katika jambo hili ili liweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakihi vilevile, pamoja na kwamba tunataka maprofesa hawa na wataalamu wengine waongezewe muda wa kufanya kazi, lakini tunao mpango pia wa Serikali wa kuendelea kusomesha wataalamu wetu ndani na nje ya nchi. Kwa mfano sasa hivi tunavyozungumza tuna wataamu 65 kati yao ni wadhamivu wanasoma nje ya nchi na watatu wanasoma katika udhamili. Kwa hiyo, tutataangalia namna ya kuweza kuongezea muda wa kufundisha wale hasa wenye uwezo wa kufanya kazi hiyo, na kwenye fani mahususi na jambo hili Serikali itakwenda kulifanyia kazi, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge muda wetu umekwenda, tumshamaliza kipindi chetu cha maswali. Nitaleta matangazo tuliyonayo leo hapa mezani, kwanza ni

matangazo ya wageni. Tutaanza na wageni walioko jukwaa la Mheshimiwa Spika, na tunao wageni saba wa Mheshimiwa Spika ambao ni viongozi wakuu wa Benki ya *NMB*. Tunayendugu Magreth ikongo ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi. (*Makofi*)

Tunaye pia Ndugu Peter Novat ambaye ni Mkoo wa Kitengo cha Digitali, Bidhaa na Mifumo. (*Makofi*)

Tunaye Ndugu Nenyuata Mejooli ambaye ni Mkoo wa Kitengo cha Huduma Shirikishi. (*Makofi*)

Yupo pia Ndugu Vicky Bushubo ambaye ni Mkoo wa Huduma kwa Serikali. (*Makofi*)

Tunaye pia Ndugu Nsolo Mlozi ambaye ni Meneja Kanda ya Kat. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge huyu pia ni mwandaaji wa *Capital City Marathon*, kwa wale ambao huwa wanakimbiakimbia hapa mjini. Wanafanya kazi nzuri, sisi wenye mazoezi tujitahidi jamani kwenda kuungana nao. (*Makofi*)

Tunaye pia Ndugu Grace Matemu ambaye ni Meneja Tawi la Bunge. (*Makofi/Vigelegele*)

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana, makofi hayo yanaashiria namna ambavyo Grace Matemu anafanya kazi nzuri kwenye hili tawi la kuwashudumia Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Viongozi wake wako hapa, kwa hiyo, naamini wanaelewa Wabunge wanamaanisha nini wakipiga makofi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge yupo pia ndugu Michael Mungure, ambaye ni Mkoo wa Idara ya Ukusanyaji na Malipo. (*Makofi*)

Karibuni sana Viongozi na Wafanyakazi wa *NMB* tunawashukuru kwa huduma nzuri mnayotoa hapa nchini, lakini pia hapa Bunge Kwa hiyo tunawashukuru sana.,

Tunao pia wageni wengine wa Mheshimiwa Spika na hawa ni wanafunzi 20 kutoka Wilaya ya Kongwa wanaosoma katika Vyuo Vikuu vya UDOM na St. John wakiongozwa na ndugu Bernard Mtachi ambaye ni Katibu wa Jumuia ya Wanavyuo Wilaya ya Kongwa, karibuni sana. (*Makofi*)

Yupo pia mgeni wangu kutoka Makongorosi Wilaya ya Chunya Mkoa wa Mbeya ambaye anaitwa ndugu Lawena Nsonda, karibu sana. Tunao pia wageni wa wawaheshimiwa Wabunge na tutaanza na wageni 26 wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu ambaye ni Naibu waziri wa Maliasili na Utalii na hawa ni viongozi na wachezaji wa timu ya mpira wa mguu ya *Geita Gold Football Club* wakiongozwa na ndugu Fadhili Hassan, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 31 wa Mheshimiwa Mwita Waitara ambaye ni Naibu Waziri, TAMISEMI ambao ni wanakwaya wa kanisa la Waadventista Wasabato kutoka Ukonga Jijini Dar es Salaam wakiongozwa ndugu Blandina Sanga, karibuni sana. Tunao pia wageni saba wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambaye Waziri wa Kilimo ambao ni wanafunzi wa Chuo Kiku cha Dodoma wakiongozwa na ndugu Olipa Lwinga, karibuni sana. Tunae pia mgeni mmoja Mheshimiwa Godluck Mlinga ambaye ni kiongozi wa Dini ya Kiislamu kutoka Ulanga Mkoa wa Morogoro na huhu anaitwa Sheikhe Nurdini Igangula, karibu sana. Tunao pia wageni saba wa Mheshimiwa Vedastus Mathayo ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimboni kwake Msoma Mjini Mkoa wa Mara wakiongozwa na ndugu John Obotto, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka ambao ni Katibu Mwenezi wa *CCM* Wilaya ya Tabora Mjini ndugu Ramadhan Rashid na Mwenyekiti wa *UVCCM* Wilaya ya Tabora Mjini ndugu Ibrahim Songolo, karibuni sana. Tunao pia wageni 41 wa Mheshimiwa Joram

Hongoli ambaao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotoka Mkoa wa Njombe wakiongozwa na ndugu Chaula Ernest, karibuni sana. Tunao pia wageni nane wa Mheshimiwa Catherine Ruge ambaao ni Viongozi wa Chadema kutoka Serengeti Mkoa wa Mara wakiongozwa na ndugu Julius Wambura, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Magdalena Sakaya ambayo ni viongozi wa CUF kutoka Kaliua Mkoa wa Tabora wakiongozwa na Ndugu Alfred Kafyeta, karibuni sana. Tunao pia wageni 70 wa Mheshimiwa Agness Mathew Marwa ambaao ni Madiwani, Wenyevit, na Makatibu wa UWT kutoka Wilaya ya Rorya Mkoa wa Mara wakiongozwa na Mheshimiwa Shelta Mang'era na Mheshimimiwa Adina Charles ambaao ni Madiwani, karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Agness Marwa. Nadhani Mheshimiwa Agness Marwa amevunja rekodi ya kuleta wageni hapa Bungeni, karibuni sana ndugu zetu kutoka Mara. (*Makofi/Vigelegele*)

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Allan Kiula, ambaao ni viongozi wa CCM Kata kutoka Mkalama Mkoa wa Singida karibuni sana. Tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Philipo Mulugo ambaao ni viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe Mkoani Songwe wakiongozwa na Mwenyekiti wa halmashauri hiyo ndugu Abraham Sambilii, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunae pia mgeni wa Mheshimiwa Kiteto Koshuma ambaye ni mdogo kutoka Mkoani Mtwara na ye ye anaitwa Kiteto Clara Koshuma, karibu sana. Tunao pia wageni sita wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula ambaao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana.

Waheshimiwa tunao pia wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo, tunao wanafunzi 85 kutoka Taasisi ya Uhasibu Tanzania T/A ya Jijini Dar es Salam wakiongozwa na Ndugu Endrew Zanny, karibuni sana. Tunao pia wanakwaya 37 wa Kwaya ya Vijana ya Kanisa ya Waadventista Wasabato kutoka Kihonda Mkoa wa Morogoro, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge hao ndiyo wageni tulionao siku ya leo, pia ninayo matangazo mengine, tangazo la kwanza linatoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania *TWPG*, Mwenyekiti wetu Mama Margaret Sitta anawatangazia Wabunge wote wanawake kwamba leo tarehe 24 Mei, 2019 kutakuwa na semina kwa ajili ya Wabunge wanawake wote Ukumbi wa Msekwa mara tu baada ya kuahirisha shughuli za Bunge.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wanawake saa saba baada ya kuahirisha shughuli za Bunge mnaalikwa na Mwenyekiti Ukumbi wa Msekwa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge ninalo pia tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge na hili ni tangizo la kuhusu Iftar siku ya leo na nadhani Mheshimiwa Susan Lyimo pengine hii taarifa alikuwa ameipata kabla.

Waheshimiwa Wabunge mnaalikwa kwenye *Iftar* iliyoandaliwa na Waziri wa Maliasili na Utalii leo Ijumaa tarehe 24 Mei, 2019 mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge saa 12 jioni Ifta hiyo itakuwa eneo la tafrija za Kibunge jirani na Zahanati ya Bunge pale ambapo ilifanyika Iftar ya Waziri Mkuu leo tutakuwa na Iftar ambayo imeandaliwa na Waziri wa Maliasili na Utalii.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa sana, baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Naibu Spika.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge bajeti yetu ya Maliasili na Utalii inatarajiwa kukamilishwa leo na orodha ya wachingiaji ni kubwa sasa, hakutakuwa na Miongozo, wala taarifa isipokuwa kuhusu utaratibu kama kuna kanuni imevunjwa. Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge tutaendelea, Katibu!

NDG.YONA KIRUMBI-KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Maliasili na Utalii

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na majadiliano na nimeletewa hapa majina kutoka kwenye vyama mbalimbali, lakini nimeletewa pia taarifa hapa inaonekana kuna wageni hawakuingizwa na Makatibu.

Wapo wageni wa Mheshimiwa Ally Ungando ambao ni viongozi wa Chama cha Walimu na wanaongozwa na Katibu na Mwenyekiti wa Chama cha Walimu Kibiti Rufiji, karibuni sana wageni wetu.

Waheshimiwa Wabunge tutaanza na mchangiaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Edward Mwalongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pudensiana Kikwembe, Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi ajiandae. (*Makofi*)

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nikushukuru sana kwa kunipa nafasi niwe mchangiaji wa kwanza kwa siku ya leo. Niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara ya Maliasili jinsi wanavyofanya kazi, ni kweli wameitia uhai Wizara ya Maliasili na kazi wanayofanya inaonekana kwa mapana na marefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Njombe Mjini nikisimama hapa ninaongelea sana sana mazao ya misitu na mazao ya misitu ninayoongelea mimi ni mbao. Wizara hii kama ingejikita kwenye uzalishaji wa mbao laini ingeliweza kuisadia Serikali kupata mapato makubwa sana. Lakini kwa bahati mbaya sana imeacha uzalishaji wa mbao unafanywa kienyeji sana, ukiangalia jinsi miti ilivyopandwa katika Jimbo la Njombe Mjini,

ukaangalia jinsi watu wanavyopasua kienyeji na kuacha west nyingi kwa maana ya kwamba upotevu wa mbao ni mkubwa sana na mbao zile kusafirishwa bila hata kufanyiwa *treatment* yoyote zinasafirishwa zikiwa ghafi pato kubwa la Serikali linapotea, wananchi wanakosa mapato, lakini na Serikali na yenye inakosa mapato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe sasa Serikali kupitia Wizara hii kwamba wahakikishe sasa wanafanya utaratibu wa kupata mashine zilizo bora ili kusaidia upasuaji wa mbao katika Jimbo la Njombe Mjini uwe wa kitaalam mbao zile tuwe kuzi-*treat*, tuweze kuzisafirisha na tuwe na mbao ambazo zina ubora wa hali ya juu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiacha suala la uzalishaji wa mbao nije kwenye suala la usafirishaji. Suala la usafirishaji wa mbao limekuwa ni kero kubwa sana kwa wafanyabiashara wote wanaosafirisha mbao, lakini hata kwa matumizi binafsi ya mbao. Usafirishaji wa mbao unapakia mbao kwenye gari ukimaliza kupakia mbao hizo saa 11 jioni huwezi kusafirisha, ikifika saa 12 ukitembeza gari lenye mzigo wa mbao lazima upigwe faini.

Ndugu zangu tunakwenda na maendeleo sasa, maendeleo yetu yanakwenda kwa kasi sana, hii biashara kusimamisha magari ya mizigo saa 12 jioni yasisafiri na mzigo halafu yaanze kusafiri kesho yake saa 12 ya asubuhi tunawasimasisha kwa ajili ya nini? Na hasa hasa hizi mbao za miti ya kupandwa kwanza anayesafirisha ana leseni, ana vibali vyote, amelipa ushuru, kila kitu amefanya, lakini bado ikifika saa 12 jioni lazima asimame mzigo ulale hapo na kesho asubuhi uanze kusafiri. Yaani gari la mzigo linalala kabla kuku hawaajaingia ndani na sisi tunatafuta maendeleo hatuwezi kufika kwa staili hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri unafanya kazi nzuri sana, Naibu Waziri unafanya kazi nzuri sana, Mkurugenzi wa *TFS* anafanya kazi nzuri sana na watu wake, lakini kwa hili kwa hili hebu angalieni mnafanyaje, vinginevyo leo shilingi hapa hamtoki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mwalikishi wa watu wa Njombe wenzangu tunaotoka Njombe na Iringa hatuwezi kukubali hili, tumekuwa tukiwaambieni mara kwa mara tunataka mbao zisafiri usiku na mchana watu wafanye biashara, biashara ifanyike, yaani haiwezekani mtu atoke na gari la mbao Njombe afike Mwanza baada ya siku nne wakati mwenzake aliyepakia viazi anafika Mwanza baada ya siku mbili hiyo haiwezekani kabisa. Lakini kwa kufanya hivyo kwa kuondoa utaratibu huo wa kutokusafiri usiku hakuna madhara ya aina yoyote kwa maana ya mapato ya Serikali, hakuna kodi itakayopungua, hakuna mapato ya aina yoyote yatakayopungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunawaombeni sana hakikisheni mnarekebisha huu utaraibu haraka iwezekanavyo ili wafanyabiashara wa mbao na mazao mengine ya misitu ziklwemo mijengo, ziklwemo kuni, ukiwemo na mkaa. Tunalalamika misitu inaharibika, lakini tunawacheleweshea watu nishati Njombe sisi tuna miti maalum ya mkaa ya kupandwa, inaitwa uoto, au milingo. Ile miti ukitengeza mkaa ndiyo unaotumika katika familia mbalimbali watu mkaa wanataka kusafirisha wapelekee watu wasio na mkaa ili waokoe misitu sehemu nyingine ninyi mnasimamisha gari isitembee mkaa unalala watu wanashindwa kupata mkaa wa miti ya kupandwa matokeo yake wanatumia nishati nyingine, lakini wanakata miti ambayo ni miti ya asili niwaombe sana.,

Mheshimiwa Naibu Spika, katika zoezi hili la miti ya mkaa ningeliomba sana Wizara hii kwa sababu yenewe ndiyo inashughulika na upandaji wa miti na ndiyo inayoshughulika kuhamasisha utunzaji wa mazingira na kutokata miti ya asili kwa kuwa Njombe sasa sisi tuna miti inayofaa kwa mkaa na tumekuwa tukipanda miaka yote. Lakini sasa hatuna uwezeshaji wa aina yoyote ile tunafanya wenyewe kama wananchi tumekuwa tukijitahidi na wananchi wa Njombe niwaambieni, wananchi wa Njombe hawatumi kazi, wananchi wa Njombe wanafanya hawana kikao na mtu kwenye suala la kazi, suala la bidii, suala la kilimo, suala la upandaji wa miti hawashauriani mtu yoyote wao

wanajua ratiba yao ya maisha ya kila siku ni kupanda miti kwa ajili ya maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe sasa wataalam wa *TFS* na Wizara hebu jikiteni Njombe mpate miti mingi ipandwe kwa ajili ya mkaa ili kusudi wananchi wa nchi hii waweze kupata mkaa kutoka kwenye miti ya kupandwa badala ya kupata mkaa kutoka kwenye miti ya asili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tena kusisitiza suala la usafiri na usafirishaji wa mazao ya msitu ya mbao ya kupandwa. Nimuombe sana Mheshimiwa Waziri na watu wake wajitahidi kadri wanavyoweza leo atakapokuwa anahitimisha taarifa yake aseme lolote lile linalowezekana kuhakikisha kwamba mbao zinaweza kusafiri usiku na mchana; wakati huo wa zamani, kwanza sheria ukiangalia utaratibu huu wa kizamani sana wakati nchi haijaendelea, barabara hazijafunguka, hasa manufaaa ya kufungua barabara ni nini? Kama tumefungua barabara ya Dodoma, Iringa imekuwa ya lami lahafu unalaza mzigo Mtela maana yake nini, kuna maana ya, lazima tuone haya maendeleo mengine yaliyopatikana lazima kila Wizara sasa iyapokee iyatumie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *TFS* bado hamjatumia fursa hiyo ya kufunguka kwa barabara zetu, *TFS* hamjatumia fursa hiyo ya magari makubwa kuwepo ndani ya nchi yetu. Nakumbuka miaka ya zamani kama miaka kumi, 15 iliyopita gari kubwa kabisa lilikuwa ni Bedford au Isuzu, ilikuwa inabeba mbao 500, mabao 100, 250. Lakini leo gari inabeba bao 3,000 tumefanya maendeleo halafu unalilaza njiani tena unachelewesha maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe sana na kwa kufanya hivyo mtawapunguzia gharama wasafirishaji, moja kwa moja mtawapunguzia gharama wananchi, pia mtaifanya nchi ipate fedha nydingi kwa sababu gari linapotembea linakwenda lina rudi, linakwenda linarudi, linatumia mafuta na kwenye mafuta kuna ushuru wa Serikali.

Kwa hiyo, mtakuwa mmeisaidia Serikali kupata mapato zaidi; kwa hiyo, niwaombe sana mlione hilo na mlifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa nafasi naunga mkono hoja, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Jemsi Mbatia, Mheshimiwa Catherine Ruge ajiandae.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipatia niweze kuchangia katika hotuba hii ya Maliasili na Utalii. Kwanza kabisa napenda niwapongeze Mawaziri wote na viongozi wote wa Wizara chini ya Serikali ya Awamu ya Tano kwa namna ambavyo mmekuwa mkifanya kazi kwa bidii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende moja kwa moja katika Sheria ambayo inaongelea mazao ya misitu ambayo ni Sheria ambayo inasema kwamba ni *The Forest Act Cap 323* ni Sheria ya *TFS agency* ambayo *schedule* yake namba 8 na 14 zilizofanywa marekebisho kwa mwaka 2017.

Mheshimia Naibu Spika, naomba niende moja kwa moja kwenye fees na *loyalty for forest product and services*. Nimesimama hapa kutokana na malalamiko ya wananchi amba Sheria hii imekuwa kwao ni kandamizi, imekuwa kwao ikiwaonea na kama ilikuwa ikifanya kazi kipindi kile kwa sasa hivi nafikiri haiko sawa sawa. Kwa hiyo ni vyema sasa niiombe Wizara waweze kuileta hii Sheria tuweze kuifanyia marekebisho iende na wakati kutokana na kwamba Mheshimiwa Rais amekwishatamka tozo zozote na feesozote tunazoona kwamba zinawakandamiza wananchi tuzirekebishe ili tuweze kuendelea kupata mapato kwa urahisi na kwa wingi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano ninaongea nini *shattery* milango kwa one piece *shattery* mlango, kutoka Mpanda Mjini kwenda Jimboni kwangu Kavuu halmashauri moja kwenda halmashauri nyingine wanatozwa per piece

one shatter shilingi 50,500. Fremu moja ya mlango ama dirisha moja kutoka Mpanda Mjini kwenda Jimboni kwangu Kavuu shilingi 51,800, wakati *shatter* ya mlango pale Mpanda ataitengeneza kwa shilingi 22,000, mnamtoza 50,000 bado hajasafirisha kwenye gari kutoka Mpanda kwenda wapi kwenda Kavuu. Hii maana yake nini, maana yake mnawaambia wananchi wangu wa Kavuu hawapaswi kutoka kwenye umaskini kwenda kwenye kima cha kat, kwa maana kwamba lengo tunataka kujenga uchumi wa kima cha kat.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni lazima sasa hizi *fees* tuziangalie, lakini utakuta kuna kitanda shilingi 20,000, uyoga shilingi 200, sasa yaani unashindwa kuelewa, kiti ama stuli shilingi 17,250, dawati la shule mzazi ametengeneza dawati anapeleka kule Kavuu shilingi 17,250 kutoka halmashauri kwenda halmashauri yaani inamaana hizi ni *fees* ndani ya Mkao mmoja. Kitu ambacho nafikiri ilikuwa imewekwa kwa ajili ya ku-*discouragelabda* wale wafanyabiashara wakubwa wanaosafirisha mininga labda kutoka Inyonga kule kupeleka Mkao mwagine na kwamba Mkao mwagine unazilipia hiso *fees*.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana mfano mkeka ama kikapu unaambiwa ulipe shilingi 1,700, vitu vidogo vidogo vinavyotokana na mbao nikimaanisha labda mwiko, kijiko kwamba shilingi 1,700. Sasa nashindwa kuelewa, kama tunaona hizi zimekuwa ni kero naomba tuziondoshe kama Rais anavyoelekeza ili wananchi waweze kulipa vizuri na tuweze kuongeza mapato kwa wingi kwa sababu haiwezekani ndani ya Mkao uka-*charge* hivi vitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mila na desturi, binti anapoolewa anapewa kitanda, anapewa sofa, atapewa godoro hivyo vitu vyote lazima alipie sasa inakuwa kwa kweli haiteti maana kabisa hata kidogo. Ukizingatia kwangu ni halmashauri mpya sitarajii na wala hatutarajii kuwe mafundi wengi wa kusema kwamba kule watajitosheleza wasiweze kusafisha, kwanza Mininga sasa hivi hakuna ndiyo tunaanza kusubiria ianze kuota upya kwahiyio naomba sana muangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba nikumbushie tena kuhusu suala langu katika Kata ya Mwamapuli, Kata Luchima, Kata ya Majimoto Kijiji cha Luchima; pale tuliwaomba na *TANAPA* wamekwishaanza kutengeneza kisima kile. Naomba kisima kile kimaliziwe ili tuondoe mgogoro kati ya wananchi wanaotumia maji katika ule mto unaopakana na mbuga. Wananchi wamekuwa wakipigwa sana na Askari wa *TANAPA* na nimekwishaongea na wamekwishaanza kwanini hawamalizii kile kisima ili tuondoe migogoro inayotokea kati ya Wannachi pamoja na hao watu wa *TANAPA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini naomba niulize na naomba tena niongelee suala lingine; Askari wa *TANAPA* kati ya mwaka juzi na mwaka jana katika Kata ya Kibaoni walimonga Mama mmoja pale na kwa bahati nzuri nafikiri nilikuwepo Jimboni yule Mama alifariki pale pale. Sasa naomba nielewe ni fidia ili mtampa yule Baba, huyo ni Mzee pale anaitwa Mzee Lusambo mke wake ndiye aliyegongwa na gari na wale *TANAPA* hawakusimama walipitiliza walichofanya ni kusaidia tu maziko. Kwa hiyo, nilikuwa naomba ni namna gani huyu Mzee Lusambo sasa kupitia kifo cha mke wake mtampa fidia ili naye aweze kuona kwamba angalau Serikali imeweza kumjali kwa sababu wanapita kwa *speed* kali kiasi kwamba inabidi muwe waangalifu na kuangalia namna ambavyo mtavuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nirejee katika kisima change cha Luchima, naomba kikamilike na ikiwezekana kikamilike mapema iwezekanavyo, Mheshimiwa Naibu Waziri uliniambia kwamba umekwishaongea na watu wa *TANAPA* na najua wako hapa, Mkurugenzi Kijazi yuko hapa, naomba sasa umuelekeze kile kisima kiishe haraka iwezekanavyo kabla ya Septemba kiwe kimekwisha na Wananchi waanze kutumia maji yale kuepuka vurugu ambazo wanazipata kutohana na Askari wa *TANAPA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sina mengi zaidi ya kuiomba Serikali ilete hiyo Sheria ili tuweze kuifanyia marekebisho Wananchi waweze kunufaika na

mazao na vitu vyao wanavyosafirisha. Meza imekwishatumika una sababu gani ya kum-*charge* mtu wakati ana hama kutoka halmashauri moja kwenda halmashauri nyingine? Na siyo kitu kipywa na wala hakijazidi hata tani moja kwanini um-*charge*? Kwa hiyo, hizo ndiyo kero ambazo naziwakilisha kutoka kwa Wananchi wangu wa Jimbo la Kavuu ambao wamekuwa wakilalamika kila siku namna wanavyo hapa kutoka Mpanda Mjini kwenda Kavuu kwa ajili ya kufanya shughuli zao za maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipatia nafasi hii, naunga mkono hoja, naomba Serikali mzingatie haya yote niliyokwisha waeleza, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi atafuatiwa na Mheshimiwa James Mbatia, Mheshimiwa Catherine Ruge ajiandae. Mheshimiwa Dkt. Semesi dakika tano.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita katika sekta ya misitu kwa sababu sekta hii ni muhimu sana kwa uhai wetu na kwa uhai wa Nchi yetu kwa masuala ya kijamii pamoja na kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali yetu kuhusu suala la misitu iko bado tete sana kwa sababu zaidi ya asilimia 90 ya nchini kwetu tunategemea bidhaa zinazotokana na misitu hususani kwa shughuli za Nishati aidha kwa kutumia kuni au shughuli za mikaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuna suala zima la Sheria ambazo zinaangalia sekta hii kwa ujumla ambazo zinajikanganya inavyoshughulikia misitu yetu. Tuna Sheria mbalimbali mfano, *The Local Government Finance Act* na *Mining act* nafikiri mwaka jana tulifanya marekebisho katika

Mining Act na *Finance Act* kwenye masuala ya uvunaji wa chumvi katika maeneo hususani ya mwambao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kule maeneo ya mwambao tuna misitu mahususi sana, misitu ya mikoko. Sasa baada ya kufuta taratibu ambazo zinashughulikiana na mazingira, watumiaji au *mining* katika maemeo haya imekuwa kubwa sana na mikoko hii imekuwa ikikatwa kwa kasi sana na misitu hii ni muhimu sana katika utunzaji wa mazingira na inasaidia kutu-*shield*na zile dhoruba za baharini. Sasa tunapozidi kuikata hii miti tunazidi kujiweka katika mazingira hatarishi pale tunapopata dhoruba kama wenzetu wa Mozambique hiki kimbunga kilichopita kwa bahari nzuri hakikutupata ilihali ingetupata basi madhara yake yangekuwa makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Sheria yetu ya Mipango Miji ya mwaka 1982 inakataza shughuli za kilimo na upandaji wa miti kwa ujumla wake katika maeneo ya miji. Sasa nafikiri Sheria hii iangaliwe upya kwasababu unapokuwa na miti au misitu tunasema maeneo ya Miji tunasema ni mapori lazima yaondolewe. Lazima tuliangalie hili kwa ukubwa wake na mapana yake na *effect* ambazo zinaweza zikajitokeza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nigusie suala la biashara la soko la mbao Nchini; biashara hii inaweza ikatuinua kiuchumi, tunaongelea mabilioni ya Dola za Kimarekani katika biashara hii lakini biashara hii kwa sasa hivi imekuwa kama biashara haramu ambapo tunavuna sana kuliko kuangalia uvunaji endelevu na jinsi soko hili linavyotakiwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba suala la biashara la soko la mbao Nchini liangaliwe na pia tuweze kuviedeleza viwanda vyetu vya ndani vya kutumia mbao viweze kutumia mbao yenyewe kama mbao hata zile *by product* nazo ziweze kuzalisha na kuleta manufaa kiuchumi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nigosie suala la *TFS*; *TFS*sasa hivi ni kama *agency*. Naomba kulia mkazo kwamba sasa igeuke kuwa *regulatory authority* najua mchakato unaendelea basi naomba ufanywe kwa haraka ili *TFS* iweze kusimamia masuala yote ya mazingira na miti maeneo ya mijini, vijijini, halmashauri wawe na *authority* ya kuweza *to regulate* na siyo kuingilia Sheria na Sera mbalimbali ambazo zinawakwaza wao sasa hivi kutekelza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuangalia umuhimu wa misitu Nchini na Nchi zinazotuzunguka, Tanzania imeingia maridhiano na makubaliano mbalimbali ya Kimataifa basi naomba Tanzana sasa ijikite na iwe *reflected* kwenye bajeti na watupe *update*. Kwa mfano, hapa hapa Nchini tumeingia mkataba wa Zanzibar *declaration status* iko wapi hususani katika soko la biashara ya mbaao, *African forest scape restoration borne challenge* na *UN-CCD* sasa Tazania imesimama vipi ili kuweza kuboresha hali ya miwitu yetu Nchini? Tunaomba Mheshimiwa Waziri anapohitimisha basi atupe *status* yetu ikoje au kuna vikwazo gani ili Bunge hili liweze kusaidia kuweka mambo vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nigosie *status* ya *Community base forest management*; najua kuna *policy* mahali sjui imeishia wapi sasa uharibifu mkubwa wa mazingira haya ya misitu yanatokea katika vijiji vyetu. Vijiji tumevipa mamlaka, naomba Serikali husika, Wizara husika iangalie masuala ya Vijiji vinasimamiaje misitu ili viwe endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa James Mbatia nilikuwa nimekutaja, Mheshimiwa Catherine Ruge nilisema utafuata baada ya huyo lakini kuna watu wana dharura kidogo utavulimia, atafuatia Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mheshimiwa Yussuf ajiandae. Mheshimiwa Mbatia dakika saba.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, kwanza nitoe pole kwa shule ya Wasichana ya

Ashira Mabweni yao yameungua moto jana na wanafunzi zaidi ya 100 hawako kwenye hali nzuri na eneo hili linapakana na Mlima Kilimanjaro kwa hiyo, niombe na *TANAPA* pia waweze kuangalia ni namna gani tunaweza tukashirikiana katika kurudisha hadhi ya shule yetu ya Ashira ili iweze kuwa kwenye hali nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoepongezi kwa *TANAPA* kwa kazi nzuri wanayoifanya na ujirani mwema wa vijiji 88 vya Mkoa wa Kilimanjaro kupitia *KINAPA* wamefanyakazi nzuri na wameshirikiana na Vunjo *development foundation (VDF)* pamoja na Ofisi ya Mbunge tumeweza kutengeneza barabara zaidi ya kilometra tisa kwa hivyo niwapongeze sana *TANAPA* kupitia Mkurugenzi wake Kijazi na Mwenyekiti wa Bodi Gen. Waitara na wote pamoja na Sakayo Mosha sekondari imejengwa vizuri, Zahanati ya Kitoo wanafanyakazi nzuri na mtu akifanyakazi nzuri yapasa kumpongeza, tunawapongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tabia yetu sisi Watanzania kwenye sekta ya utalii badala ya kuuza utalii au kuza huduma tunauza neno "samahani". Huduma vigezo vyetu au uwezo wetu wa kutoa huduma unavyokuwa chini badala ya kuona namna gani ya kuboresha kutoa viwe kwenye *standard* tunatoa neno "samahani" hasa kwenye mahoteli yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitasema kwanini nasema hivyo; kwanza sekta ya utalii ndiyo sekta kuu inayoongeza fedha za kigeni hapa Nchini. Asilimia 25 ya *forex* yote inatokana na utalii sasa tuisiangalie ugali wa leo tu, nitumie lugha rahisi, tuangalie kesho. Nasema hivyo kwa sababu ukiangalia bajeti ya Wizara hii ni bilioni 120, fedha za maendeleo ni bilioni moja tu za ndani za nje ni bilioni 47.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiangalia maduhuli na mwaka jana niliomba tena, ukiangalia maduhuli yanayotokana kwa mfano na *TANAPA* peke yake mwaka jana ilikuwa zaidi ya bilioni 292. Unamlisha Ng'ombe vizuri ili umkamue vizuri na aweze kukuletea tija zaidi. sasa kwa kweli

bajeti ya Wizara hii ni kidogo sana. Kwa mfano, Bosi ya utalii, Jaji Thomas Mihayo ambaye ni Mwenyekiti na wenzake wanafanyakazi nzuri lakini tunawawezesha kiasi gani waweze wakatangaza utalii wetu? Fedha zinazotolewa kwenye kutangaza utalii, kwa mfano, tukijifunza kwa wenzetu wa Kenya ni zaidi ya Dola milioni 100 yaani zaidi ya bilioni 200 yaani fedha zote za bajeti ya Wizara hii hazitoshelezi kuutangaza utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine nipayendekeze tu; maduhuli yanayotokana na Wizara hii Serikali ione umuhimu wa kuacha ndani ya Wizara angalau kwa miaka mitano ili Wizara iweze ikakua na *GDP*yake iweze ikakua ili Taifa liweze likavuna zaidi kutokana na hali ya namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, viko vigezo vingi ambavyo vinarudisha nyuma utalii wetu. Kwa mfano, *work permit* za *expert* kama kuna wafanyakazi 100, wafanyakazi wawili ambaoni *experts* au wataalam kwanini wasipewe mazingira rafiki ya kuweza kufanyakazi vizuri. Ubora wa vyakula vyetu, kwa mfano, lile katazo la vyakula vya mifugo au maziwa kutoka Kenya, kodi nyingi nyingi tuangalie ushindani zaidi kwenye *standardization, standards* zetu tuziboreshe zaidi ziashindane badala ya kuwelka *restrictions* ambazo siyo rafiki, utitiri wa kodi. Nipongeze Kambi ya Upinzani wameandika vizuri utitiri wa kodi uliopo, Kamati nayo imeandika vizuri pia, tuangalie utitiri mwingu sana kwenye kodi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matamkao yanayotolewa, Serikali ikitoa matamkoia iangalie sana. Kwa mfano, matamko ya magonjwa kama ya Dengue ambayo watalii wanaibebaje kwamba Tanzania tayari yote ina magonjwa ya namna hiyo wanaogopa hata kuja Tanzania. Hata hii mifuko ya *plastic* namna gani wanafanya *package, restrictions* ziko namna gani, tamko la Serikali liko namna gani kwa hivyo matamko haya tunayoyatoa lazima yaangalie kwa mapana yake, utalii Kusini na mazingira, *UNESCO* wako kwenye *position* gani tunaitangaza namna gani Dunia kwenye mambo ya namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu ukiamua kupanga vizuri, kwa mfano, Kilimanjaro marathon wakati wa *low season* ukaipanga kama ni *package* moja ya kuanzia unawaambia watalii wanakuja wanaanzia Arusha kwenye kuangalia wanyama Serengeti, wanakuja kwenye Kilimanjaro *marathon*, wanatoka kwenye Kilimanjaro *marathon* kwenye kukimbia huko wanakwenda Zanzibar (*Zanzibar music festival*) kwenye raha huko, wanakuja Dar es salaam, Dar es salaam wanaangalia biashara na Mji ulivyo, wanakwenda mbuga za Saadani-Bagamoyo kwahivyo inakuwa ni *package* moja na ukiipanga vizuri ni taaluma tu yaani inakuwa ni *tourist plan* ambayo ikiipanga *as a tour* moja faida yake ni kubwa kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, wataalam wapo, tuwawezeshe watalaam wetu waweze kuzifanya hizi *tourzikiweza* kuwa na hili *route* ikawa na manufaa na maslahi mapana kwa Taifa. Kwa mfano, kipindi cha *low season*, kwa mfano, *Easter time* ukasema wiki mbili nzima ni za *plan* nzima ambayo ina-*compensate* sio ina *compensate* ile zitakwenda sambamba na *high season*, ukimaliza kipindi cha *Easter high season* nayo inakuja kwa hivyo unakuta mwaka mzima utalii na tuweke *priority* kutokana na vivutio vyetu nya utalii. Kipaumbele kwenye eneo hili kwa ukubwa wake kiko hivi, kipaumbele kwenye eneo hili kiko hivi, eneo hili la kutangaza vivutio vile tulivyonyavyo yaani kwa lugha nyingine niseme *we must organize what we have and plan for it*, tu-*plan*, tu-*organize*, turatibu, tuweze kuelekeza na kuweza kutawala vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia watu kwa mfano, *European wana-route* zao wanazi-*plan* vizuri unaanzia Belgium, unakwenda France, unakwenda Spain, unakwenda Germany wanakuwa ni *package* moja sasa hapa kwetu na vivutio vingi hivi tulivyonyavyo nya utalii yata-*stick big*. Mheshimiwa Waziri naujua uwezo wako na mmetulia vizuri sana kwenye Wizara sasa hivi nikupongeze kwa hilo na ubinifu washirikishe wadau walio wengi, tuishirikishe Dunia, tushirikishe wawekezaji kwenye sekta hizi kwa sababu uwekezaji kwenye utalii pamoja na *communication* kwenye utalii ni watoto

pacha, wanarandana, wanaingiliana sasa namna gani unachukua wataalam hawa, kwa mfano, Makampuni ya humu ndani tukatumia...

Mheshimiwa Naibu Spika, dakika moja namalizia sekunde 30; Makamouni ya huku ndani yakatmika vizuri katika kuwekeza na kutangaza utalii badala ya Makapuni ya humu ndani kutumika na watu wa nje zaidi tuyawezeshe Makapuni ya ndani na wao waweze kuwekeza vizuri katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana Mwenyezi Mungu akubariki.

NAIBU SPIKA: Amina, ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Mbilinyi dakika tano atafuatiwa na Mheshimiwa Yussuf Hussein dakika tano, Mheshimiwa Catherine Ruge ajiandae.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, moja kwa moja nitakwenda ku-stress kwenye suala la utalii *Southern circuit* (Ukanda wa Kusini) naona mkazo bado kabisa. Wakati Mheshimiwa Waziri anazungumzia mafanikio ya watalii milioni 1.5 kwa mwaka jana walitembelea Tanzania ningependa aniambie katika hao milioni 1.5 ni watalii wangapi walikwenda kwenye ukanda wa Kusini ikiwemo Kitulo, Ruaha, Katavi, Selous na hata Mbeya kama Mbeya tuna maeneo kama Lake Ngozi, Lake Kisiba, tuna Matema *beach*, tuna Ngonga *beach* yote hayo ni maeneo ya vivutio vya watalii kwenye eneo lile la *Southern circuit*. Kwa hiyo, nilitaka kujua kwamba katika 1.5 million ni wangapi walikwenda kutembelea kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara kwa ile *branding* ya "Tanzania unforgettable" *it is a super thing*. Nilivyoiona tu ile kitu nikasema sasa Dkt. Kigwangala yuko kazini lakini *take it international; CNN, BBC* na kwenye *platform* zingine za Kimataifa na wewe mwenyewe pia *brothersafari* nenda Mamtoni, nenda Ulaya, nenda Marekani ukajue watalii wanataka nini ili uje uwaandalie hayo mazingira huko. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenda wewe mwenyewe tu kitalii Serengeti, kwenda wapi haisaidii kuvutia watalii wa Klmataifa ni sisi tu ambao tunakuwa na *Instagram* na maeneo mengine. Kwa hiyo *brother* utoke, uende Ulaya, uende Marekani ukajue watalii wanataka wanataka nini halafu sasa hii Tanzania *unforgettable* itakuwa imekaa sawa sawa na siyo ile *channel* yetu ya *TBC* ambayo tumeianzisha kutangaza utalii ambayo badala ya kutangaza utalii unakuta wanaonyesha miradi iliyofadhiliwa na *TANAPA* ya ujenzi wa vyoo na madarasa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hiyo inasaidia vipi katika kutangaza utalii tunasema wkamba tumeianzisha ile *channel* kwa ajili ya kutangaza utalii ile inasaidia vipi kuonyesha kwamba *TANAPA* wako pale? Au unaonyesha madaktari wa wanyama wanachoma Tembo sindano. Kuna watu ni waoga hawapendi kuona hata vidonda vya wanyama ukiwaonyesha vile unawaogopesaha hata kwenda tena kitalii kwahiyu tuonyesheni vitu vizuri, tuonyesheni wanyama, tuonyesheni Ngorongoro, tuonyesheni Serengeti kupitia hii Tanzania *unforgettable* na siyo vinginevyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tozo kwenye biashara; nitangaze *interest* kidogo, kwenye biashara za hoteli kama alivyoongea Mheshimiwa Lucy Uwenya jana tozo zimekuwa nyingi sana, unakaa mtu anapiga hodi mimi ni idara fulani nataka tozo, huyu anapiga hodi hatuwezi kwenda. Na tena ilitakiwa hoteli hizi mpya zinazoanza muwape nao kama miaka mitatu au *at least* miaka miwili ya *task* hizi tozo ili wakue kibiashara na hoteli zikikaa *standard* wakikua kibiashara huduma zikikaa sawasawa hao watalii mnaowavutia kuja watakuwa na sehemu sasa nzuri za kufikia, sehemu nzuri za kulala na si vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu jana amesema kwamba hizi tozo zitaondolewa naomba niiombe Serikali iondoe hizi tozo haraka sana kwa sababu matozo haya yamejazana katika biashara, sio tu biashara za hoteli hata biashara

nyingine tofauti tozo zimezidi saba nchi hii ndio maana biashara hazikui, tuondoe tozo katika hizi biashara watu waajiri wakishaajiri hata wale wafanyakazi wanalipa kodi *income task*, wanalipa nini nayo ni njia nyingine ya kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi kampuni au hizi biashara zinanunua bidhaa mbalimbali zinalipa kodi. *Brother Mheshimiwa Dkt. Kigwangala concentrate* kwenye kazi kwa sababu vitu vingine *sometime* unakuwa kama unaenda *off step* unavunja bodi halafu Mheshimiwa Rais siku mbili baadaye anakuja anairudisha vitu kama vile havitakiwi inakuwa ni kama *political movies*. Nakujua una *potential* yaani *probably* katika watu wanaokuja katika hili jengo na uwezo wako na *potential* wako mimi nikoo kwa kule tulikotoka *forget about political issues, zile petty issues za politics, concentrate* kwenye kutuongezea watalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi kama Malaysia kwa mwaka wana watalii 25 milioni *brother* yaani wana watalii wengi kuliko *population*. *Population* ni 20 milioni lakini wanakuwa wana wataalii kwa mwaka 25 milioni ukiuliza vivutio hawana. Kuna siku nilikwenda Malaysia nikwauliza vivutio vyenu ni nini wakasema tuna maghorofa sijui ghorofa gani limejengwa kwa vyuma, tuna daraja gani, tuna *beach* na vyakula yaani mpaka vyakula wameviweka kama sehemu ya kivutio cha watalii. Sisi tuna madude yote haya kuanzia Ngorongoro, kuanzia Serengeti, kuanzia sijui Ruaha, kuanzia wapi kwa kweli tulitakiwa tuwe na watalii hata angalau milioni 10,15 kwa uwezo wetu wa kujitangaza, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Yussuf Hussein dakika tano atafutiwa na Mheshimiwa Catherine Ruge, Mheshimiwa Mohamed Mgimwa ajiandae.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi na kwa sababu ya dakika tano itabidi niende *in a point form* kwa sababu ni mijumbe muhimu sana katika Wizara hii. kwanza nianze kwa kuwapa pole

ndugu zetu wa Pemba ambao ni wadau wakubwa katika utunzaji wa rasilimali hizi za Maliasili na Utalii wa Kisiwa cha Fundo ambao wamepata ajali jana mashua kama 34 zimepotea na tano hazijaonekana mpaka sasa hivi na watu zaidi ya 30 hawajulikani walipo. Kwa hiyo, wale Kasa na Makobe wanaowatunza kwa ajili ya Utalii na watalii watapata shida, kwa hiyo, tunawapa pole kwa tukio hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema mwaka jana wakati anachangia Wizara hii kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba ni Wizara moja ngumu sana ni Wizara yenye changamoto nyingi sana, ni Wizara ambayo inahitaji umakini mkubwa sana na nikamuonya Mheshimiwa Waziri kwamba asipokuwa makini anaweza kuwa ni Waziri atakayehudumu kwa muda mfupi. Lakini nitaanza kusema kwamba Mheshimiwa Waziri katika kipindi kifupi ameonesha umahiri na umakini na ameenda vizuri sana na haya mafaniklo yanayopatikana sasa hivi basi ni kwa umahiri wake na kubwa zaidi au siri ya mafanikio yake ni ile namna anavyoshirikiana na walio chini yake na watalaaam pamoja na wadau wa Sekta hii. Kwa hiyo, nikupongeze Mheshimiwa Waziri na timu yako kwa kufanya kazi vizuri. Niseme pia ni Mbunge nina miakasita humu Bungeni wewe ni Waziri wa nne katika Wizara hii tokea niingie humu lakini kwa uelewa wangu na nilivyoona nathubutu kusema kwamba ni Waziri bora kulikoni hao waliokutangulia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisemi haya kwa utashi nasema kwa mifano. Kuna meli zaidi ya 12 za watalii za kitalii na watalii ambazo zimeingia katika kipindi hichi. Kuna Waisraeli 1000 wameingia hapa, Wachina 349, kuna kukuzwa hizi hifadhi za Biharaulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika lakini kuanzishwa kwa Jeshi Usu vyote ni vitu ambavyo ni uthubutu wa Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake ambavyo ameweza kuvifanya, kwa hiyo, sisemi kwa utashi nasema kwa mifano ambayo iko wazi kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niache katika hilo kwa sababu ya muda niseme tu kwamba Mheshimiwa waziri ili tuweze kupata watalii wengi basi ni lazima kuna mambo

lazima yatendeke, na kuna mambo Serikali lazima ijipange, wewe kama Waziri hutaweza ni mambo ya Kiserikali, *Political stability transparent democracy* hivi vitu lazima viwepo katika nchi, lakini pia kuboreshwa kwa miundombinu ya maji, umeme na barabara katika maeneo ya uwekezaji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuwe na sheria na sera pamoja na kanuni za uwekezaji ili ziweze kuwavutia wawekezaji kuja kuwekeza katika nchi yetu. Kwa hiyo hatuna haja ya kuona watalii 2,000,000,000; 3,000,000,000 hiyo sio *issue hoja* ni kupata *serious investors* tukipata *serious investors* wakawekeza maana yake tutapawa watalii wa daraja la kwanza na daraja la pili na tukipata watalii wa daraja la kwanza na daraja la pili maana yake mtalii mmoja anaweza *ku-spend from 1000 Dollars* kwenda mbele, kwa hiyo, hata tukipata hao watalii 1,500,000 lakini watalii wenye maana ambao tuna *serious investors* wamewekeza basi tutaweza kupata fedha nyingi zaidi kulikoni kuwa na namba kubwa ya watalii lakini Pato dogo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia watalii ili waje kwa wingi na wajirudia kuja na kuja kila mwaka lazima huduma zetu ziwe nzuri, kwa hiyo lazima uboreshe Vyuo vya Utalii ili vijana wetu waweze kusomeshwa na kuhitimu vizuri waweze kutoa *service* nzuri. Wageni wanaokuja wanakuwa na mila tofauti, tabia tofauti, madhehebu tofauti sasa ni sisi kazi yetu kuweza kuhakikisha kwamba tunawapatia huduma iliyo nzuri ili waweze kuja na mara nyingine tena. Kwa hiyo, lazima tuboreshe vijana wetu wasome.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu a muda nikuombe Mheshimiwa Waziri kuna sheria zinazokinzana sheria hizi zinahatarisha Maliasili zetu, kwa hiyo tukuombe kwamba Mheshimiwa Waziri uwe *initiator* ukae na Mheshimiwa Waziri wa Madini, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi ili muweze kupitia sheria zote zile ambazo zinakinzana zinaleta ukakasi katika kutunza rasilimali zetu ili sasa tuweze kutunza. Mheshimiwa Waziri kuna sheria zinakinzana na zinahatarisha Maliasili zetu, hususani wanyamapori, tunakuomba katika hili basi wewe

uwe *initiator* katika hawa Mawaziri muweke hiyo timu mupitie zile sheria na mlete hapa Bungeni ili tuzifanyie kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ...

NAIBU SPIKA: Kengele imeshagonga Mheshimiwa ahsante sana, sekunde 30.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Naibu Spika, dakika moja tu. Niombe Wizara ya Fedha hili suala la tozo zilizowekwa kwa ajili ya TANAPA basi ziondoshwe, kwa nini ziondoshwe kwa sababu TANAPA imepewa mzigo mkubwa sana inahudumia zaidi ya mbuga 11 sasa hivi ambazo hizo haziji nini na zimeongezwa na nyingine tano, sasa na hii fedha ambayo inakusanywa kama kodii inarudi kwa wananchi kuititia ujenzi wa barabara, shule na hospitali wakti TANAPA wanafanya kazi hiyo. Sasa kwa nini wakiingiza Magreda, Makatapila, Magari walipishwe kodii? Kwa hiyo naomba Wizara ya Fedha... (*Makof*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Yussuf umeshaeleweka. Mheshimiwa Catherine Ruge dakika 10, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Mgimwa, Mheshimiwa Dkt. Mollel ajiandae.

MHE. CATHERINE N. RUGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa hii fursa niweze kuchangia Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Ningependa kuanza na *issue* za Jimboni kwangu Jimbo langu la Serengeti ninapotoka. Ningependa kuzungumzia suala la kifuta jasho kwa wananchi ambaa wanaishi pembezoni ya mbuga ya Serengeti ambaa wamekuwa wakipata madhira ya kuvamiwa na Tembo kwa kubomolewa nyumba zao, kuharibiwa mazao pamoja na kupoteza maisha. Naomba nitoe mifano michache tu, mfano mwaka jana Kata ya Machochwe Jimbo la Serengeti karibia asilimia 50 ya mazao yaliharibiwa na mpaka sasa hawajalipwa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kijiji cha Makundusi kuna mama alikuwa na mtoto mgongoni aliuwawa na Nyati na yule mtoto alikuwa mdogo wa miezi mitano anatambaa yule mama alifariki na yule mtoto ameachwa yatima mpaka leo hajawenza kulipwa fidia. Kuna wakazi wa kijiji cha Nata wamebomolewa nyumba zao hawajalipwa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri naomba unisikilize, kwenye kitabu chako ukurasa wa 31 umeonyesha shilingi bilioni 1.4 zimeipwa kwa wananchi 7320 kwa wilaya 57 kama kifuta jasho na machozi, lakini kuna malalamiko makubwa na mengi kwa wakazi wa Jimbo la Serengeti kuhusu kulipwa fidia au kifuta jasho kwenye mazao yao yaliyoharibiwa, wanakijiji waliopoteza maisha na nyumba zilizobomolewa. Sasa nikuombe Mheshimiwa Waziri naomba nipate *list* ya watu walilipwa kutoka katika Wilaya ya Serengeti kati ya hizi shilingi bilioni 1.4 ulizozionyesha, na usipofanya hivyo leo nitaondoka na mshahara wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niende kwenye mambo ya Kitaifa, kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri ameonyesha kwamba mapato yanayotokana na Utalii ni *dollar* za Kimarekani milioni 2.4, idadi ya watalii ni milioni 1.5. ukitafuta *per-capital spending* ya kila mtalii kwa maana ukichukua mapato yale tuliyoyapata *dollar* za Kimarekani milioni 2.4 ukigawa kwa idadi ya watalii wapatao milioni 1.5 unapata shilingi *dollar* 1.6 sawa na shilingi 3,500, maana yake ni nini, ni kwamba kila mtalii alitumia shilingi 3500 na ningependa kupata ufanuzi hizi *data* ni za kweli au hata wale vijana wa bodaboda wanafika kwenye geti la Serengeti na wao mnawahesabia ni watalii?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la mradi wa *Stiegler's Gorge* ambao Serikali imeamua kwenda kuutekeleza katika Bonde la Mto Kilombero pamoja na Rufiji ambako kuna pori la Akiba la *Selous*. Wote tunafahamu Selous is the World heritage, ni urithi wa Dunia. Lakini pia tunafahamu Utalii wa Southern Circuit unategemea mbuga ya Pori la *Selous* lakini nasikitika kwamba Serikali imeamua kwenda kuharibu mazingira *bioanuai* na kuathiri

maisha ya Watanzania zaidi ya 500,000 wanaofanya *activities* na wanaoishi pembeni mwa bonde la Kilombero pamoja na Mto Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa watu ambao wa umri wangu ambao walisoma *Literature* wakati nikiwa *form three* kuna kitabu kimoja kilikuwa kinaitwa *Song of Lawino*, kwetu sisi *Stiegler's Gorge* ni kama *Song of Lawino*. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwetu sisi tutaimba mradi wa *Stiegler's Gorge* kama *Song of lawino* ili mtanzania, ili Watanzania wote wenye masikio na wasikie kwamba mradi huu una madhara na hautakwenda kuwaafidisha Watanzania. *Stiegler's Gorge is nonstarter project* na ninawaomba namuomba Mungu Waheshimiwa Wabunge 2020 tuweze kupata...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MHE. CATHERINE N. RUGE: Namuomba Mungu atujalie Waheshimiwa Wabunge turudi hapa 2020 ili muweze kuthibitisha maneno yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivyo, *Stiegler's gorge is non-economically viable*, *Stiegler's gorge is not economical viable*.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo statement huwezi kurudi Bungeni.

MHE. CATHERINE N. RUGE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kwanza kabisa gharama za utekelezaji wa huu mradi umekuwa *under estimated*, kuna taarifa ya mtu anaitwa George Hartman amesema amefanya *economic feasibility* na ripoti yake inasema kwamba mradi huu utatekelezwa kwa triliioni 21 wakati sisi Tanzania tumesema ni triliioni 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Benki ambazo tumezifuata kwenda ku-*finance* huu mradi hazina uwezo *Egyptian Banks* haziwezi ku-*finance* huu mradi na tukisema tutumie mapato ya ndani pia hatuna uwezo wa ku-*finance*

triliuni 21 kwenye *Stiegler's Gorge*. Pia mradi huu unakwenda kuwaathiri watu zaidi ya 500,000 wanaoishi pembezoni mwa Bonde Mto Rufiji pamoja na Bonde la *Selous* kwa sababu shughuli zao zinategemea maji yanayotoka katika Mto Rufiji. Pia hatujafanya *environmental impact assessment* kuona madhara ya muda mrefu kwa ajili ya huu mradi.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Catherine Ruge naomba ukae. Mheshimiwa Subira kanuni iliyovunjwa.

KUHUSU UTARATIBU

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni iliyovunjwa ni kanuni 64 naomba nisilsome.

NAIBU SPIKA: Endelea Mheshimiwa Subira.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, hatatoa Bungeni taarifa ambazo hazina ukweli wowote Kanuni 64(1)(a). Mheshimiwa Mbunge Catherine anayechangia anatoa taarifa ambazo hazina ukweli wowote, mradi wa Rufiji *hydro power* ulifanyiwa tathimini na tenda iliyotangazwa wakandarasi wameomba kwa kadri wanavyoweza kufanya ule mradi na ndio maana tumeingia mkataba nao wa kiasi cha triliuni 6 ambazo wakandarasi na timu ya Serikali ya wataalam iliyondwa kwa pamoja na kwa majadiliano tumekubaliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa anaposema kwamba mradi utagharimu triliuni 21 na kwamba Serikali imeingia na mabenki ambapo Serikali utagharamia mradi huo kwa vyanzo vyake vya ndani na imeshatoa asilimia 15 kiasi cha bilioni 685. Sasa anaposema kwamba Serikali imetumia mabenki ambayo hayapo asilipotoshe Bunge Serikali itagharimu mradi huu kwa pesa zake za ndani na imeshalipa asilimia 15 na kazi inaendelea. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Catherine Ruge alikuwa akichangia, Mheshimiwa Subira Mgali amesimama akionesa kwamba katika mchango wa Mheshimiwa Catherine Ruge ametoa taarifa ndani ya bunge ambazo hazina ukweli kwa mujibu wa Kanuni ya 64(a). Sasa Waheshimiwa Wabunge uksoma masharti ya hii Kanuni ya 64 na Kanuni ya 63 inanitaka nikiombwa utaratibu kuhusu jambo hili nimtakie Mheshimiwa Mbunge aliyejewa akichangia kwa maelezo hayo yaliyotolewa na Mheshimiwa Subira Mgali kwa sababu yeye ndio aliyesema hilo jambo si la kweli na amejaribu kuonyesha namna ambavyo yeye taarifa zake alizonazo zinaonyesha kwamba taarifa unayotoa ni tofauti na anayoitoa.

Kwa hiyo, kwa mujibu sasa wa hii Kanuni ya 64 na Kanuni ya 63 inayozungumzia kutokusema uwongo Bungeni Mheshimiwa Catherine Ruge taarifa hiyo ya Mheshimiwa Waziri na taarifa uliyoitao wewe uyafute hayo maneno labda kama nawe unao ushahidi tutakutaka kwa mujibu wa kanuni hii. Kwa hiyo, unayo hayo mawili, moja ni kufuta kwa mujibu wa kanuni hizi kama unaoushahidi utanijulisha ili niweze kutoa maelekezo mengine Mheshimiwa Catherine Ruge. (*Makofii*)

MHE. CATHERINE N. RUGE: Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni maoni yangu na nimesoma *report* ya George Hartman inasema hivyo mradi utatekelezwa kwa trilioni 21 hiyo ni *research report* amefanya utafiti kama hauna hiyo *report* nitaweza kukupa, lakini pia sheria mpya ya madini inasema...

NAIBU SPIKA: Sawa ngoja Mheshimiwa Catherine Ruge kabla hujaendelea kuchangia tulimalize hili kwanza, kwa hivyo katika yale mawazo mawili wewe unasema unao ushahidi.

MHE. CATHERINE N. RUGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ndio.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa hizi Kanuni zetu mchango wa Mheshimiwa Catherine Ruge

nimelazimika kumuuliza mara ya pili kama anao ushahidi kwa sababu ameanza kwa kusema ye ye ni mawazo yake, lakini sasa amethibitisha kwamba ye ye anao ushahidi. Kwa hivyo, nitamruhusu aendeleee kuchangia ataleta ushahidi wake ambao ushahidi huo kama taratibu zetu zilivyo ili kumbukumbu zetu zikae sawasawa ushahidi huo utapelekwa kwenye Kamati ambayo itatusaidia kuangalia uhalisia wa hiyo taarifa anayoitoa. (*Makofî*)

Kwa sababu hiyo Mheshimiwa Catherine Ruge mchango wako kuhusu *Stiegler's Gorge* kwa kuwa sasa utapeleka ushahidi kwenye Kamati utaangaliwa wakati huo, naomba uendeleee kuchangia kwenye jambo jingine linalofuata. (*Makofî*)

MHE. CATHERINE N. RUGE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee na mchango wangu. Nafahamu Tanzania tuna vyanzo vingi sana vya umeme ambavyo tungeweza kuwekeza huko na tukapata *megawattshizo* hizo 2,100 au zaidi, lakini pia nafahamu Wajerumanî ambao wamekuwa wakitoa fedha kwa ajili ya kuhifadhi mazingira kwenye Bonde la Akiba la *Selou* toka mwaka 1959, lakini pia wakitoa pesa kwa ajili ya kuzuia ujangili, walitoa *offer* kwa Serikali kuweza kuwekeza kwenye *alternative source of energy* ya *geothermo* na wakasema wanaweza waka-*finance* huo mradi wa umeme wa *geothermo* kupata *megawatts* 2,000, lakini Serikali imekataa *offer* hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa tu kufahamu, ni kweli tuna nia ya kupata nishati ya umeme au nia yetu ni kwenda kuharibu Bonde la *Selou* ambalo limekuwa kivutio kikubwa cha watalii kwa *Southern Circuit*, lakini pia utalii wa *Southern Circuit* unategemea sana Mbuga ya *Selou*. Naomba niseme na iwekwe kwenye *hansard*, mpaka mwaka 2025 hamtakuwa mmetengeneza hata *megawatt* moja kutoka kwenye Mradi wa *Stiegler's Gorge*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye jambo lingine. Kulikuwa na hoteli za kitalii ambazo ziliikuwa kwenye hifadhi ambazo ziliikuwa chini ya Serikali, lakini

wakapewa watu binafsi, lakini hoteli hizi zimekuwa na hali mbaya kuliko hata zilivyokuwa chini ya Serikali. Jumla ya hoteli hizi ziliikuwa 16, lakini nina mifano michache; moja ya hoteli hizo ni *Mafia Lodge* ya Mafia, *Lobo Lodge* Serengeti, *Seronera Wildlife Lodge*, *Ngorongoro Wildlife Lodge*, *Manyara Wildlife Lodge*, zina hali mbaya kimiundombinu, mapato, huduma. Ningependa kufahamu msimamo wa Serikali kuhusu hoteli hizi ambazo zilibinafsishwa na hazifanyi vizuri na ni nini sasa *way forward* kuhusu kuzihusisha hoteli hizi.

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili imegonga Mheshimiwa Catherine Ruge.

Waheshimiwa Wabunge nilikuwa sijamaliza kuhusu Taarifa ambayo Mheshimiwa Catherine Ruge ataipeleka kwenye Kamati. Mheshimiwa Catherine Ruge atapewa muda kwa ajili ya kuwasilisha taarifa hiyo na kufikia Jumatano, wiki ijayo, awe amepeleka ushahidi huo.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Matiko.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nilikuwa nataka tu kupata utaratibu wa hicho ulichoongea cha Mheshimiwa Catherine Ruge, nimefuatilia wakati anachangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Catherine Ruge anachangia na naomba Kuhusu Utaratibu kwa kipengele cha 63(2). Wakati Mheshimiwa Catherine Ruge anachangia alisema huu mradi hautakaa utekelezeke kwa sababu, Serikali kwa kuangalia imesema itatumia trillioni sita, lakini kuna tafiti ameionna ambayo inasema itatumia, ya

George Hatman, itatumia trilioni 21, *I think*. Sasa ukirejea Kipengele cha 63(2) kinasema, Mbunge yeote anapokuwa akisema Bungeni hatachukuliwa kuwa amesema uwongo iwapo anafanya rejea ya habari kuhusu jambo fulani lilitangazwa au lilioandikwa na vyombo nya habari. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Catherine Ruge amejaribu ku-refer kwamba, kuna tafiti imefanyika na George Hatman ambayo inaonesha kwamba, ili mradi ukamilike utatumia trilioni 21, lakini Serikali imesema itatumia trilioni sita. Kwa hiyo, anajaribu kuona kwamba, huu mradi kama kweli ile tafiti hautatekelezeka kwa trilioni sita. Sasa ningepata *guidance* kwa sababu, kwa alichokisema nilichokifuatilia sioni kwamba, anatakiwa kusemekana kama amesema uwongo bali amefanya rejea ya jambo. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge amesimama Mheshimiwa Esther Matiko kuomba Kuhusu Utaratibu kuonesha kwamba, kuna kanuni pengine imevunjwa au inavunjwa. Ameeleza kwa mujibu wa Kanuni ya 63(2) kuonesha kwamba, yeye kwa aliyosikia mchango wa Mheshimiwa Catherine Ruge na majibu ambayo ameyatoa pia, kuitia utaratibu Mheshimiwa Subira Mgalo kwa mawazo yake yeye Mheshimiwa Esther Matiko anaona kwamba, hawezi kudhaniwa kwamba, amesema uwongo kwa kuwa ametaja taarifa aliyokuwa anaizungumza ameipata kwenye utafiti fulani.

Sasa hapa Bungeni kwa sababu, utafiti huo hatukonao kwa hivyo, sijatoa mimi hukumu kwamba, amesema uwongo ama hajasema. Ndio maana nikampa fursa ya aidha afute kama hana hakika, kama anao ushahidi nikampa pia fursa kwamba, aseme akasema anao ushahidi na atathibitisha. (*Makofî*)

Kwa sababu hiyo, kanuni hii inanitaka nimpe muda wa kuwasilisha ushahidi wake, ili tufahamu alichokichangia ni nini na kile ambacho wenzetu watakaotusaidia kuangalia, kwa sababu hatuwezi kuangalia sote hapa, watakuja watutaarifu, hakuna kosa katika hilo. Hata hivyo kwa sababu,

usikilizaji wetu Waheshimiwa Wabunge wakati mwingine tunachagua ya kusikiliza kwa hivyo, Taarifa Rasmi za Bunge zitawenza kutupa mwongozo Mheshimiwa Catherine Ruge alisema kipi, Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu kipi, tutaongozwa na hayo mawazo ambayo wenzetu watakuwa nayo na Mheshimiwa Catherine Ruge atakuwa amepata fursa ya kujieleza kwenye Kamati, tunaendelea. (*Makof!*)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, samahani.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Matiko, ataenda kwenye Kamati kwa sababu atapeleka huko ushahidi.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Kamati gani? Kamati gani?

NAIBU SPIKA: Anapeleka ushahidi si jambo lingine, unao utafiti hapo Mheshimiwa?

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, anatakiwa ai-table kwa Spika sio kwenye Kamati ya Maadili. Kwa Spika, anai-table kwako.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Matiko naomba ukae. Naomba ukae.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata
utaratibu)*

MBUNGE FULANI: Acha uwoga, acheni uwoga, tuendelee.

*(Hapa Mhe. Esther N. Matiko aliongea bila kufuata
utaratibu)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Matiko nimesimama unaendelea kuzungumza. Mheshimiwa Matiko nimesimama unaendelea kuzungumza.

*(Hapa Mhe. John W. Heche aliongea bila kufuata
utaratibu)*

NAIBU SPIKA: Naomba mnyamaze, Mheshimiwa Heche naomba unyamaze, nimesimama. Nimesimama naomba ukae, naomba usizungumze nikiwa nazungumza ndio maana ya Spika; *when I am speaking you have to keep quiet.* (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tuzisome hizi kanuni zetu vizuri, ukiomba Kuhusu Utaratibu Kanuni ya 72 nikishazungumza baada ya huo utaratibu nimemaliza. Kama liko jambo ambalo wewe unaona maamuzi yangu Kuhusu Utaratibu hukubaliani nayo, unarudi kwenye kanuni nyingine ambayo inakupa wewe fursa ya kusema sikubaliani na maamuzi ya Kiti, ndio utaratibu wetu, tuzisome kanuni vizuri. Kwa hiyo, kwa kanuni hizo nilizozitaja kuhusu maamuzi yangu, kuhusu jambo alilolichangia Mheshimiwa Catherine Ruge kwenda kupeleka kwenye Kamati, mimi ndiye niliyeona Kamati itaangalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Esther Matiko tafadhali, narudia tena. Mheshimiwa Esther Matiko tafadhali narudia tena.

Kamati yetu ya Haki na Maadili itamsikiliza. Nimemaliza kuhusu hilo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Mohamed Mgimwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mollel. Mheshimiwa Magdalena Sakaya ajiandae.

MHE. MOHAMED H. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nichukue fursa hii kumpongeza ndugu yangu, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, Waziri wa Maliasili pamoja na mdogo wangu Mheshimiwa Kanyasu kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara yao, waendelee kuchapa kazi, sisi tuko nyuma yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajielekeza kwenye ushauri zaidi. *TANAPA - Hifadhi ya Taifa* tulikuwa tuna hifadhi 16 na katika hifadhi 16 hifadhi tano tu ndizo zilizokuwa zimeweza ku-*break even point*; Hifadhi ya *Arusha National Park, Kilimanjaro National Park, Serengeti, Manyara* na *Tarangire*, lakini hifadhi nyingine 11 zilizokuwa hapo awali zilikuwa hazijaweza ku-*break even point* na sasa hivi tumeiongezea *TANAPA* hifadhi nyingine tano kwa hiyo, wana hifadhi 11, kwa hiyo, mzigo uliokuwa unaendeshwa katika hifadhi hizi nyingine 11 umeongezewa nyingine tano zimekuwa 16, kwa hiyo, kwenye eneo hili tuna hifadhi 16 ambazo hazi--*break even point*, kwa hiyo, *TANAPA* tumewaongezea mzigo mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili tunatakiwa tuliangalie kwa makini. Lengo letu ni kuhakikisha hizi hifadhi zinatuletea mapato ya kutosha, lakini kama hatutakuwa tuna mkakati mzuri wa kuhakikisha tunazisaidia hizi hifadhi zikapata mapato ya kutosha hilo ni tatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna hifadhi kama Saadani. Saadani ina utalii wa aina yake, hapa tunaweza tukapata hadi maeneo ya fukwe. Sasa naiomba sana Wizara ije na mikakati mizuri ambayo itatusaidia kwenye hifadhi hizi 16 ambazo tumeziorodhesha sasa ziweze ku--*break even point*, otherwise tutakuwa hatuna sababu ya kuongeza kwa sababu kwenye taarifa yake ambayo Waziri ameizungumza amesema bado kuna hifadhi mbili kwa maana ya Moyowosi na Rubando Rumanyika, wanataka kuziingiza kwenye Hifadhi za Taifa kwa hiyo, tutakuwa tunazidi kuwaongezea hawa wenzetu wa *National Park* mzigo mzito. Tunajua Dkt. Kijazi anafanya kazi nzuri, lakini watakuwa wanambebesha mzigo ambaao atakuwa anashindwa kuufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ushauri wangu kwenye eneo hili, gawio ambalo linapelekwa kwenye Serikali Kuu hawa wenzetu wangeli-*retain* kusudi waweeze kuzihudumia hizo hifadhi zilizobaki kwenye maeneo haya. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliangalie hili. Tunataka hizi hifadhi ziendelee kutupatia pesa,

kwa hiyo, hilo gawio tuli-retain kwenye hizi hifadhi kusudi hawa wenzetu wa *National Park* waweze kufanya kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima wenzetu watuambie wana mikakati gani ambayo wameitengeneza kwa ajili ya kuhakikisha wanaboresha utalii hapa nchini? Sisi kama Watanzania tumekuwa mara nyngi tunategemea utalii wa nje; je, tuna mikakati gani ya kuhakikisha tunakuza utalii wa ndani?

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii wa ndani unaweza kuboreshwa tu kama tutatengeneza *infrastructures* za uhakika ambazo zitawasaidia watu wa kawaida waende kutalii ndani. Gharama za utalii zikiwa ziko rahisi zaidi Watanzania wengi watapata nafasi ya kwenda kupumzika. Kwa mfano Saadani, Mbuga ya Saadani iko karibu na mikoa mashuhuri kama Mkoa wa Dar-es-Salaam, Morogoro na kadhalika, kama tutaitengezea utaratibu wa *infrastructure* kwa maana ya maboma mle ndani yakawa bei rahisi, itakuwa rahisi kwa watu siku za *weekend*, Jumamosi na Jumapili kwenda pale Saadani na kupumzika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka kuchangia ni suala la *Ruaha National Park*. *Ruaha National Park* ni mbuga ya pili kwa ukubwa katika Bara la Afrika baada ya Mbuga ya Kruger ile ya *South Africa*, lakini pamoja na ukubwa uliokuwepo hii mbuga inaonekana iko *idle* na hakuna mkakati wowote amba o unaonesha unataka kuikuza hii Mbuga ya *Ruaha National Park*. Kwa Sababu tuna *interest* ya kuhakikisha utalii ulioko pale katikati ya Tanzania uwe unalingana na ule wa Kusini mwa Tanzania, kwa hiyo, tutengeneze mkakati tuhakikishe na mbuga kama ya *Ruaha National Park* inapewa kipaumbele na inaboreshwu kusudi iwe mionganoni mwa mbuga muhimu katika nchi yetu. *Ruaha National Park* ni mbuga ambayo ina tembo wakubwa amba huwezi kuwalinganisha na tembo wanaopatikana katika maeneo mengine yoyote hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nilipenda kuchangia ni eneo la msitu na eneo hili nataka tena

kutoa ushauri. Mheshimiwa Waziri naomba atusaidie sana tuangalie bei na tozo mbalimbali kwenye eneo hili la mazao ya misitu. Biashara ya msitu katika Mikoa ya Njombe na Iringa ni moja ya biashara nzuri sana katika mkoa wetu, lakini cha kusikitisha kwa sababu ya tozo hizi zilizopo biashara hii imeshakuwa ngumu. Uchumi wa Mufindi ulikuwa unategemea sana biashara ya msitu, lakini kwa sasa hivi kutokana na tozo zilizopo nyangi kwenye hili eneo imekuwa ngumu hizi biashara kufanyika kwa hiyo, watu wameshaanza kuhama. Mbao zimekuwa bei ghali kwa hiyo, kumetokea mbadala, watu badala ya kuezeka kwa kutumia mbao, sasa hivi wanaezeka kwa kutumia vyuma. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri aliangalie hili jambo. Tumewekeza hela nyangi kwenye eneo la msitu, lakini tukiendelea kuliacha hili zao likaendelea kukaa kwa utaratibu huu litapotea kabisa na msitu utakuwa hauna thamani tena. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri zile tozo zilizopo kwenye eneo hili ziangaliwe upya na thamani na gharama za kuuza mbao kwenye eneo hili tuziangalie upya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri ni mahusiano, Mheshimiwa Waziri angetusikiliza ingekuwa bora zaidi kuliko anachokifanya sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mahusiano yaliyopo kati ya maliasili pamoja na maeneo yetu katika Majimbo ya Mufindi Kaskazini; katika Jimbo la Mufindi Kaskazini ni eneo ambalo tumewekeza sana katika Mradi wa *Sao Hill* kwa maana tumepanda miti mingi, lakini *infrastructure* nyangi zinaharibiwa sana wakati wa uvunaji wa misitu, lakini maliasili hawachangii chochote katika utengenezaji wa ile miundombinu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri jambo hili aliangalie kwa kina. Sisi watu wa Mufindi Kaskazini hili jambo linatusikitisha sana. Tukiwaomba hata siku nydingine wenzetu watupe makatapila na mimi kama Mbunge wao nitoe hela kidogo katika Mfuko

wa Jimbo nichangie, hawako tayari kwenye jambo hili. Kwa hiyo, itafika kipindi sisi watu wa Jimbo la Mufindi Kaskazini tutakataa wenzetu wasiende tena kwenye msitu, watumie barabara za kwao, wasitumie barabara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha atwambie tunajengaje mahusiano ya kuhakikisha wenzetu walioko kule *Sao Hill* wanatusaidia katika kutengeneza *infrastructure* za barabara zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho ambalo nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri, kule katika Jimbo la Mufindi Kaskazini kuna maeneo mawili ambayo ni mazuri sana kwa ajili ya utalii. La kwanza lipo Mpangatazara. Kule Mpangatazara kuna kisiwa ambacho kinahama, asubuhi utakuta kisiwa kiko kushoto baadae utakuta kiko Kaskazini. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri namwomba sana Waziri awatume wataalam wake waje kwenye maeneo yale na waangalie, pale pana utalii mkubwa kwenye hilo eneo la Mpangatazara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine katika eneo hilo kuna *waterfalls* za Mpangatazara ambazo huwezi kuzipata sehemu yoyote hapa nchini. Kwa hiyo, utalii uko kwenye maeneo mengi, lakini kitu kingine, tulikuwa tuna vyura va Kihansi ambaao walivuma sana miaka ya nyuma, lakini leo hatusikii chochote kuhusu vyura wa Kihansi, vyura hawa wanazaa, hakuna vyura wowote hapa duniani ambaao wanazaa. Kwa hiyo, namuomba sana Mheshimiwa Waziri, wenzetu wazungu walikuja wakawachukua wale vyura wakawapeleka Ulaya, lakini sisi Watanzania tumenyamaza kimya hatutaki kuendelea kuukuza utalii katika eneo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja atwambie sisi kama Watanzania tuna mkakati gani kuhakikisha tunaendelea kuenzi eneo hili la utalii wa vyura ambaao wanazaa ambaao huwezi kuwapata sehemu yoyote hapa duniani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Nawataka vijana waendelee kuchapa kazi. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Dkt. Mollel, atafuatiwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Dkt. Kiruswa ajiandae.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri, lakini zaidi niwapongeze wananchi wa Nzega kwa kutuletea jembe. Nimpe Waziri salamu zake kwa wale ambao tulijipanga Muhimbili kumchagua akawa Rais wetu wamemwambia kwamba, hawakukosea walijua yeye ni kichwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, naenda kutumia *kigwanomics* naomba Mheshimiwa Waziri anisikilize vizuri sana. Wilaya ya Siha ni wilaya pekee Tanzania ambayo iko katikati ya milima miwili mikubwa na Wilaya ya Siha tulishajipanga kwenye *cable cars* zile za kupanda kwenye milima na tulitenga eka 800 kwa ajili ya kufanya shughuli mbalimbali pamoja na hizo *cable cars* na mambo ya utalii. Tayari tumeshawakabidhi *TANTRADE* eka 200 zimebaki 600, aje kwetu Siha uchukue eka 600 ili tuweze kujipanga na ni mkakati mzuri kwa sababu, tukifiria kutengeneza *cable cars* tukaanza kuitafakari Wilaya ya Hai, Wilaya ya Siha, tukiangalia vizuri tunaweza kupanga hizo *cable cars* ninaamini ni kitu ambacho kita-*boost* sana kuongeza pato la Wizara ya Maliasili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba, Wilaya ya Siha iko katikati ya milima mizuri miwili, lakini imezungukwa, utakuta huku kuna Mlima Meru ambao kuna hifadhi, lakini kwa Kaskazini kwake kuna *corridor* ambayo wanyama wanapita kutokea huku upande wa Meru na kwingine Tarangire kuelekea upande wa Kenya. Maana yake ni utalii, lakini kunakuwepo na ule wakati wa kupanda Mlima Meru, ukipanda Mlima Kilimanjaro sio tu unapanda moja kwa moja kwenda Mlima Meru ukipitia Siha, unapanda Mlima Meru, lakini Mlima Kilimanjaro wakati unapanda Mlima

Kilimanjaro unakutana na hifadhi na unakutana na wanyama, wanyama ni wengisana. Maana yake tukiwekeza kwenye hizi *cables* wakati wanapanda Mlima Kilimanjaro lakini chini yake watakuwa wana-enjoy sana kuona wanyama wakiwa chini wanapoendelea. Kwa hiyo, kwa sababu sisi tulishachora mpaka michoro ya hoteli na hizo *cables*, namwomba Waziri atembelee Wilaya ya Siha ili aweze kuona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Siha vilevile ukiangalia tuna mlima unaitwa Donyomorwak ambao ni sehemu ya kuhiji Wamasai Tanzania nzima. Pale kuna heka zaidi ya 3,500 ambayo sasa hivi wameshikiria Polisi CCP. Kwa kushirikiana na polisi na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Idara ya Mambo ya Kale tunaweza pale tukatunza ule utamaduni wa Kimasai tukafanya *cultural tourism* kwenye ule mlima. Kila baada ya miaka saba Wamasai *East Africa* wanakutana pale. Tutaweka kwa ajili ya kutunza zile, tukatoa kama heka 500, heka 500 zile zikasaidia kupunguza makazi na shida za wananchi na zile heka zinazobaki tukawekeza ikasaidia Wizara ya Mambo ya Ndani kwa pato lakini ikasaidia maliasili pamoja na vitu vingine. Kwa hiyo, mimi nasema hiyo tukifanya vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Kilimanjaro tuna Uwanja wa Memorial lakini tuna CCP wana eneo kubwa sana; tunaweza tukajenga uwanja wa kimataifa wa mpira pale, *Manchester United* wakaja kucheza pale lakini wakafanya utalii wa kupanda mlima. Kwa hiyo ndiyo maana leo nikakwambia natumia *Kigwanomics* ili unisikilize uunganishe hivyo vitu ili twende pamoja tukatengeneze fursa, maana watu wengi wamekuwa wakizungumza yaliyokuwepo na yaboreshweje, twendeni tukaanzishe mapya ambayo yanaweza kutusaidia kuongeza fursa kwenye utalii wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini dada yangu Mheshimiwa Sware ameongea vizuri kuhusu viwanda vyta mazao ya miti. Mimi nafikiri ameongelea vizuri viwanda vyta mazao ya miti, tuna nchi nyingi sana ambazo zimeingia vitani

sasa hivi zinajengwa upya; lakini tukiwekeza vizuri kwenye mazao ya miti na kutafuta masoko nje na kuboresha hivi viwanda vyta miti, tutatengeneza sana fursa mpya kwa watu wetu na kutafuta masoko nje na kwa sababu leo tunazungumzia utakuta wanaajiri watu wengi sana, *saw-dust* nyingi kuna watu wanakuja kuchukua bure tu kwenye maeneo yetu ambayo kuna hivi viwanda vidogo vidogo vyta mazao ya miti. Tunaweza tukawekeza pale na tukaleta teknolojia na tukauza mambo mengi sana, nagongea tu vizuri alichokisema Dkt. Sware.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema tena, rafiki yangu Mheshimiwa Ruge amezungumzia kitu pale na akataka kulinganisha sayansi kubwa inayoendelea *Stiegler's Gorge* na *Song of Lawino*. Pale *Stiegler's* inaendelea sayansi kubwa sana ya ikolojia pamoja na nishati, huwezi kulinganisha kabisa na *Song of Lawino*. Kinachogomba kwenye taifa letu hapa si suala la kupata tu nishati, kinachogomba kwenye taifa letu ni kupata nishati ambayo ni bei rahisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi ukalinganisha gharama ya *thermo energy* (umeme wa jotoardhi) na umeme ambao tutazalisha pale ambapo pamekuwepo. Hapa kwetu viwanda vinashindwa kuja kwa sababu gharama ya umeme ni kubwa, hilo ndilo swali kuu ambalo watu wote tunatakiwa kujibu ndiyo maana mtaelewa kwa nini tukakimbia kule, tumekimbia kule kwa sababu kambi ilikuwa imeshauzwa na imenunuliwa na watu kutoka nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme hivi George Hartman ni nani *anyway?* Tanzania tunasema tunaenda kuwekeza kwenye umeme, umeme rahisi utakao-*bust* viwanda ndani ya Tanzania hii halafu anatokea mtu anaitwa George Hartman anakuja mtu amevaa suti nzuri amependeza kwa pesa za kodi ya Watanzania, anapinga vitu ambavyo vitaboresha kodi ya Watanzania, anakuja kuzungumza mambo ya Hartman hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunasema watu wamechanganyikiwa, tukisema tunaenda kwenye kamati; tunataka tuende hiyo kamati mpelekeni kwenye hiyo kamati achunguzwe na tuanze sasa kujua wasaliti wa taifa hili. Hatutaki mtu ukiwa Mbunge hapa, ukija hapa Bungeni kama unazungumzia masuala ya kitaifa na yale ya msingi usituletee *idea* za watu wenye *interest* na vita vya kiuchumi kwa ajili ya taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi hili Taifa litakwenda kulindwa, mambo ya Hartman, huyu Hartman ndugu yake huko miaka 1800 aliyahi kuandika kitabu kuhusu *Stiegler's Gorge*, akasema *this is the cornerstone of development* ya hiyo nchi yake wakati huo *East Africa* yaani huyo huyo babu yake alisema wakiwekeza *Stiegler's Gorge* itakuwa *cornerstone* ya maendeleo ya Taifa lao wakati ule kutokea *East Africa*.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo unatokea na *ki-proposal/cha* mtoto sijui anaitwa Hartman *thesis* yake ya chuo kikuu unakuja kutuambia hapa Bungeni tukae tukusikilize, haiwezekani. Sisi tunachosema Tanzania iende kujengwa, tunataka vijana wazuri madaktari wenye akili nzuri kama Kigwangala, tunataka waende kuchapa kazi tukija hapa wakifanya kazi nzuri tunawaambia tumefanya kazi nzuri, wakikosea tunawaelekeza vizuri kwa sababu lengo ni kujenga Taifa hili. (*Makofii/Vigegelele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo siongei sana, nilikuwa nataka kusema hao, nimeshaongea na madalali wa siasa, asante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, nilimtaja Mheshimiwa Magdalena Sakaya atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kiluswa, Mheshimiwa Saed Kubenea ajiandae.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nikushukuru kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii muhimu sana kwa uchumi wetu, ambayo ipo mbele yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi niungane pia na Waheshimiwa Wabunge kupongeza kazi nzuri ambayo inafanywa na Wizara, kwa kweli Mheshimiwa Waziri kuna kazi inayofanyika, tunaiona na inaonekana. Pamoja na kazi inayofanyika lakini bado kuna mambo ya msingi sana ambayo ni lazima Wizara iangalie tena kwa jicho la pekee sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri ametuambia kuhusiana na kiwango kikubwa sana cha utowekaji wa misitu, *speed* ya kutoweka misitu Tanzania ni kubwa sana. Mwaka 2015 na mpaka 2018 tumepokeza *almosthekta* 469,420; kwa mahesabu ya haraka haraka ambayo nimepiga kwa mwaka mmoja tunapoteza hekta 29,000 za misitu ambayo tayari ipo, wakati huo huo *speed* ya kupanda miti bado ni ndogo sana. Kwa hiyo, kwenye suala la misitu inayoteketea bado lazima tutafutie *solution*, kwa mwendo tunaoenda nao bado.

Mheshimiwa Naibu Spika, na leo hili linaloongeleta kwenye vitabu wala huhitaji hata kwenda shule sana, ukiangalia spidi ya kukata misitu inayoendelea na mkaa unavyopelekwa Dar es salaam na magunia ambayo yamejaa kila unakopita yamerundikwa inadhihirisha wazi kwamba hali ya misitu yetu inakwenda kuwa hatarini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba, naomba Wakala wa Misitu wapewe mamlaka. Leo tunazisifia *TANAPA* na Ngorongoro kwa sababu ni mamlaka, wanatumia sheria ya kuhifadhi ndiyo maana unaona wanafanya kazi kulikoni hata mamlaka nyingine. Kwa hiyo, ukipewa mamlaka unakuwa na nguvu ya kisheria. Naiomba Serikali ione umuhimu kuifanya *TFS* waweze kuwa ni mamlaka ili wasimamie kikamilifu matumizi ya rasilimali zote za misitu kwa ukamilifu wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, kuna tatizo kubwa sana la ukataji wa miti kwenye mashamba yaliyopandwa Iringa na Njombe, miti ambayo haijakomaa,

na kwa lugha ya kule wanasema ni kubakwa kwa miti, ,miti inabakwa kabla ya wakati wake. Hili ni tatizo kubwa sana kwa sababu tunaingiza *product* za mbao kwenye masoko ambazo hazijakomaa; wananchi hatujui mbao ipi imekomaa na ipi ambayo haijakomaa, tunanunua, unakwenda kujenga nyumba siku mbili/tatu upepo ukija paa lote limeezuliwa, ni kwa sababu tumeruhusu miti inavunwa ambayo haijakomaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao wataalam wa misitu, nataka nipate majibu ni kwa nini wataalam wa misitu wanakubali mbao ambayo haijakomaa inaingia sokoni? Pia njue mkakati wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa nashangaa, huko nyumba ukienda kuuliza mbao ya *Sao Hill* gharama yake ipo juu sana, ukienda kwenye mbao nyingine gharama iko chini, nikawa nasema ni kwanini tofauti hii ni kubwa sana? Kumbe tatizo ni kwamba mbao ya *Sao Hill* inakomaa vizuri, mbao za wananchi kwenye mashamba hazikomai vizuri lakini zote ni *product* ambazo zinatakiwa ziwe zimekomaa vyatutu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba njue mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba kwanza ni namna gani wananchi watajua mbao isiyokomaa na iliyokomaa sokoni lakini nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba wanatatua tatizo hili ambalo ni kubwa sana ndani ya matumizi ya rasilimali ya misitu na hasa kwa ajili ya ujenzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu *TANAPA*; wengi wamelizungumzia. Kiukweli Serikali isipoangalia, leo tunajivunia wanakuja wageni wataalii mara Waisraeli na Wachina wanakuja kuangalia vivutio vilivyo hifadhiwa na haviku hifadhiwa kwa siku moja, imechukua muda kuvihifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo tusipoenda kimkakati tukaendelea kuweka majukumu mazito kwenye

TANAPA wakati huo huo bajeti ya mwaka huu ya *TANAPA* tumeipunguza kwa asilimia 18, lakini wakati huo tumewaongezea majukumu hifadhi nyingine tano ambazo ni mapori yaliyokuwa yamechoka hayana kazi tena. Tumewapa wayahifadhi, waya-groom mpaka yaweze kuwa ni maeneo ambayo yanatembelewa; watengeneze miundombinu na wawe na watumishi wa kutosha kuhakikisha kwamba hifadhi zile pia zinapeleka watalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ni lazima ikubali, kwa kuwa *TANAPA* wamepewa majukumu makubwa, ipunguze zile tozo na angalau lile gawio la asilimia 15 lipungue liende kwenye 10. Lakini *TANAPA* inafanya kazi kubwa kwelikweli, ukienda kwenye Land Use Plan ya Taifa, *protection*, miundombinu, ujirani mwema kote huko *TANAPA* inachangia. Kwa hiyo, kazi inazofanya nje ya kazi zake ni nyingi sana. Kiukweli kuendelea kupunguza bajeti yake na kuendelea kuwapa majukumu na tunategemea kwamba majukumu hayo yaweze kuwa na tija huko tuendako tunaenda kuiua *TANAPA* kama ambavyo tumeua mashirika mengine ambayo yalikuwepo ndani ya nchi hii miaka ya nyuma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ngorongoro; Kamati tumewahi kuleta maoni ya kwa muda mrefu sana, kwamba sheria hii iliyotengeneza Ng'orongoro miaka hiyo inawezekana leo ikawa inahitaji maboresho. Leo ukienda kule Ngorongoro wananchi wanalamika na ni hifadhi pekee nadhani duniani ambapo ni *multiple plan land use* ambapo wananchi, wanyama na mifugo wapo huko huko, ni kitu kizuri kwelikweli. Kwa nini Serikali haileti Sheria ya Ngorongoro tuweze kuifanyia mabadiliko ili Ngorongoro iweze kuwepo *sustainably* lakini pia jamii inayoishi kule iweze kuridhika na kuendelea kuishi vizuri na kuendelea kutunza huu utamaduni wa kuweza kuwepo na *multiple land use* kwenye eneo la Ngorongoro. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la tasnia ya uwindaji wa kitalii. Kwa mwaka 2017 tasnia hii imeyumba kidogo na mpaka sasa hivi nadhani hajasimama vizuri kutokana na kwamba Serikali itaenda kuingiza mfumo

wa kugawa vitalu kwa njia ya mnada katikati ya muhula wa uwindaji, matokeo yake vitalu vingi vikarejeshwa Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri ya vitalu kurejeshwa Serikalini ni kwamba vile vitalu havina ulinzi, hakuna watu wanaovilinda kwa sababu sheria ni kwamba unapewa kitalu kwa ajili ya uwindaji pia unaweka askari kwa ajili ya kulinda rasilimali iliyopo kule. Sasa vile vitalu vyote ambavyo vimerejeshwa havipo salama lakini Serikali inakosa mapato *and at the same time* wale wanyama kule wanawinda kiholela kwa kuwa hakuna anayetunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba Mheshimiwa Waziri atakavyokuja ku-*wind* leo atuambie amefikia wapi kuhusu mchakato wa kuhakikisha kwamba tasnia hii ya uwindaji wa kitalii inakuwa *sustainable*, lazima tupate majibu. Tuklendelea ku-*dilly-dally* kwanza wale wawekezaji wanaondoka lakini pia yale maeneo yanakuwa hayapo salama sana kwa ajili ya kuhakikisha kwamba yanaendelea kuleta kipato lakini pia yaendelee kuwa eneo salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Suala la Migogoro ya Ardhi Kwenye Maeneo ya Wananchi na Maeneo ya Hifadhi. Hili ni lazima tuliseme kila siku kama wimbo kwa sababu ni kitu ambacho kinagusa jamii ya chini kabisa ya wananchi wetu. Mimi nashukuru kwa mara nyingine Mheshimiwa Rais ameunda tume; na mimi nashukuru kwamba hii tume ina Mawaziri ambao tuna imani nao. Sasa hivi tunaambiwa kwamba wamekamilisha kazi na wanaandaa ripoti, lakini maeneo mengi hawajafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninasema kama Mawaziri hawa wataenda kukaa maofisini na watendaji wakapata taarifa za ofisini, tatizo la migogoro hii halitakwisha, watakuja na ripoti hapa *still* kule matatizo yataendelea kuwepo. Mimi nawaomba maeneo ambayo hawajafika, wafike wakaangalie haya maingiliano ya maeneo ya hifadhi waone ili watakopokaa mezani kutoa mapendekezo na kuandika ripoti wampelekee Rais kitu ambacho ni *reality*. Leo

unakwenda kukaa na watu wa TAMISEMI wa Wilaya ambapo hao hao ndio wamesajili vijiji ndani ya hifadhi, unategemea kupata nini? Ukienda kukaa na watu wa mkoa ambaa na wenyewe pia wameshiriki unategemea kupata nini? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hawatapata uhakika (*reality*) mpaka waende kwenye maeneo ambayo yana migogoro wakaongee na wale wananchi na wenyewe waone ule muingiliano, wanaweza kukaa chini wakatoa taarifa ambayo ni nzuri na itaweza kusaidia kuondoa migogoro hii ambayo imedumu kwa muda mrefu lakini pia kiukweli inaleta madhara makubwa sana kwa wananchi wetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la hoteli zetu. Tulikuwa na utaratibu huko nyuma ulianzishwa na nitapenda Mheshimiwa Waziri aje atuambie, ya kuweza ku-*grade* hoteli zetu. Lazima tuwe na *grade* ya hoteli zetu zote, tujue *five star* ikoje, *four star*, *three star* mpaka mwisho. Leo unaweza ukaenda kwenye hoteli unaambiwa hii ni hoteli haifanani hata na *guest*, unavyoenda kwenye hoteli ujue hii ni hoteli, hii ni *lodge* na hii ni *guest house*; lakini leo mtu anajiardikia tu, chumba cha ajabu hakina hadhi anakwambia hii ni *lodge*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Serikali ituambie utaratibu wa kufanya *grading* ya hoteli zetu zote, leo sasa tunaanza kupata wageni wengi, mgeni anaweza akaja akaingia kwenye chumba ambacho alijua ni hoteli, mazingira yale ya hoteli tu yatamfanya *next time* asije tena au picha anayopeleka kule ikawa siyo nzuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba zoezi la ku-*grade* hoteli zetu maeneo yote lilianzwa vizuri sana na Mheshimiwa Shamsi nadhani kipindi hicho, mpaka leo hatujui limefikia wapi. Naomba sana hoteli zetu zote zipatiwe *grading* kwa kuwa ni sehemu moja wapo ya utalii. Mgeni anavyokuja ukimwambia hii ni *lodge* ajue ni *lodge*, *guest* ama *five star hotel*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa muda, yangu ni hayo machache, ahsante sana. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, nilikuwa nimeshamtaja Dkt. Kiruswa, Mheshimiwa Kubenea dakika zake anampa Mheshimiwa Grace Kiwelu. Kwa hiyo Mheshimiwa Dkt. Kiruswa dakika tano atafuatiwa na Mheshimiwa Grace Kiwelu dakika 10, Mheshimiwa Amina Mollel ajiandae.

MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hii hoja muhimu ya Wizara yetu ya Maliasili na Utalii ambayo na mimi ni mjambe wa kamati yake ya kudumu. Kwa hiyo mambo mengi ambayo ningependa kuyasemea bahati nzuri yapo katika ripoti ya makini tulioandaa kama kamati. Kwa sababu nimepewa dakika 5 sina muda wa kuyapitia hayo ila nina maswali machache ambayo nitamuomba Waziri na kweli azingatie ayatolee ufanuzi baadaye atakapokuja kuhitimisha hoja yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza ni kwenye haya maeneo ya jumuiya ya hifadhi ya wanyamapori ambayo tunaita *WMAs* na nitatumia mfano wa *WMA* ya Jimbo langu ya Enduimet. Naomba Mheshimiwa Waziri utakapokuja kuhitimisha hoja yako baadaye unipatie ufanuzi kuhusu hili suala la kucheleweshwa kwa mgao wa fedha za *WMA* zinazotokana na upigaji picha (*photographic safaris*) na hizi za uwindaji. Maana kwenye mfumo zinapokelewa, na tulitegemea kila mwezi baada ya watalii kupita, wanapewa mgao wao, baada ya msimu wa uwindaji kufanyika wanapewa hela yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhalsia ni kwamba hajji kwa wakati na ukweli ni kwamba hii inaathiri sana shughuli za uhifadhi kuwalipa ma-*game scouts* na kufanya shughuli nyingine za kulinda rasilimali lakini pia inachelewesha miradi ambayo vijiji viliviyotenga maeneo yao yahifadhiwe yalishabuni na walikuwa wanategemea hayo mapato ili waweze kujilettea maendeleo waone manufaa ya eneo walilolitenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo Mheshimiwa Waziri nitakuomba utoe ufanuzi baadaye ni kuhusu utaratibu usiwafurahisha wanajamii wa *WMA*, labda zote lakini mimi naseme ya Enduimet ambayo ndiyo ya pekee tuliyonayo ambayo imeshasajiliwa ya uwindaji. Hawa jamii ya *WMA* wanao watu wao waliondaliwa tayari wamefunzwa, wapo *village game scouts* wanajua kusimamia, kukagua na kusaini vibali; lakini uhalisia ni kwamba wanapokuja wale viongozi wa idara ya wanyamapori wanawaleta wawindaji wanawa-*bypass*, hawawashirikishi, na wanasa hau kwamba hawa ni watu walijirisha na jamii yenye we waliopewa mamlaka kamili na ambao wanaaminika, wanalamika kwamba kulikoni mamlaka yao yanaporwa wakiangalia mbona hawashirikishwi. Mheshimiwa Waziri utakapokuja baadaye naomba utolee ufanunuzi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo linahitaji ufanuzi maana nimejikita kwenye *WMA* kama eneo nyeti, ni hili la hii Jumuiya ya Enduimet ambayo imetokea sintofahamu baada ya eneo lao la uwindaji lenye hadhi ya *grade A*, *grade* namba I kushushwa hadi kuwa *grade* namba II bila kuwashirikisha wanajumuiya na kusababisha kupoteza mapato yanayotokana na uwindaji katika eneo la *grade A* kwa asilimia 50. Jamii imeshikwa na taharuki wanashangaa kwa nini hawajashirikishwa, pengine kuna vigezo vya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa hebu uwaambie wananchi wa Enduiment kulikoni maana wamejipanga kuja kukuona ofisini lakini waliposikia leo nitachangia hapa, wakaomba nilisemee mbele ya Bunge zima ijulikane kwa sababu wao walishaingia mkataba na muwekezaji kwamba wamemsainisha *grade A* lakini wameshalipwa kwa mara ya kwanza malipo ya *grade II* ambayo ni nusu ya malipo ya *grade A*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nilipenda kulisemea kwa haraka haraka kwa sababu dakika zangu zinaisha, ni oparesheni za kudhibiti wawindaji haramu. Mimi naunga mkono asilimia 100 kudhibiti wawindaji haramu kwa sababu kizazi hiki na vijavyo vitategemea rasilimali hii ya

wanyamapor. Lakini kuna utaratibu unaotumika ambao unawasababishia watu na raia wasio na hatia kutiwa hatiani na kuumia karibu yote magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyoongea, nina barua hata hapa ya mmoja lakini sitaweza kusoma kwa sababu ya muda, wapiga kura wangu waliopo mahabusu wananiandikia. Kuna mmoja hapa sitaki kumtaja hata jina namhifadhi, lakini amewekwa mahabusu takriban miaka miwili sasa, tangu mwaka 2017 na kosa alilolifanya niliamini kwamba vyombo vilivyopo vinavyobaini watuhumiwa vina uwezo wa kuwadadisi, kuwafikisha mbele ya vyombo vyasheria, kuwahukumu na kuwafunga wasio na hatia na kuwaachia wasio na hatia. Kuna watu wanatumika kuwarubuni watu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kiruswa, kengele imegonga, lakini naona una barua ya huyo mtu; nadhani unaweza kuwaona watu wa Serikali, utawaona wao na orodha yako yote wewe wakabidhi ili sasa uweze kuwafuatialia, kwa sababu hata ukitaja hapa na wao watahitaji muda wa kuwafuatialia.

Kengele ilishagonga Mheshimiwa, ahsante sana.

Mheshimiwa Grace Kiwelu, dakika kumi, atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Mollel, Mheshimiwa Pauline Gekul ajiandae.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nimshukuru pia Mheshimiwa Kubenea kwa kunipa dakika zake tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, lakini na yale maoni yaliyotolewa na Kamati yetu ya Ardhi, Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na upatikanaji wa fedha katika Wizara hii muhimu sana katika Taifa letu. Kumekuwa na ucheleweshwaji au kutokupelekwa kabisa kwa fedha za maendeleo katika Wizara hii. Wachangiaji wengi wameonesha umuhimu wa Wizara hii, lakini Wizara ya Fedha imekuwa haipeleki fedha za maendeleo na kufanya miradi mingi ya Wizara hii kushindwa kutekelezeka kwa wakati. Pia miradi mingi imekuwa ikitegemea wafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tumwombe Waziri wa Fedha kuhakikisha kabisa zile fedha tunazozitenga hapa ndani ya Bunge ziwe zinapelekwa kwa wakati ili kuisaidia Wizara hii iweze kufanya vizuri zaidi. Amesema kaka yangu, Mheshimiwa Mbatia hapa kwamba ili ng'ombe aendelee kutoa maziwa mengi ni lazima alishwe vizuri. Kwa hiyo tunaomba fedha hizo ziwe zinakwenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, Kamati yetu imekuwa ikifanya ziara mbalimbali katika taasisi zilizoko chini ya Wizara hii, kwenye hifadhi zetu na hata misitu. Tumekutana na changamoto mbalimbali, mojawapo ni uhaba wa watumishi katika taasisi hizo na hasa kubwa ni askari wale wa wanyamapor. Tunajua ukubwa wa hifadhi zetu na misitu, hivyo, tuiombe Wizara sasa ihakikishe kwamba inaaajiri askari wengi ambao watakwenda kuhakikisha wanalinda mali zetu, wanyama wetu na rasilimali zote zilizomo ndani ya misitu yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo malalamiko ambayo tumepata kutoka kwa askari hawa wa Jeshi Usu kwamba kumekuwa na utofauti wa malipo kutoka kwa askari hawa wa Jeshi Usu wa *TAWA*, *TANAPA*, Ngorongoro na *TFS*. Wamekuwa wanalipwa pungufu, posho na wengine mishahara. Tunajua kazi wanazofanya ni kubwa na wanafanya kwenye mazingira magumu wote, kwa hiyo tunaomba sana Wizara ihakikishe askari wetu hawa wote wanalipwa sawasawa, yaani kusiwe na tofauti za mishahara wala posho kwa sababu kazi wanayoifanya ya kulinda rasilimali zetu ni kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo upungufu wa magari; tunajua mbuga zetu zilivyo kubwa, lakini pia miundombinu yake si mizuri, magari yaliyopo kule ni machakavu, yanafanya utendaji kazi wao kuwa mgumu sana. Kwa hiyo tunaomba wapate magari ya kutosha na vifaa vingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile wana uhaba wa nyumba za kukaa, wanafanya kazi lakini nyumba za kukaa hawana na wanakwenda kupanga mbali na maeneo yao ya kazi. Tunaomba basi nyumba wajengewe na kama inashindikana basi wapewe *housing allowances* ambazo zinaweza kuwasaidia wao kutekeleza majukumu yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nisemee suala la migogoro ya mipaka; suala hili limechukua muda mrefu sana na migogoro bado tunaendelea kulona. Jana Mheshimiwa Waziri Mkuu amejibu swali kwamba ile taarifa ya zile Wizara nane imeshapelekwa kwa Mheshimiwa Rais, tunashukuru kwa hilo, lakini tunaomba taarifa hii basi itakapofanyiwa kazi na kurejeshwa kwa ajili ya kuanza kutekelezwa wawashirikishe wawakilishi wa wananchi; Wabunge pamoja na Madiwani wa maeneo yale ili kuondoa migogoro hiyo, kwa sababu ikifanywa kimyakimya migogoro hii haitaisha na itaendelea kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tumekuwa tukiona kauli nyingi nzuri na matamko mazuri yanatolewa kwa wananchi, tunaomba yakatekelezeke yasije yakawa ni ya kisiasa kwa sababu tunakwenda kwenye uchaguzi. Tunaomba haya yakafanyike, yafanyiwe kazi vizuri, wananchi wetu waondokane na hii migogoro ya mipaka kila wakati, tupunguze vifo kwa wananchi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pale kwa askari niongeze jambo moja; tulikwenda kwenye mahafali ya hawa askari wa Jeshi Usu, tuliwaomba kwamba pamoja na mafunzo yote wanayopewa lakini wawe wanatimiza wajibu wao wasionee raia, kupiga raia bila sababu. Kwa sababu kumekuwa na

malalamiko ya maaskari hawa kupiga wananchi wetu bila sababu, niwaombe sana wasimamie maadili ya kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo tuliliona na imesemwa kwenye Taarifa yetu ya Kamati na ya Kambi ya Upinzani, ni kuhusu migongano ya sheria zilizopo. Mfano ni Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999, Sheria ya Vijiji Na.5 ya 1999, Sheria ya Wanyamapori na ile Sheria ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yetu tumefanya ziara mbalimbali kwenye hifadhi zetu na tumeona Sheria ya Madini inaweza kutoa kibali cha kuchimba madini kwenye eneo lolote. Tulipita kwenye Hifadhi ya Manyara Bunge lililopita, tulikuta yapo machimbo watu wanachimba kule na hii ni hatari sana kwa watumishi wetu wanaofanya kazi kwenye hifadhi hizo, lakini pia kwa wanyama wetu. Mashimo yale ni makubwa sana yanaweza kuleta athari kwa wanyama wetu. Kwa hiyo niiombe Serikali, Serikali hii ni moja, sheria hizi zimetungwa ndani ya nchi hii, basi ikae kwa pamoja kuhakikisha wanapitia sheria hizi ili kuondoa huo mgongano uliopo katika sheria hizi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala la biashara ya viumbe hai; suala hili limechukua muda mrefu sana, toka 2016, huu ni mwaka wa nne sasa. Wafanyabiashara hawa walizuiwa wakasema wanaweka utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba wataweza kupangiwa ili kufanya biashara zao vizuri, lakini juzi Naibu Waziri alipokuja kwenye Kamati yetu alituambia kwamba biashara hii imepigwa marufuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuiomba na kuishauri Serikali kwamba wafanyabiashara hawa walifuata taratibu zote zinazohusika, walikata leseni, wamelipa kodi na walishakamata wanyama hawa, wameingia gharama ya kuwatunza. Niombe, inawezekana wapo wahalifu wachache walioingilia biashara hii na kufanya wengine kuzuiliwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanyama ambao tunawazungumzia siyo wale wanyama wakubwa kama tembo, twiga na swala kama wale waliosafirishwa kwenye Uwanja wa *KIA* wakati ule; ninaowazungumza na waliokuwa wanasafirishwa ni nyoka, mijusi, ngedere, kenge na vipepeo. Wanyama hawa kama hawatavunwa itakuwa ni hatari sana hapo baadaye kwa *Taifa* letu kwa sababu hawa watatuletea athari kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimuombe Mheshimiwa Waziri kubadilisha maamuzi ambayo wameyafikia na kuruhusu wafanyabiashara hawa kuendelea na biashara hiyo. Wale waliokosea basi wachukuliwe hatua za kisheria, hakuna anayekubaliana na kusafirisha wanyama hao wakubwa nje ya nchi lakini hawa wengine wadogowadogo ambao wanaweza kuleta madhara hapo baadaye waweze kuruhusiwa kuendelea na hiyo blashara. Kwa sababu tunajua hawa walilipa kodi na walifanya taratibu zingine zote na haya ndiyo maisha yao. Wengine wamekopa wanasesmeshea watoto kwa hiyo kuwafungia tu hivihivi siyo sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalotaka kulisemea ni lile ambalo limezungumziwa kwenye Kamati yetu kuhusu *TANAPA*, tozo nydingi sana. Tunaiomba Serikali kuliangalia Shirika hili la *TANAPA*, limekuwa likifanya kazi nzuri kusaidia wananchi wetu lakini limekuwa likirundikiwa kodi nydingi na juzi zimeongezewa tena hifadhi nyininge tano, kwa hiyo kuziendesha itakuwa ni gharama kubwa sana. Kwa hiyo tuiombe Serikali, tuiombe Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba wanaliangalia Shirika hili la *TANAPA* ambalo limekuwa likifanya vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni lile la *TFS* kuwa mamlaka; wamesema wenzangu, jukumu la *TFS* tunalijua, inalinda misitu yetu, lakini ni vizuri sasa kuifanya iwe mamlaka ili iweze kusimamia sheria zake na kufanya maamuzi kama linavyofanya Shirika la *TANAPA* ili nalo liweze kufanya vizuri, tunaomba ikafanyike hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Waziri pia na Naibu wake, wamesema Wajumbe wenzangu kwamba mwanzo Wizara hii ilikuwa ikija mbele ya Kamati ilikuwa ina mambo mengi, lakini wameweza kutekeleza maagizo ya Kamati, wanakwenda vizuri. Niwapongeze sana, lakini yale yote tuliyyoyasema kwenye Kambi ya Upinzani na yale ya kwenye Kamati yetu, tunaomba wahakishe wanayafanya vizuri na hususan posho kwa maaskari wetu pamoja na mishahara yao mkaiboreshe kwa sababu hawa wanalinda rasilimali zetu, ni vizuri wote wakalingana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Amina Mollel, atafuatiwa na Mheshimiwa Gekul na Mheshimiwa Vedastus Ngombale ajandae.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia Bajeti hii ya Maliasili na Utalii.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Amina Mollel, samahani, ni dakika tano, wachangiaji wote wanaofuata wa Chama cha Mapinduzi wanachangia kwa dakika tano.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nitachangia vitu vitatu, lakini awali ya yote niipongeze Wizara, nimpongeze Waziri, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Kanyasu, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Nimpongeze pia Katibu Mkuu wa Wizara hii pia kwa kazi nzuri na ushauri mzuri, pamoja na watendaji wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa niwapongeze Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Ndugu Manongi pamoja na wa *TANAPA* Ndugu Allan Kijazi, kwa kweli wamekuwa na mchango mkubwa sana kwa Tanzania na hasa kwa mimi ninayetoka Mkoa wa Arusha nawapongeza sana kulingana na kazi nzuri wanazofanya za kijamii, na hasa

katika kuwasaidia wanawake. Hongera sana Ndugu Manongi pamoja na Ndugu Allan Kijazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia katika upande wa *promotion* na *advertisements* na hapo ndipo tunapojuiliza nini maana ya utalii. Maana ya utalii pasipokuwa na *promotion* pamoja na *advertisements* ni sawa na kazi bure. Tunafahamu umuhimu wa haya mambo mawili katika kuhakikisha kwamba tunautangaza utalii wetu, tunaitangaza Tanzania kimataifa na hapo basi ndipo ambapo tunapoweza kupata watalii wengi kuja nchini Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri, Nchi ya Tanzania Mwenyezi Mungu ametujalia na tuna kila sababu ya kujivunia kutokana na maliasili zilizopo pamoja na vivutio vingi vivilvyopo katika nchi hii. Wakati mwengine ndipo tunapojuiliza kwamba tunasemwa ni nchi maskini, au sisi maskini; umaskini wetu unatoka wapi wakati tuna utalii, tuna maliasili na tuna mambo mengi ambayo yanaweza kutuletea fedha za kigeni na hatimaye kumkomboa Mtanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, jana tuliona wageni waliofika hapa ambao kwa namna moja wamechangiwa na Wizara hii kuweza basi kuja hapa na kwa namna moja au nyingine, hasa yule *Miss Ukraine*. Hata hivyo, nitakwenda kwa upande wa hapa nyumbani kwetu kuona ni kwa jinsi gani tunawatumia Watanzania ambao wameonesha mafanikio makubwa katika kuwa-*brand* na wao sasa wakatumika kama mabalozi wetu kuweza kuutangaza utalii wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilisimama kwa Mbwana Samatta na nitaendelea kumzungumzia Mbwana Samatta kutokana na kazi nzuri aliyoifanya ya kuitangaza ramani ya Tanzania kupitia soka la kulipwa kule Nchini Ubelgiji. Wizara inapaswa sasa basi kumtangaza kama huyu ni balozi ili aweze kuendelea kuutangaza utalii wetu kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbwana Samatta kwa bahati nzuri sana amefanya mazungumzo na daktari wa hiyo

timu na amehamasika kuja kutembelea Tanzania. Kama ameweza kufanya hivyo, kaka yangu, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, kaka yangu, Mheshimiwa Kanyasu, kwa nini tusimtangaze huyu na kumtumia kuwa kama ni *brand* Balozi, kuweza kuitangaza nchi yetu na kuutangaza utalii wetu kwa kupitia soka analocheza? Kwa kufanya hivi, Mbwana Samatta ataweba kwa kiasi kikubwa pia kuweza kuwaleta watalii wengi kuja kutembelea nchi yetu na hatimaye kupata pesa kutokana na wale watakaokuja hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzijuzi tumemuona mwanadada Azara Charles ambaye tumekuwa tukimuona ni mtu wa kawaida akikaa chini na kupiga zile danadana. Lakini Azara ameweza kumhamasisha kiasi kwamba mpaka Rais wa Taifa kubwa la Marekani, Donald Trump, kuweza kumzungumzia mwanadada huyu ambaye sisi Watanzania tumemwona kwa muda mrefu tukimchangia vipesa vidogovidogo na tayari sasa Azara ameingia mkataba na Kampuni ya Nike.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa je, sisi kama Watanzania tunamtumiae Azara ili kuweza kuutangaza utalii wetu huko atakakokwenda? Hii itasaidia kwa Watanzania. Lakini pia wasanii wetu na wanamuziki mbalimbali na wao pia mbali ya kufaidika, lakini Taifa tutaweza kufaidika mara mbili zaidi kutokana na kazi zao au vipaji vyao wanavyovifanya. Na...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Amina, kengele imeshagonga.

Mheshimiwa Pauline Gekul, atafuatiwa na Mheshimiwa Vedasto Ngombale, ambaye na ye ye ni dakika tano, Mheshimiwa Maftaha Nachuma ajiandae.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niseme machache

katika Wizara hii ya Maliasili. Niipongeze Wizara; Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yake, toka moyoni niwapongeze. Mimi ni Mjumbe wa Kamati, nafahamu kazi kubwa wanayoifanya na Wizara hii imetulia. Hongera sana na hongera pia kwa ushirikiano, maana yake Mawaziri wanapowapa ushirikiano watendaji maana yake mambo yanakwenda. Hongera mno na ndiyo maana Wizara hii sasa imetulia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme hili la Ngorongoro. Mheshimiwa Waziri ametuletea mchakato mzima ambao ulifanyika kwa mwaka mzima, tangu tarehe 23, Mei, 2018, ile timu aliyoiunda ya wataalam kuhusu Hifadhi yetu ya Mamlaka ya Ngorongoro. Nafikiri kwamba hata Kambi Rasmi ya Upinzani walikuwa hawana sababu ya kuandika katika ukurasa wa nane, kwa sababu Mheshimiwa Mchungaji, *to be honest* yeye ni Mjumbe wa Kamati, nilitegemea angempongeza kabisa wala asingeandika hiki cha Ngorongoro kwa sababu hatua ambazo zimechukuliwa na Serikali yeye mwenyewe anazifahamu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri, wapitishe hiyo *document* mapema kwenye Baraza la Mawaziri, walete mapema tumalize mgogoro wa Ngorongoro ili mwisho wa siku ile hifadhi yetu tuiokoe. Kwa hiyo nimpongeze sana kwa hili ambalo wamelfanya na taarifa ameshalandaa tunasubiri tu *finishing*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwapongeze kwa Kamati hii ya Mawaziri ambayo Mheshimiwa Rais ameiunda na kazi inaendelea. Nafikiri ni vizuri *sample size* ikaongezeka, maeneo mengi hayajafikiwa kama ambavyo Wabunge wengine wamesema. Kuandaa hii taarifa ni jambo moja lakini naamini matatizo hayafanani; matatizo ya Tarangire na vijiji vile vitatu hayawezi yakafanana na maeneo mengine. Niombe kama taarifa hii sasa haijafanyiwa *finishing*, waongeze *sample sizes* zao ili vite vijiji ambavyo havijafikiwa viwe *treated* kwa maeneo yao na matatizo yao. Hilo naamini wanaweza wakalipokea maana ni *concern* ya Wabunge wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ambalo nahitaji kuwapongeza ni suala zima la mchakato waliouanza wa kurekebisha Kanuni ya Fidia au Kifuta Machozi ya mwaka 2011. Nimekuwa nikilizungumzia hili kwa muda mrefu sana, nimwombe; kabla hajafikia *finalization* ya kanuni hizo waweze kufika Babati Mjini kuhusu wanyama ambaao kwenye ile kanuni ya mwanzo walikuwa wanasema siyo wanyama waharibifu na siyo wakali, hawawezi waka-*attack* binadamu na boko wamekuwa kwenye kundi hilo, waje waone kwa sababu tuna watu zaidi ya 28 waliopoteza maisha, siyo kwenye Ziwa Babati tu, lakini wakiwa mashambani ambaao wamekuwa *attacked* na wale viboko.

Mheshimiwa Nabu Spika, sasa niombe kabla hawajamaliza kanuni hizo, ambazo wako kwenye mchakato na nawapongeza, naomba wafike Babati waone waathirika na wahanga wa viboko ambaao kwenye kanuni tunawa-*define* kwamba hawa hawana madhara na wananchi hawahitaji kufidiwa. Kwa hiyo kabla hawajamaliza niwaombe wafike ili tuone ni jinsi gani na hawa wahanga wanaweza kufidiwa. Nina majina yao nimeshapeleka ofisini kwao, tunafikiri kwamba sasa wana sababu ya kulitazama hilo kwa upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, na la mwisho kwa siku ya leo nikuombe Mheshimiwa Waziri; Hifadhi ya Tarangire inafanya vizuri hata kwenye *collection* tunaona, kwenye mapato inafanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spia, lakini tuna mageti matatu, kuna geti la kibaoni kilomita sita kuingia Hifadhini ambapo watalii wengi wanatoka Arusha wanaingia hifadhini na kutoka. Pia tuna geti la Sangaiwe ambayo ina kilomita nane, vilevile tuna geti la Babati mjini Mamire to Tarangire kilomita 17. Nikuombe Mheshimiwa Waziri kuititia hifadhi ya Tarangire na Wizara yako muone jinsi gani ya kufanya *maintenance* ya malango yote haya matatu kwa sababu wakiingilia kibaoni Minjingu wakatokea geti la Mamire wakaingia Babati Mjini, ni mahali salama zaidi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Babati tuna hoteli nzuri ambazo naona hata Dodoma hazipo, nzuri kabisa, lakini pia hali ya hewa Babati ni nzuri, tuna ziwa Babati ambako hata hao watalii Mheshimiwa Waziri wanaweza kuja kutazama hawa viboko. Pia tuna mlima Kwaraa ambapo pale watalii wanaweza wakapanda. Tuna maji ya moto Kiru, tuna maji ya mungu Singu na wakilala pale Babati inaweza ikawa *exit* yao kuja Kondoaa kuangalia mambo mengine hapa Kondoaa ambako mnayo kwenye Wizara yenu. Kwahiyoo niwaombe mitazame hili kwa upya, badala kutumia milioni 600 kwenye barabara ya kilomita sita ya Kibaoni tu mkatumia milioni 600 *ku-maintain* ni vizuri pia mka-*maintain* malango haya matatu... (*Makof*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisa kwa muda wa
Mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa kengele imegonga nakushukuru sana, Mheshimiwa Vedastus Ngombale atafuatiwa na Mheshimiwa Maftah Nachuma wote hawa ni dakika tano tano, Mheshimiwa Boniface Mwita Getere ajiandae.

MHE. VEDASTUS E. NGOMBALE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nianze na kuwapongeza Mheshimiwa Kigwangwala na Mheshimiwa Kanyasu kwa kazi nzuri, hongereni sana mnakwenda vizuri. Mimi nianze na suala zima la utalii; kwa sababu ya kazi yenu nzuri, sasa tunazidi kupata watalii wengi lakini kuna maeneo ambayo huko mwanzo walikuwa wanapatikana watalii wengi lakini sasa watalii wamepungua. Kwa mfano ukisoma ukurasa wa 94 katika lile jedwali la vyanzo vya kale katika sehemu za Kilwa mwaka 2014, 2015 watalii waliflikia mpaka 2700 lakini sasa hivi watalii wamepungua. Sasa hii inaonesha namna gani ambavyo Wizara bado hajajizatiti katika kuendeleza utalii hususan katika eneo la mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo kilichotajwa pale ni kimoja tu ilhali sisi tunavyo vyanzo vingi. Kwa mfano tuna chanzo cha Pango la Nang'oma ni pango kubwa tu lakini

pale sijaona kama kimefanyiwa chochote. Kutokana na hilo kwa sisi watu wa kusini bado inaonekana neno utalii kwetu ni msamati, na ni msamati ambao tafsiri yake hujajua maana yake. Kwahiylo naomba Wizara ijaribu kutoa elimu kwa wananchi ili waweze kuona namna gani wanajihuisha kwenye utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ambalo ningependa kusema, niwapongeze kwa kutoa ruhusa sasa ya kufanya ule uwindaji wa wenyiji, sasa wenyeweji wanawenza wakanufaika maana sasa wanyama wamekuwa wengi na sisi tumezikaribia mbuga zile lakini hatupati chochote; kwa hiyo kwa ruhusa hii itawasaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna changamoto moja. Mwaka 2014 kama sikosei kulikuwa na operesheni ile ya Tokomeza ambayo ilisababisha kunyang'anya zile silaha za wenyiji; silaha zote zilinyang'anya na mpaka sasa hivi ninavyozungumza zile silaha bado hazijarudishwa. Sasa kama mmeruhusu silaha walizokuwa wanamiliki wenyiji kihalali bado mnazo ninyi hilo nafikiri nalo litakuwa tatizo. Nomba Wizara ishughulikie ili warudishiwe zile silaha ili na wao waweze kunufaika kuwindha katika maeneo haya ya wazi kama eneo la Kilwa na sehemu nyiningine.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu tembo. Tembo wameongezeka sana, na sisi ambayo majimbo yetu yanapakana na Selou imekuwa shida. Ukitaka kwenda baadhi ya vijiji ni lazima ule-*timing* kwamba sasa hivi huwezi kupita sasa hivi unaweza kupita. Kule kwangu katika Kijiji cha Mkarango tembo ameshawahi kuua mtu katika kipindi cha miezi miwili iliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi naomba Wizara ijaribu kuwa na *connection* nzuri na watu wale wa maliasili ili yanapotokea haya matatizo tunapotoa taarifa kwenu haraka sana waje ili waweze kuwarudisha tembo, vinginevyo basi muangalie njia nyiningine ambao zinaweza kusaidia kudhibiti hawa tembo; tembo wamekuwa wengine sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala zima la ustawi wa watu wa kusini ambao wanakaribiana na vyanzo na vivutio vya utalii na hususan sisi ambao tunakaribia Pori la Akiba la Selou. Niseme tu kwamba labda Wizara iangalie upya namna ya uwekezaji wa rasilimali hizi za utalii. Sisi kule kusini tuna pori tuna Mji wa Kale wa Kilwa na vivutio vingi lakini mpaka sasa hatuna chochote, yaani hakuna yale manufaa ya moja kwa moja. Kama chuo hatuna hata chuo kimoja cha utalii; basi Wizara angalieni namna ambavyo sisi tunaweza tukanufaika moja kwa moja, maana ukikaribia waridi basi na wewe unukie.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ni kama tumekuwa watunzaji tu wa yale mapori; na ndiyo maana utalii kwetu kimekuwa ni kitu cha mbali sana. Kwahiyio Wizara hebu jaribuni kutengeneza kitu ambacho kitakuwa motisha kwa watu wa kusini na wao waukaribile utalii hiyo itatusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine naomba Serikali ishughulikie mgogoro kati ya Vijiji vya pale Zinga Kibaoni. Kuna Kijiji cha Ngarambi, Kijiji cha Mtepela na Kijiji cha Namatewa na Hifadhi ya Selou bado kuna migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, na la mwisho kabisa ninaomba sasa basi hili wenzangu wengi wamelifanya, watu kama kina Samata watumike vizuri ili basi utalii uweze kwenda... (*Makofi*)

(Hapa kengele ililiakuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa shukrani, Mheshimiwa Maftaha Nachuma dakika tano, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere dakika tano atafuatiwa na Mheshimiwa Jackline Msongozi

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi; nimshukuru Mwenyezi Mungu na niombe kuchangia Wizara hii kwa dakika hizo nilizopata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli kabisa nikiri kwamba Wizara hii sasa hivi imepata majembe, tunaamini kabisa ni majembe ambao wanaweza wakafanya kazi yao sawasawa. Mheshimiwa Kigwangala kipindi umepata ajali ulikuwa kwenye mihangainko yako hiyo ya kuhakikisha kwamba Wizara hii inakaa sawa, mwenyezi mungu akubariki sana na Mheshimiwa Naibu Waziri pia nimeshawahi kukuona Mtwara umekuja pale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ya kwangu ni machache; jambo la kwanza; kwamba hiki kitabu cha hotuba ya Waziri, hii picha iliyowekwa hapa mbele ni picha ya jengo la kale liliopo mbele ya nyumba yangu pale Mtwara Mikindani. Jengo hili ni mionganoni mwa majengo ambayo kimsingi yaani kama kweli Wizara ingekuwa na nia ya dhati ya kuhakikisha kwamba TTB inatangaza, inatangaza sawasawa vivutio hivi ambavyo vipo Mtwara Mikindani mimi naamini kwamba watalii wangemiminika wengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo hili ni jengo ambalo lilitumiwa na Wakoloni na wakati huo jengo hili lilitumika kama *Custom*, kama magereza na kama ofisi zote za Serikali; yaani ofisi ya mkoa na ofisi ya wilaya vilevile ofisi. Kila kitu kilikuwepo ndani ya jengo hili ambalo liko kwenye picha hii. Jambo ninaloomba, Wizara ihakikishe kwamba sasa hivi kwasababu; tumekuwa tunaangalia hapa picha kwenye simu jana kuna dereva mmoja kamgonga mnyama twiga; twiga ni mnyama mpole sana. Sasa kwa sababu hawa wanyama wanagongwa gongwa, na pia mazingira na hali ilivyo hivi sasa hawa wanyama wataisha kwahiyoo utalii utabaki kwenye mambo kale.

Mimi niiombe Serikali iwekeze kwenye kutangaza mambo kale. Mji wa Mikindani ni mji wa kipekee sana; Mheshimiwa Ngombale ameongea hapa, Mji wa Kilwa ni mji wa kipekee sana, una majengo mengi ya kale. Kama tukiamua kutangaza sawasawa TTB kafanya kazi yake tunaamini kwamba Serikali itaongeza idadi ya watalii. Tuanze na Mji wa Mikindani mji mkongwe wa mikindani ambao uko Mtwara Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo linguine, kuna fedha zinaitwa fedha za *REGROW* kazi yake ni kukuza utalii ukanda huu wa Kusini. Nilikuwa naomba kujua, nimekuwa nikzisikia fedha hizi kwa muda wa miaka minne hivi sasa. Hizi fedha zimeletwa ama zipo kwenye makaratasati tu? Kama zimeletwa kule kwetu kusini mkakati upoje? Kwa sababu kuchanganya, yaani leo hii watu wanavyosema kwamba Kusini wanazungumza Mbeya wanavyosema kusini wengine wanazungumza Morogoro. Kusini ni Mtwara na Lindi, kwamba kusini Kiserikali nchi hii ni Mtwara na Lindi. Kwahiyu tunataka Serikali kama fedha zimepatikana fedga za *REGROW* zije kutangaza utalii kusini Mtwara pale kwenye mji wa Mikindani, kule Kilwa Kaskazini na kule kwenye msitu ule wa Selou uliopo Lindi; tunaomba hizi fedha ziletwe kule. Isiwe inazungumzwa tu Iringa Kusini; watu wanazungumza Iringa wanazungumza Mbeya na Mtwara na Lindi mnaisahau. Kwa hiyo naomba hizi fedha za *REGROW* ziletwe kweli Kusini kwenyewe, kusini halisi ambako ni Mtwara na Lindi tunashida ya kutangaza vivutio vyatia kitalii na kuboresha ...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: ...katika mji wa Selous.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nilikuwa naomba nizungumze kuna hizi fukwe za bahari. Kuna fukwe za bahari kule kusini kuanzia pale Mnazi Bay Mtwara ni fukwe ambazo ni za Kimataifa, Wakoloni wote walipitia kwenye fukwe ya Mnazi Bay wakajenga mahema yao pale akina Vasco Dagama, akina nani na wengine wengi sana; wakaja mpaka Mji wa Mikindani wakajenga mahema yao pale. Hizi fukwe zimesahaulika; ni fukwe nzuri kuliko fukwe zote duniani; fukwe ya Mnazi Bay ipo, Mtwara Vijijini pale na Msimbati. Nilikuwa naomba Serikali kama imeisahau hii fukwe ihakikishe ya kwamba inatangaza hii fukwe; watu wa TTB waje kuiangalia hii fukwe kwa sababu Wajerumani wameweka kwenye *page zao* zote duniani; kwamba mionganoni mwa maeneo ambayo wamepita maeneo muhimu ya fukwe muhimu Tanzania ni fukwe ya Mnazi Bay ambayo iko Mtwara Mikindani; naomba Wizara ije kuiangalia hii fukwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilikuwa naomba kujua; kuna suala la wauza mikaa. Wauza mikaa imekuwa ni kero sana kule Mtwara, wanakamatwa sana. Yaani mtu akishikwa na gunia moja na mkaa anapigwa sana na watu wa maliasili, ukiwaliza wanasema wanataka walipe ushuru. Sasa hawa wauza mikaa ni watu masikini kabisa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, muda umekwisha, ahsante sana; lakini umezungumza kuhusu mikoa ya kusini, kuna mikoa ya kusini na kuna Nyanda za Juu Kusini, kwahiyio hayo mambo mawili lazima uyatofautishe na kwenye Nyanda za Juu Kusini; nadhani Mtwara na Lindi hawaopo kwenye Nyanda za Juu Kusini. Tunaendelea na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere dakika tano, Mheshimiwa Jacqueline Msongozi atafuatia halafu Mheshimiwa Margreth Simwanza Sitta ajiandae

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye hii hoja ya maliasili. Kwanza niwashukuru ndugu zangu wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii; kimsingi ni kwamba Wizara hii sasa imetulia, na tumewapa sifa nyingi Kigwangala, mwenzako Kanyasu, Katibu Mkuu na wengine wote wa TANAPA na mambo ya misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hofu yangu ni kwamba tumewasifia sana sasa msije mkafanana na timu fulani iliyofanya mambo yake jana tukayaona; kwamba mkishasifiwa halafu mnarudi nyuma halafu mnapigwa magoli huko mbele mnakokwenda. Kwahiyio naomba tu-*maintain* hiyo ambayo tumewasifia muendelee kuwa nayo tu msifanane na mambo ya Simba ya jana ili muendelee kufanya vizuri huko mnakoenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tofauti kubwa sana ya kuhifadhi mazingira au kuhifadhi kwa jumla ya mbuga zetu

na kufanya biashara ndani ya mbuga zetu, tofauti ni kubwa sana. Tukisema kuhifadhi tunaweza kuweza askari kwenye mbuga zetu zote, *national parks na game reserves*; wakazunguka, hakuna mtu anaingia na sisi tunaendelea kuhifadhi kilichopo mle ndani. Tukisema kufanya biashara katika mbuga zetu tunahitaji tuboreshe miundombinu katika *national parks* zetu na *game reserves* zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapo ndipo kuna shida. Tunataka hela ndani ya *game reserve*, tunataka hela ndani ya *national park* lakini miundombinu yetu yote katika maeneo yote ni mibovu; na *national parks* tunazozitaka zote ni kama tano ndizo zinazofanya biashara vizuri. Kwahiyo tunaomba sasa Serikali yale makato na TANAPA, tumezungumza na Waziri wa Fedha, tumezungumza kwenye Kamati, Spika alizungumza hapa, Bunge linazungumza, shida ni nini? Sisi tunataka mapato yaje ninyi mnazuia. Kwahiyo naomba sasa kwenye kipindi hiki Serikali na hasa Waziri wa Fedha aweke jambo hili, wapunguze tozo kwa kwenye *national parts* TANAPA ili ipate nafasi ya kuweka miundombinu kwenye maeneo yetu ili wafanye biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo limezungumzwa *Stiegler's Gorge* hapa, mwenzangu Dkt. Mollel amelizungumza vizuri lakini na mi niliweke vizuri. Duniani kote tunapozungumza mazingira tunazungumza *climate change*, tunazungumza *ozone layer*; na leo tunapozungumza *ozone layer* 0.0% ya *ozone layer* inaenda kumomonyoka. Marekani tangu imeundwa imeshindwa kuleta sheria za kurekebisha *ozone layer*, kwa maana ya *climate change in house*. Kupunguza hewa ukaa ambayo ni *carbon dioxide*, tangu dunia imeundwa Marekani haijapunguza kwasababu ya *interest* ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Uingereza wanataka kujitoa kwenye muungano kwasababu wanataka kulinda paundi; wanataka kulinda fedha yao. Sisi leo tunazungumza habari ya kujenga *Stiegler's Gorge* kuna mtu anasema oo hatutapata umeme, hatupata wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusema kitu kimoja, kwamba hao wenzetu wakati fulani nawashangaa, tukisema tunapitisha bajeti hawataki, tukijenga vituo vy aya wanatangaza wao, tukijenga barabara wanatangaza wao, wanasema umeme hawautaki lakini ukija wanatumia wao; sasa shida ni nini? Tufike wakati tukubaliane; kwamba sasa umeme wa *Stiegler's Gorge* ukitoka kwenye maeneo ya hao amba o hawataki *Stieglers Gorge* wapelekewe umeme wa gharama kubwa na umeme wa bei nafuu uende kwenye maeneo yetu. Tunashangaa sana hili suala la *Stieglers Gorge* lilishaisha jamani; Mheshimiwa Msigwa wewe ndiyo uko hapa tulishamaliza hilo jamani wewe ni mjumbe, tulishamaliza, tatizo liko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze kuhusu hifadhi ya kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. Makumbusho ya Mwalimu Nyerere tunaomba ...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwita Getere naomba ukae, Mheshimiwa Msigwa kanuni iliyovunjwa,

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Kanuni ya 64 Mbunge hatasema uongo ndani ya Bunge. Hakuna mahali ambapo sisi kama Wabunge wa Kambi ya Upinzani tumesema hatuutaki umeme, Bunge ni mahali ambapo tunatoa maoni tofautitofauti na hatimaye tunakuja na hitimisho lilio bora. Maneno anayoyazungumza ni ya kuligawa Taifa kwamba watu wengine wasipate umeme umeme huu siyo mali ya CCM, kodi ni mali ya wananchi. Kwahiyoo ningeomba tuongoze kwasababu anasema uongo sisi hatujasema hivyo kama Wabunge.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mmemsikia Mheshimiwa Msigwa kuhusu uchangiaji wa Mheshimiwa Mwita Getere kuhusu mradi wa umeme na maneno aliyoyssema kwamba pengine kuna watu hawahitaji umeme ama kwa namna moja wanataka kuzuia umeme usipatikane.

Kwa mujibu wa taarifa anayoitoa Mheshimiwa Msigwa ni kwamba hakuna taarifa hiyo kwenye kitabu cha Kambi ya Upinzani lakini pia wachangiaji wa upande wa Kambi ya Upinzani hakuna aliyesema hataki umeme.

Kwa hiyo Mheshimiwa Mwita Getere katika mchango wako changia kwa namna ambayo haioneshi kama kambi ya upinzani imekataa umeme.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea; nilikuwa nazungumzia kuhusu Makumbusho ya Mwalimu Nyerere. Kwa hiyo naomba; Mheshimiwa Kigwangwala kwa kweli pale ndiyo mahali ambapo kuna barabara inayotoka Kilawila inapita Mgeta kwenda Makumbusho ya Mwalimu Nyerere; ni muhimu sana kwenye hiyo barabara kwasababu tunataka tuunganishe pori la Serengeti na Makumbusho ya Mwalimu Nyerere. Jambo hill tumelizungumza kwenye Kamati na nafikiri kwamba tulizingatvie; kwa sababu makumbusho ya mwaka huu ya Mwalimu Nyerere nafikiri barabara hii ndiyo itatumika; tumezungumza sana kwenye jambo la namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilikuwa nataka nizungumze jambo moja tu ambalo linaweza kuwa lina maana sana katika mambo haya. Haya mambo ya hifadhi ya wanyama pori yanahitaji ushirikiano kati ya viongozi wa wanyama pori au viongozi wa Wizara na wananchi wanaozunguka maeneo hayo. Tumekuwa na tatizo la kulipa fidia *billions of money* kila mwaka; lakini tumeona kuna nchi zingine wenzetu wanaweka ukuta wa kutumia nyaya za umeme; tumeona kwenye maeneo mengi. Tumeona Botswana, nimekwenda *South Africa* nimeona baadhi ya maeneo; wanaweza kulinda wanyamapori wanaoingia kwenye watu. Haya mamilioni tunayotumia kulipa fidia kwanini isitumike kujenga huo ukuta wa umeme? Kwanini tunang'ang'ania vitu ambavyo kila siku vinafanya kazi ambayo inaleta hela ambazo hazipo sana?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana, niwashukuru wote wa Wizara, niwapongeze, na

Waheshimiwa Wabunge wote tuwaombe hii Wizara iko vizuri tupliche bila matatizo yoyote; ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwita Getere kwa ajili tu ya kumbukumbu vizuri nadhani Simba jana ilishinda kipindi cha kwanza mbili bila kipindi cha pili ikawa ndiyo moja bila. Kwahiyo Sevilla walishinda moja bila Simba wakashinda mbili bila. Mheshimiwa Jacqueline Msongozi atafuatiwa na Mheshimiwa Margreth Sitta, Mheshimiwa Josephine Gezabuke ajiandae.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Niende moja kwa moja kwenye hoja zangu za msingi. Hoja ya kwanza inahu suala la utalii. Nichukue nafasi hii kuipongeza sana Wizara kwa kazi nzuri ya ubunifu ambayo inaifanya; mpaka sasa tunaona kwamba watalii wamekuwa wakijia kwa wingi kutoka nchi mbalimbali; Israel, Malaysia, China na maeneo mengine, hongera sana kwa vijana ambao wanafanya kazi katika Wizara hii na siku moja Mheshimiwa Dkt. Kigwangwala alisimama hapa akasema yeye si wa mchezo mchezo; hii imejidhihirisha wazi katika utekelezaji majukumu yao ambayo wanayafanya pamoja na Naibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua kwamba huu Mradi wa Utalii katika Mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma ni lini utapelekwa na unapita kwenye maeneo gani? Nataka kusema kwamba kule tuna *Selous Game Reserve*, tuna Liparamba, tuna Makumbusho ya Majimaji, lakini tuna zoo moja ya Ruhira pale ni zuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile pale Njombe tuna nyumbanitu, nyumbanitu ni maeneo ambayo yana vitu vya ajabu ajabu sana. Kuna kuku wapo mle wanaishi kwenye ule msitu hajulikana nani amewafuga na wapo humu wakiwa na rangi nyeusi. Pia wapo ng'ombe wanazunguka kwenye hilo eneo, hajulikani nani amewaweka, kwa hiyo ni nzuri sana watalii wakienda kwenye maeneo haya yakiwemo pamoja na maeneo hayo ya Mkoa wetu wa Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie Mto Ruvuma; mto huu umekuwa na mamba wengi sana ambao wamekuwa wakileta athari kubwa sana kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma. Niwaombe Wizara ije iwavune hawa mamba, lakini pia siku moja nilimsikia Mheshimiwa Mulugo alizungumza hapa kuhusu Ziwa Rukwa napo kumekuwa na mamba wengi sana. Wizara ifanye juhudzi za makusudi kuwavuna hawa mamba ili wasiendelee kuleta athari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa tatu kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake, aya ya tatu lakini pale imeandikwa namba tisa, naomba niseme suala ambalo Kimsingi linatia huzuni, lakini pia tumekuwa tukiwazungumzia sana ndugu zetu ambao wamekuwa wakiathirika na masuala hasa yanayozunguka kwenye maeneo ya wanyamapori. Tumekuwa tukisahau kuwazungumzia askari wetu ambao ndio wanasi mamia na kulinda rasilimali hii ya Tanzania. Askari hawa wamekuwa wakijeruhiwa, wangine wamekuwa wakichomwa na mishale ya sumu, wengine wamekuwa wakujeruhiwa na hawa majangili, wamepoteza maisha, nimeona kwenye hii aya wapo zaidi ya 11.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana, hawa vijana wamejitoa wengine wanaumwa na nyoka, wanalala huko porini tuwatie moyo. Niombe sana Wizara hii, kwanza niwape pole kwa kupoteza hao vijana, lakini pia niombe stahili zao wanazostahili wapewe. Ikiwezekana waongezewehata kiwango cha mshahara ili waweze kufanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala ambalo Mheshimiwa Waziri amesema kwamba anatupa *offer*. Mheshimiwa Waziri tunakushuru sana kwa hii *offer* ya futari. Hata hivyo, niombe amekuwa akitupa futari kila wakati tunamshuru sana, lakini safari hii afanye kitu kingine mbadala, ataulike Bunge zima kwenda kufanya utalii katika Mbuga ya Ngorongoro, Serengeti, Saadani na maeneo mengine, futari tumekula sana baba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Mawaziri wanafanya kazi nzuri sana, waendelee kuchapa kazi. Matarajio ya Mheshimiwa Dkt. John Joseph Magufuli anayoyatarajia kufikia mwaka 2020/2025 ni makubwa na wao ndio vijana amewaweka na amewaamini, waendelee kuchapa kazi. Kazi zao ni nzuri, wanasikiliza watu vizuri, wanatoa maelekezo vizuri, tunawashukuru hawajidai wala nini. Pia Makatibu Wakuu, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu wapo vizuri, nimekwenda ofisini kwa Katibu Mkuu amenisikiliza vizuri na tatizo langu likatatuliwa kwa haraka, nashukuru sana.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kengele imeshagonga muda umeshaisha.

(Hapa Mhe. Jacqueline N. Msongozi aliendelea kuongea wakati muda umekwisha)

NAIBU SPIKA: Muda umeshakwisha Mheshimiwa Msongozi Ahsante sana. Mheshimiwa Margaret Sitta atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji ajiandae.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja iliyopo mezani. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na wakati huo nawashukuru sana wananchi wa Urambo kwa kunipa ushirikiano wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Kigangwalla, Naibu Waziri Mheshimiwa Kanyasu, Wakuu wa Idara wote wa Misitu, Wanyamapori na kadhalika. Watendaji wote kwa kweli Wizara hii wanastahili sifa hongereni sana. Wameanza

vizuri, tunawatakia kila la heri, waendelee na kazi kubwa wanayoifanya hadi wakati huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kushukuru ushirikiano ambao nimeshakuwa naupata na Wizara hiyo. Kwa mfano, alipokuwepo Naibu Waziri wakati huu Mheshimiwa Hasunga nilimwelezea kuhusu mgogoro wa mpaka nilionayo na tukaenda naye mpaka Urambo namshukuru sana. Aliiona, akajaribu kusuluhisha lakini baadaye akaondolewa kwenye Wizara hiyo. Kwa hiyo naamini waliopo watafuatilia huo mgogoro ambao nazungumzia kati ya wananchi na mipaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui kama wenzangu Waheshimiwa Wabunge kama wanajua Urambo nasi tuna *game reserve*, wanaongelea Ngorongoro lakini wasisahu na sisi Urambo tuna *game reserve*, kuna wanyamapori hawa wanaowaona huko nasi tunao, lakini pia tuna Hifadhi ya Msitu wa Ugalla.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kumekuwa na mgogoro wa mipaka kwa muda mrefu hasa katika Kata za Nsenda, Ukondamoyo, Ugalla na Uyumbu na hasa katika maeneo ya Lunyeta ambapo tulikwenda na Mheshimiwa Hasunga, Holongo, Utenge, Mwagimagi, Izengabatogwile, Magangi, Tebelia na sehemu nydingi tu, chanzo chake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaambie Wizara kwamba katika miaka 2007 Serikali ilirasimisha mipaka ya vijiji na wakaweka mawe ambayo yapo mpaka sasa. Baada ya kurasimisha mipaka Wizara ya Maliasili na Utalii nao wakaja na mipaka yao ambayo ikawarudisha nyuma kama kilometra 54 hivi na bahati mbaya wakachomewa nyumba na mali zao. Tukalileta hapa hapa wakati huo akiwa Mheshimiwa Pinda, Waziri Mkuu kwa sababu tume iliundwa na matokeo yake yakaonekana kweli wale wale wananchi walionewa. Wamechomewa mali zao, lakini walikuwa katika mipaka ambayo ni halali ambayo ipo mpaka sasa kwa kurudishwa nyuma. Tukawabembeleza wananchi wale tukasema suala hili litaendelea kushughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipaka ile sasa ipo miwili, mpaka wa Serikali wa kwanza ambao ni wa halali kabisa na Mheshimiwa Hasunga aliiona. Wananchi wa kule wameendelea wanakuonesha mipaka kwa kufukua kwa mikono tu. Kwa hiyo kuna mipaka kwa kufufua kwa mikono tu kwa hiyo kuna mipaka ile ya zamani ipo na ni mipaka ya sasa hivi ambayo imewarudisha nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni nini? Ni kwamba, sasa Serikali iende ikakae na wananchi ione, nami ningetoa wito kwa Serikali yenyewe kuwa ni Maliasili lakini waende na Ardhi kwa sababu wao ndio waliweka ile mipaka ya kwanza kabla Maliasili hajaja na mipaka ya pili. Kwa hiyo wananchi wanaomba waende wakaone na nitafurahi sana kama watafuatana na uongozi wa Wizara ya Ardhi ili wakaone kosa la wananchi nini, walikaa pale kihalali lakini wakawachomea mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maliasili ilipokuja na mipaka ya pili ndio ikasababisha wale wananchi hawapo pale kihalali. Sasa wananchi wanauliza, je, mpo tayari kuwarudisha pale walipokuwa? Kwa sababu kwa kuwapunguzia kilomita nne sasa hivi hawana mahali pa kutosha pa kulima na walizoea mashamba yao na wafugaji pia hawana mahali pa kufugia. Kwa hiyo tunaomba sana Serikali iende kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuna tatizo...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda umekwisha Mheshimiwa, pole sana. Mheshimiwa Genzabuke atafuatiwa na Mheshimiwa Ashatu Kijaji tutamalizia na Mheshimiwa Subira Mgusu.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuruku kwa kunipa nafsi hii. Naomba niungane na wenzangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Dkt. Kigwangalla pamoja na Naibu wake

Mheshimiwa Kanyasu, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja. Pia naomba niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuweza kuruhusu baadhi ya maeneo ya wafugaji na wakulima waweze kupatiwa maeneo ya kulima na maeneo ya malisho.

Vilevile naomba niendelee kusema kwamba maeneo ya kilimo na malisho ya mifugo yameendelea kupungua kutokana na ongozeko kubwa na watu hivyo basi, unakuta eneo la kilimo halitoshi, lakini pia eneo la malisho ya mifugo haitoshi. Ombi langu, Serikali iweze kuridhia kupunguza eneo la hifadhi na maeneo ya akiba kurudi kwa wananchi ili waweze kupata maeneo ya kulima na maeneo ya kulishia mifugo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali izingatie kauli ya Mheshimiwa Rais kwa kuweza kuendelea kutenga maeneo ya wafugaji na wakulima. Ukiangalia migogoro mingi iliyopo nchini ni kutokana na upungufu wa ardhi ya wananchi kulima lakini pia na malisho ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwetu Kasulu, Eneo la Akiba la Makere Kusini, bado kuna mgogoro mkubwa pamoja na kwamba Serikali imeongeza eneo kidogo, lakini bado wananchi wana mahitaji makubwa ya kupata eneo la kulima kwa sababu watu wameongezeka, ardhi inabaki kuwa ile ile naomba Serikali iweze kuruhusu kuongeza kipande kingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe watu wa *TFS* waache kuwasumbua wananchi, waendelee kuwaelimisha, kwa sababu nimeshawahi kusimama hapa kulalamika kuhusu watu wa *TFS* wanavyowasumbua wananchi. Naomba wawaelimishe kwa kukubaliana na kuwaelekeza jinsi gani wanatakiwa kufanya kuliko kuchukua wakati mwingine mali zao, kuchukua pipipiki wakachoma, wakati mwingine kuchua baiskeli zao. Wawaelimishe, wakae nao wakubaliane ili wote waweze kutoka kwa pamoja.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Kengele imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa shukrani zangu kwako kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika Wizara hii. Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimaye kuwasilisha katika Bunge lako Tukufu hotuba hii kwa ufanisi mkubwa. Katika kuchanglia hotuba hii napenda kutoa mchango katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Utalii; napenda kuipongeza Wizara hii kwa mikakati na matayarisho mazuri katika Idara hii ya Utalii. Hii ni Idara muhimu sana katika tasnia ya utalii. Ni idara ambayo inatakiwa iweze kupanga mipango mikakati ya kuongeza watalii nchini. Utalii ni mionganoni mwa vyanzo vizuri katika nchi yetu, hivyo idara hii inafanikiwa kujua hilo na kulitafsiri kwa vitendo ili kufikia azma hii ya kuwa chanzo cha nchini katika nchi yetu badala ya kutegemea vyanzo vingine ambavyo havina uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu mwingine katika Idara hii ni kutayarisha mazingira ambayo watalii wanaokuja nchini waweze kufika katika vivutio vyetu vyote hasa vile vya Zanzibar. Zanzibar ni sehemu ambavyo vivutio vyake ni vya bahari na huku bara vivutio vyake vingi ni vya mapori, hivyo ni vizuri kuwaonesha watalii wanaokuja nchini vivutio vya aina tofauti vilivyopo kwenye nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. RHODA S. KUNCHELA: Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi na utekelezaji wa bajeti; makato ya mshahara zaidi ya shilingi bilioni 168 kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo hayakupelekwa katika taasisi husika (*CAG* Ripoti ya Ukaguzi wa Serikali Kuu 2017/2018 ukurasa 189).

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ambazo hazina mpango wa matengenzo na kumbukumbu za matengenezo ya mali za kudumu (Maliasili na Utalii) ukurasa wa 287. Kwa mujibu wa *CAG* mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Maliasili ina kesi Mahakamani baina yake na kampuni na watu binafsi ikidaiwa Sh.23,399,564,809 ukurasa wa 238. Kuna hatari ya kulipa fedha hizo kutoka kwenye bajeti endapo Wizara ya Maliasili na utalii itashindwa katika kesi hizo zilizoko Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni muhimu kwa ustawii wa utalii nchini katika taasisi za Serikali. Wizara hii ni kinara kwenye madeni makubwa kuliko taasisi yoyote, kiasi hicho ni zaidi ya fedha za bajeti ya maendeleo. Wizara hii imefanya matumizi ya Sh.3,559,102,398 na hajalipwa. Waziri akija kuhitimisha ajibu jambo hili likoje?

Mheshimiwa Naibu Spika, safari za *ATCL* kutochochea ukuaji wa utalii nchini. Uamuvi wa kufufua Shirika la Ndege la Tanzania (*ATCL*) ulipaswa kwenda sambamba na sokola utalii nchini. Kwa sababu Sekta ya Utalii ndiyo sekta kinara wa ongezeko la mapato ya kigeni na takwimu zinaonesha Kenya ndiyo inaongoza kuleta utalii nchini baada ya Marekani na tatu Burundi. Sasa jambo la kushangaza *ATCL* imetangaza kwa itaanza kufanya safari mara nne kwa wiki kutoka Dar es Salaam – Afrika Kusini. Ukiangalia masoko 15 yanayoongoza kuleta idadi kubwa ya watalii nchi ya Afrika Kusini ni ya nane. Sasa naomba Waziri akija kujibu anijibu yafuatayo:-

Je, kama hatuwezi kuitumia *ATCL* kuchochea soko la utalii tutaitumia kwa ajili ya kukuza sekta ipi? Napenda pia kujua uamuvi wa kupeleka *ATCL* Afrika Kusini baada ya kuanza na safari ambazo kuna soko kubwa la utalii, uamuvi huo unatokana na nini? Pia ni kwa namna gani ndege mpya

ya ATCL mfano *Dreamliner* zinavyotumika kuchocha Sekta ya Utalii nchini? Napenda kujua kama upo mkakati kabambe wa kuyafuata masoko hayo ya utalii?

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya hifadhi na wananchi Mkoa wa Katavi; kuna migogoro inayoendelea katika Jimbo la Mpanda Vijiji, Kata za Vijiji vya Lyamgoloka, Iseganyanya, Isengule, Chamalendi, Ihefu, Kapalambsenga, Ikola, Karema. Wananchi hawa wanateswa na Askari wa Maliasili kwa maagizo kutoka kwa Mkuu wa Wilaya Mheshimiwa Mhando, wanapigwa risasi, wanachomewa nyumba na mifugo yao inatozwa faini kubwa. Sasa nataka kufahamu ni sheria gani inatumika kuwanyanyasa hawa raia wakati lengo la Serikali ni kutatua na si vinginevyo?

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa fursa hii. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa hotuba nzuri asubuhi ya leo. Katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 16 amezungumzia juu ya mpango wa ukuzaji wa utalii Kanda ya Kusini (*REGROW*) ambao unaenda kukuza utalii katika ukanda huo. Mpango huu bado hausemi chochote juu ya utalii katika fukwe za Pwani ya Kusini hususan Kisiwa cha Mafia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kisiwa cha Mafia kina vivutio vingi vya utalii ikiwemo *scuba diving, whale shark, sports, fishing, snorkeling* na fukwe nzuri. Kupitia Mpango huu wa Kuendeleza Fukwe katika Kanda ya Kusini tunaiomba Wizara iingize ujenzi wa miundombinu katika Kusini cha Mafia kama ujenzi wa barabara ya lami kutoka Kilindi mpaka Ras Mkumbi kilometra 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hilo la Ras Mkumbi Kaskazini mwa Kisiwa cha Mafia kina fukwe nzuri kwa ujenzi wa hoteli za kitalii sambamba na utanuzi wa kiwanja cha ndege cha Mafia. Kwa kuongeza urefu wa barabara ya kutua na kuruka (*runway*) kutoka urefu kama kilometra 1.6 ya sasa mpaka kufikia kilometra 3.0 ili kuwezesha ndege kubwa kutoka nchi za nje kutua Mafia moja kwa moja. Upanuzi wa

uwanja ulenge kwenye kujenga jengo kubwa la abiria na eneo la maegesho ya ndege (*apron*).

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wanyama waharibifu akiwemo boko bado ni tatizo. Katika Kisiwa cha Mafia tunashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri Kanyasu alifanya ziara na kusaidia upatikanaji wa fidia ya aliyepoteza maisha kwa kushambuliwa na boko na wale walioharibiwa mazao yao. Hata hivyo bado tatizo halijakwisha na viboko wameendelea kuingia mashambani na kula mazao na kutishia maisha ya wananchi. Niendelee kuomba Serikali itupatie kibali cha kuvuna viboko hao kwani idadi yao imeongezeka maradufu. Vile vile Serikali iangalie uwezekano wa kujenga uzio kuzunguka maeneo ya mabwawa wanamoishi viboko hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni *Channel ya TV* ya utalii haioneshi vivutio vya Kisiwa cha Mafia. Tunaomba wahusika waje Mafia kurekodi katika *channel* hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naunga mkono hoja.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapa pole sana viongozi na watendaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kazi kubwa wanayofanya pamoja na changamoto za rasilimali kidogo. Naiomba Wizara hii muhimu kwa uchumi wetu ione umuhimu wa kutembelea Jimbo la Moshi Vijijiini kwa ajili ya kutambua vivutio vya utalii katika Kata za *Old Moshi Mashariki* na Uru Mashariki (Materuni) ambapo kuna maanguko ya maji (*waterfalls*) ya ajabu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vivutio hivi havijaweza kuwa vyanzo vya maana vya mapato kutokana na miundombinu ya barabara na vyoo kuwa mbaya sana. Nikilinganisha na vyanzo vya aina hiyo mahali pengine duniani naona kinachokosekana kwetu ni matangazo na kuboresha miundombinu tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, niombe Wizara ikaone mti ulio katika Kata ya Mbokomu ambao ni mrefu kuliko yote Barani Afrika na wa sita duniani. Watu toka sehemu mbalimbali duniani toka ugundulike wamekuwa wakiutembelea, jambo ambalo linaweza kusababisha madhara kwa mazingira ya eneo hilo, hasa uoto wa asili ikiwa hapatakuwepo na utaratibu wa kuuendea mti huo na hifadhi yake. Mti huu unaweza kuwa chanzo cha mapato pia.

MHE. ENG. GERSON H. LWENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hoja hii na nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na viongozi wa Wizara hii kwa kazi nzuri ya kusimamia majukumu ya Wizara hii. Mwaka jana wakati wa kuwasilisha hoja ya bajeti kwa Wizara hii nilichangia kuhusiana na kuwepo kwa Pori la Akiba la Mpanga/Kipengele lilianzishwa mwaka 1995; wananchi wa vijiji 14 vya Wilaya ya Wanging'ombe walihamishwa kupisha uanzishaji wa pori hili la akiba, walilipwa fidia na mipaka iliwekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hao wamejenga nyumba za kudumu, shule, majengo ya ibada na kadhalika. Hivi karibuni Mamlaka ya TANAPA wamekuja kuweka vizingi tofauti na mipaka ya awali bila kuwahusisha wananchi au viongozi wa wilaya. Jambo hili limeleta tataruki na hivyo kuzusha mgogoro mkubwa. Jambo hili nilimfikishia Mheshimiwa Waziri ili achukue hatua ili wananchi hawa waishi kwa amani na vilevile azma ya kuwepo hifadhi ya pori la akiba iwe endelevu. Nilitarajia ningeona lolote ndani ya hotuba hii, lakini sijaona mpango wowote uliopo kwa ajili ya pori hili la Mpanga Kipengere, kwa hiyo, lipolipo tu. Basi kama ni hivyo naomba ramani ya awali iheshimiwe na vijiji hivi viliviyosajiliwa viachwe viendeleze maeneo yao. Vijihi hivyo ni Moronga, Kipengele, Imalilo, Ikanga, Wangama, Masage, Malangali, Wagamiko, Mpanga, Luduga, Hanjawananu, Igando, Iyayi na Mayale.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa tamko lake alilolitoa kwa vijiji vile vyenye migogoro na wananchi

kwamba, Wizara iende kutatua migogoro ikihusisha wananchi, Serikali za Wilaya na ikikupendeza kumshirikisha Mbunge wa Jimbo. Nina imani agizo la Rais linahusisha pia mgogoro uliopo katи ya Hifadhi ya Pori la Akiba la Mpanga/ Kipengele na wananchi wa vijiji hivi 14 nilivyovitaja.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Dkt. Kigwangala, Naibu Waziri Mheshimiwa Kanyasu, Makatibu Wakuu na viongozi wote wa Wizara kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. Naomba mchango wangu ujikite katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *Regrow*: naipongeza Serikali kwa kutoa kipaumbele na kuona umuhimu wa kuendeleza utalii Kanda ya Kusini (*Regrow*). Mradi huo unalenga kuongeza ubora wa vivutio vyta utalii Kusini mwa Tanzania ikiwa ni pamoja na kuimarishe fursa za kiuchumi kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ukiwemo Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze sana Serikali kwa kuanza kutua ndege kubwa aina ya *Bombadier* katika Kiwanja cha Ndege cha Iringa. Pamoja na hilo ni vyema sasa Serikali ikaboresha kiwango cha lami barabara inayokwenda katika Mbuga ya Wanyama ya Ruaha, mbuga ya pili kwa ukubwa katika Afrika na ina wanyama wengi. Wizara hii ya Utalii inatoa msukumo gani kwa Wizara ya Ujenzi na kuona hiyo barabara inaharakishwa kujengwa kwa sababu imechukua muda mrefu sana kutangazwa ujenzi, lakini haufanyiki. Naomba kujua ni elimu kiasi gani inatolewa ili kuwaandaa wananchi wanaozunguka Mradi huu wa *Regrow* wanaandaliwa ili kujajiri kuititia utalii?

Mheshimiwa Naibu Spika, Ongezeko la Watalii nchini; niipongeze Serikali kwa kufanya jitihada na kusababisha watalii kuongezeka kutoka 1,327,143 mwaka 2017 na kufikia 1,505,702 mwaka 2018 na kuongeza pato la Taifa, lakini ningependa kujua mkakati wa kuhakikisha watalii wengi wanafika katika mikoa yetu ambako kuna vivutio vingi ambavyo bado hatujaona kutembelewa na watalii wa kutosha katika Mkoa wetu wa Iringa. Je, Serikali imejipangaje

kuajiri Maafisa Utalii kila Halmashauri, Wilaya na Mikoa kwa sababu, kuna Halmashauri nyingine zina vivutio vingi, lakini hakuna Maafisa Utalii kuna Maafisa Misitu tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia Wizara hii ya Maliasili na Utalii kwa kuwa ni Wizara ambayo ni muhimu sana kwa kuliletea Taifa letu fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la katazo la kutumia mkaa; bado kuna changamoto kubwa katika ukamataji, naomba Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Muungano na Mazingira kwa Maafisa Mazingira pamoja na Maafisa Misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro kati ya wananchi na maeneo ya *reserve*; kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kwa wananchi wetu katika maeneo yao ambayo yanazunguka *reserve*. Ni vema Wizara hii ya Maliasili na Utalii kushirikiana na Wizara ya Ardhi ili kupima maeneo yao na kutatua migogoro hiyo ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya kifuta jasho imepitwa na wakati. Ni vyema Serikali ikaleta sheria hii Bungeni ili ifanyiwe marekebisho kwani imepitwa na wakati. Ni vema Wizara ikachukua hatua ya haraka kwani wananchi wana malalamiko ya muda mrefu kuhusu mazao yao yanayoliwa na wanyama, lakini kifuta jasho hakikidhi athari zinazowakabili baada ya mazao kuharibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maporomoko ya Kalambo; Wizara ichukue hatua kwa maporomoko haya kwani tunatumia nchi mbili lakini nchi ya Zambia inafaidika zaidi. Naomba kushauri Serikali kuwekeza fedha kwenye maporomoko haya ili na sisi tunufaiki kama Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tubadilishe aina ya matangazo yetu ya utalii.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, utalii na fursa ya watalii ambaao ni askari wa *UN* wanaolinda amani kupitia *UN – Mission*; kuna kundi kubwa la askari ambaao wako kwenye *UN – Mission* mbalimbali katika eneo la Maziwa Makuu na pia pembe ya Afrika. Nitafafanua kidogo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, DRC kuna *Mission* ya *MONUSCO* na Central Africa kuna *MINUSCA*. *MONUSCO* tu ina takribani watumishi 16,000, wengi wao askari kutoka Mataifa kama Pakstani, Bangladesh na Nepal. *MINUSCA* ina wafanyakazi zaidi ya 12,000, kutokana na mazingira ya kazi kila baada ya kipindi fulani hupewa likizo. Kwa sababu ya umbali wa kwenda makwao wengi hupendelea kwenda maeneo jirani kupumzika ikiwemo Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto; kwa sababu ya utaratibu wa *Visa Rejea (Referred Visa)* ambayo maombi yake huchukua muda mrefu na wakati mwininge hakuna majibu. Tunawapoteza watu hao ambaao sasa wanakwenda Rwanda, Kenya na Uganda. Hili soko kubwa ikiwa mtu huyo ameshafanyiwa *vetting* katika *level* ya *UN* na ana *passport* ya *UN*, tunakosaje kuwa na utaratibu maalum. Tufikirie kwa mwaka tukiwapata japo 5,000 tu ni mapato kiasi gani. Ikizingatia kuwa hawa ni wale ambaao *High Value Tourism* na *ni long stay* kwa sababu watakaa muda mrefu mpaka likizo yao itakapokwisha ambayo huwa ni wastani wa siku 14 mpaka 21.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri; Serikali kupitia Wizara husika ya Mambo ya Ndani (Uhamiaji) na Mambo ya Nje na wao washirikiane kuona kuwa tunafaidi fursa hii.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa siku ya leo kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uwezo wa kuchangia leo. Naomba kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na nzuri ya kuleta maendeleo anayofanya na hasa katika masuala ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Pia kwa nia yake ya dhati ya kuleta mabadiliko na

pia kuleta ndege za shirika letu la ndani ya usafiri wa anga (*ATCL*) kuboresha na kutangaza utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wote Wizarani na pia taasisi zilizo chini ya Wizara hii. Pia Wakurugenzi wa *TANAPA* na *NCCA* kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri katika maeneo machache *ili* kuboresha Sekta hii ya Maliasili na Utalii. Kwanza naomba Wizara hii ifuatilie kwa karibu kutatua migogoro baina ya hifadhi, jamii na watumiaji mbalimbali wa ardhi. Babati tuna hifadhi mbili ambazo tuna tatizo la mipaka, Tarangire ikiwa na *Vijiji* vya Ayawayo, Gedamar na Gidejabung. Wananchi walipewa fidia ya majengo yao (au maendelezo) kabla ya miaka zaidi ya kumi na walihidiwa ardhi mbadala sababu hao wananchi walipelekwa hapo na *operation vijiji* ekari 17,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni la miaka mingi sana, tunashauri eneo hilo wapewe wananchi kwa ajili ya ufgajji jambo ambalo litaendana na uhifadhi. Pia tuna eneo la Ziwa Manyara (hifadhi) ambapo pia kuna mgogoro na *Vijiji* vya Mayoka, Moya na Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni eneo kubwa la Babati, Monduli, Kondoa, lipo kwenye eneo la hifadhi ya wanyamapor (game controlled area) ambapo zamaani shughuli za kibinadamu zilikuwa zinawezekana. Kwa marekebisho ya Sheria ya 2009, shughuli zote za kibinadamu ilikuwa makazi, kilimo, uvuvi, ufgajji haziruhusiwi kufanyika tena ila sheria ilitaka Waziri ndani ya miezi 12 atangaze maeneo ya game controlled area na nyngine zitolewe kwa wananchi. Tuna mkinzano wa Sheria ya Ardhi, ya Wanyamapor, *WMA*, Madini na nyngine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye game controlled area ya eneo la Babati na wilaya za jirani pia tuna *WMA* ya Burunge. Sheria ya Madini inamruhusu Waziri wa madini kutoa leseni ya kuchimba madini ndani ya hifadhi ambayo ni tatizo.

Tunaomba Wizara itusaidie kutatua mgogoro wa *WMA* Burunge na jamii ya kifugaji wameondolewa kwa nguvu katika maeneo yao na kupewa maeneo ya makazi tu ya ekari tatu kila mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nishauri Serikali itekeleze suala la *Blueprint*. Utalii wetu haukui sababu kubwa ikiwa ni ada, tozo, kodi na ushuru mkubwa ambao unafanya utalii wetu kuwa ghali (*expensive destination*) na pia uongozi wa masuala ya utalii. Binafsi *TATO* wameomba pawe na *one stop centre* kulipia leseni, tozo, ada na ushuru pamoja wakati mmoja kupunguza gharama. Nashauri Serikali iwekeze kupeleka nishati katika geti la Tarangire, Sangaiwe na Mamire pamoja na barabara ya lami ili kupunguza gharama za ukarabati wa kila wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri kila hifadhi ilipe fidia au kifuta machozi na kifuta jasho badala ya Wizara ambayo inachelewesha kutokana na bajeti ndogo na hizo hifadhi zikilipa hiyo fidia watafanya kazi ya kuhakikisha wanyama hawatoki nje ya hifadhi kila wakati. Naomba Wizara iharakishe kulipa deni hilo kuanzia 2011 hadi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara iwekeze zaidi katika *TFS*, Kitengo cha Nyuki na pia Wakala wa Miti Taifa. Tukiwekeza hapo zaidi kwa rasilimali watu, fedha na elimu kwa uma, sekta hii inaweza kuchangia zaidi katika pato la Taifa na pia uchumi wa wananchi. Naomba pia nishauri Serikali ibaki na msimamo wake wa kutoruhusu biashara ya wanyama hai. Nashauri tuwe na marufuku ya kudumu (*total ban*).

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri pawe na uratibu ndani ya Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji kuangalia namna ya kila Wizara kuwekeza kuboresha maeneo muhimu ya miundombinu, nishati, maji, mawasiliano, uwekezaji ili kukuza utalii katika maeneo mbalimbali nchini, utalii wa ndani na nje. Pia Wizara ya Fedha na Wizara nyingine kupunguza kodi, tozo, ada na ushuru kulingana na kukuza biashara ya utalii (*coordinate efforts*).

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii pekee unaweza kufanya Serikali yetu ipate kipato kikubwa bila kugusa rasilimali zetu nyingine kama madini. Bidhaa za misitu kama mbao na magogo hadi tutakapokuwa tayari kama nchi kuvuna wenyewe. Hongereni kwa kazi nzuri na tunawataki kila la kheri.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa fursa ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ambayo ni Hotuba ya Wizara ya Maliasili na Utalii, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Dkt. Kigwangalla, Naibu Waziri, Mheshimiwa Kanyasu Constantine na Watendaji wote kwa kuandaa hotuba hii tunayoijadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza mafanikio ya Wizara kama ilivyobainishwa katika ukurasa namba 10 hadi 18 wa hotuba, ikiwemo kupungua kwa ujangili, uanzishwaji Jeshi Usu, kubadilisha hadhi baadhi ya maeneo ya hifadhi, ongezeko la watalii, mapato na kadhalika. Pamoja na mafanikio yaliyopo bado kuna changamoto ambazo zikipatiwa ufumbuzi zitaleta tija na ufanisi katika utendaji wa Sekta ya Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, iwapo Serikali itatoa fedha iliyoidhinishwa yote na kwa wakati ni dhahiri miradi iliokusudiwa itatekelezwa, kuna wakati na kuiletea pato kubwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Suala la Biashara ya uwindaji wa Kitalii ni tofauti na biashara nyingine, ni ukweli usiopingika uwindaji wa kitalii unahitaji amani, uwepo wa vivutio vyenye sifa ili wawindaji wa kitalii waendelee kuja na kuliongezea Taifa kipato, Wizara iwe na mikakati endelevu ya kuwezesha biashara ya uwindaji wa kitalii ishamiri, pia mazingira ya wanyama stahiki yalindwe vema, kwani kuna baadhi ya wananchi wanavamia maeneo ya mapitio ya wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Idara ya Misitu na Nyuki, Wakala wa Misitu (*TFS*) nina ushauri ufuatao: Uwepo uhifadhi wa misitu wenyе tija, kwani uhifadhi misitu, si utaalami tu bali ni pamoja na matumizi endelevu ya misitu, bila kupoteza sehemu yoyote ya malighafi hususan na kuzingatia utaalami wa teknolojia ya kisasa katika uhifadhi misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado usimamizi wa Misitu haukidhi viwango na misingi inayolenga kuendeleza uchumi wa nchi na uboreshaji mazingira, mfano mashamba ya miti, Tanzania ina maeneo makubwa lakini kasi ya upandaji miti si wa kasi sana. Kasi ya upandaji miti na uvunaji haziwiani hivyo kutishia uvunaji endelevu, hasa miti ya asili. Miti ya asili inazidi kupotea, ni budi Serikali kuititia Wizara ikawe na utaratibu wa kuelimisha watoto, vijana na jamii kwa kuwapa elimu kuhusu umuhimu wa misitu katika maendeleo ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Misitu katika mabonde na miti nayo wananchi waelimishwe umuhimu wake. Katika mazao ya Nyuki, nampongeza Mheshimiwa Mizengo Pinda, Waziri Mkuu Mstaafu na wadau wengine wote wanaoendeleza zao la nyuki, ni zao ambalo linaweza kuleta mapinduzi makubwa kiuchumi, hivyo wananchi wengi wahamasishwe ili wajiiingize katika biashara ya mazao ya nyuki pamoja na uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iendelee kuwaelimisha hasa wananchi wa pembezoni na vijiji faida ya mazao ya nyuki badala ya kuharibu mazingira kwa kuchoma mkaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kusisitiza Wizara ijikite kwa undani katika masuala ya utalii na fukwe, mapango, mila na desturi za makabila, historia ya Viongozi wa kimila na makabila mbalimbali Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2016 tembo walishambulia mashamba ya wananchi ya Mkoa wa Iringa, Wilaya ya Kilolo, Kijiji cha Mgowelo ambapo zoezi la kuhakiki lilifanyika lakini hadi leo hii hawajalipwa na uharibifu ulikuwa mkubwa, hakuna mwananchi aliyeambulia kitu chochote, wananchi hawa walipata shida kubwa sana ya chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ipo wazi shida ya kutowalipa watu hawa ni nini? Kwa kuwa ni haki yao kulipwa, nimwombe Mheshimiwa Waziri wa mwenye dhamana wakati wa kuhitimisha hoja ya Wizara hii atoe majibu juu ya hatma ya wananchi hao.

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto na utatuzi wake; ukurasa wa 68-b-4-3 kutatua migogoro, Mheshimiwa Waziri napenda kujua ni jinsi gani utaweza kutatua migogoro ya Wafugaji na Watumishi wa TANAPA na wenye maeneo tengefu, kwani kumekuwa na sheria kandamizi kwa Wafugaji ambayo hutumika katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ng'ombe wakiingia kwenye hifadhi au *game reserve*, ng'ombe wanataifishwa, kutozwa faini kila ng'ombe Sh.50,000 hadi Sh.100,000, Mchungaji au mwenye Mifugo hutozwa Sh.300,000 au kifungo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, mfugaji aitwaye Wambura huko Serengeti alipigwa faini ya Sh.5,000,000, au kifungo cha miaka mitano (5) na kutaifishwa ng'ombe mia mbili tisini na nne (294).

Mheshimiwa Naibu Spika, Upande wa hifadhi ya Tarangire pia kupigwa faini wafugaji kila wakati na huo umekuwa ni utaratibu wa kila mara, Je, huo sio unyanyasaji kwa wananchi walio karibu na hifadhi hizo? Unyanyasaji huu umesababisha vifo kwa wafugaji kwa ajili ya kufilisiwa je, Mheshimiwa Waziri ataisaidiaje kupunguza adha kwa wafugaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vilivyozunguka Hifadhi kurejeshwa kwa wananchi kama vile Vijiji vya vya Gedamar, Gijedabung na Ayamango vilivyopo Wilaya ya Babati Tarafa ya Galapo, kwani Hifadhi ya Taifa ya Tarangire ina ukubwa wa kilomita za mraba 2,600 kwa Tangazo la Serikali la mwaka 1970, iweje mwaka 2010 kuwe na uwekaji wa *beacon* kwenye vijiji hivyo hapo juu? Ni vema kufanya uchunguzi wa hali ya juu kwa kuondoa huo uonevu kwa wananchi ambao wapo kwenye hivyo vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarangire *National Park*, Ruaha *National Park*, Rukwa Rwafi, Gurumeti *Game Reserve*, Ikorongo *Game Reserve*, Kijereshi *Game Reserve* na Maswa *Game Reserve*, baadhi ya Hifadhi za Taifa na maeneo tengefu yenye kunyanyasa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza kazi nzuri. Naomba nitangulize kauli ya kusema kuwa naunga mkono hoja na pia niseme kuwa kwa kuwa mimi ni mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Wizara hii, mengi ya masuala ambayo ningependa kusema nimechangia katika taarifa yetu ya Kamati. Hata hivyo, naomba Waziri anipe ufanuzi katika maeneo yafuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapor (WMAs); naomba ufanuzi kuhusu suala la kucheleweshwa kwa mgawo wa fedha za WMA (za *photographic* safari na uwindaji) toka Serikali, sambamba ni vifuta jasho na machozi. Uchelewashaji huu unaathiri shughuli za utaratibu za uhifadhi na miradi ya maendeleo ya vijiji vilivytenga maeneo yao yahifadhiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ufanuzi kuhusu utaratibu usiofurahisha jamii wa usimamizi wa shughuli za uwindaji ni kwa nini *Game Scouts* wa WMA ambao wamekidhi vigezo vya usimamizi, ukaguzi wa utiaji saini vibali vya wawindaji. Hawapewi fursa hiyo watendaji na Idara ya Wanyamapor? Kwa nini wao ndio wasimamie uwindaji ndani

ya eneo la WMA wakati *Game Scouts* walioelimishwa na wanaoaminiwa na jamii wapo? Tena hawa *Game Scouts* pia wanatambulika na Mkaguzi wa Idara ya Wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jumuiya ya Wanyamapori Enduimet WMA inalalamikia Wizara ya Maliasili na Utalii kwa sintofahamu ya kushusha daraja eneo lao la uwindaji toka *grade one* kuwa *grade two* bila kuwashirikisha wala kuwafahamisha vigezo walivyotumia kuamua kitalu chao cha uwindaji cha Engasurai kushushwa hadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, athari za kushushwa hadhi kitalu hiki bila ridhaa ya wanajumuiya siyo tu kimewadhalilisha wenyе jumuiya bali pia inawapunguzia mapato kwa zaidi ya 50%. Baya zadi ni kwamba Jumuiya ilishaingia mkataba na mwekezaji wa kitalu hiki kwa makubaliano ya kitalu cha daraja la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, adha wanayopata baadhi ya wananchi kutokana na utaratibu unaotumiwa na vikosi vya kudhibiti ujangili kubaini wawindaji haramu. Katika wilaya yangu ya Longido nina orodha ndefu ya watuhumiwa wa uwindaji haramu ambao wamewekwa mahabusu magereza ya Arusha kwa zaidi miaka miwili sasa bila kesi zao kusikilizwa kila mara ni kutajwa tu na kurejeshwa magereza kwa madai kuwa uchunguzi unaendelea. Miongoni mwao wapo wa vijana wa umri mdogo ambao wamerubuniwa, ni watu wenyе visa nao. Naomba Mheshimiwa Waziri aunde tume maalum ya kupitia tuhuma za mahabusu wote waliokaa muda mrefu magereza kwa tuhuma za uwindaji haramu bila kesi zao kusikilizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni za shoroba na maeneo ya mapito ya wanyamapori; napongeza juhudи za Wizara za kutenga masharoba ya kuendeleza uhifadhi katika nchi yetu. Hata hivyo, napendekeza juhudи hiso zishirikishe jamii zinazoishi katika maeneo hayo kwa karibu. Itapenda zaidi wakifanya matumizi bora ya ardhi na kupewa maeneo hayo wayasimamie wao wenyewe kama WMA au misitu asilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubadili hadhi maeneo ya hifadhi; hii pia ni dhana yenye tija kwa uhifadhi wa mapori yetu isipokuwa nashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria za Wizara zinazokinzana zirekebishwe kwanza mfano TAMISEMI, Maliasili, Ardhi na Madini. Eneo la Ziwa Natron libaki ni ardhi oevu inayohifadhiwa chini ya jumuiya pendekezwa ya *lake Natron WMA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, naunga mkono hoja.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Naibu Spika, hoteli zote zilizokuwa za Serikali zilizopewa, zilizokodishwa au zilizouzwa zifuatiliwe mikataba yake na utekelezaji wa mikataba kwa kuangalia hali za hoteli hizo na utendaji kazi wake kwani hoteli nyingi zinaonekana kuwa na hali mbaya na haziingizii faida Serikali na nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TFS* iendelee kuimarisha ushirikiano wake na jamii kwa kuondoa migogoro iliyopo kati yake ni vijiji kama kule Korogwe kwenye Hifadhi ya Nilo na Msitu wa Chang'andu, Kata ya Kwalukonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TFS* na Wizara kuendelea kuacha kiwanda cha mazao ya misitu cha *TAMISO CHIPBOARD* ambacho bado kina mashine nzuri kimeendelea kuchezewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utetezi wa *TFS* na Wizara kuwa kiwanda hicho kinaangaliwa na Msajili wa Hazina sio sawasawa kwani hata uanzishwaji wa kiwanda hiki ulikuwa maalum kwa ajili ya mazao ya misitu ya shamba la miti la Shume na Gologolo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendelea kukitelekeza kiwanda hiki ni matumizi mabaya ya fedha za nchi na kufifisha nia na dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutohana na kazi nzuri ya kupambana na ujangili kumekuwa na ongezeko kubwa la tembo na wanyama wakali. Je, mamlaka zinazohusika zimejiendaaje kupambana na ongezeko hilo?

MHE. JANETH M. MASABURI: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu watendaji wote na taasisi zilizoko kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, vivutio vyote vya utalii hapa Tanzania viwekwe kwenye *website* kwa kila Ofisi za Balozi zetu zilizoko nje ya nchi. Pili, kivutio kikubwa katika nchi yetu ni amani kwa hiyo ni jambo jema kutangaza nchi yetu kuwa ni nchi ya amani na ni mahali patulivu kwa kupumzika na kufanya utalii kwa utulivu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuititia utalii, Wizara hii ishirikiane na Wizara nyingine kama Wizara ya Madini, Wizara ya Kilimo, Wizara Viwanda na Biashara na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki kwa pamoja tuweze kutumia Balozi zetu kutangaza rasilimali zetu kama utalii, madini, mazao, Kiswahili, amani yetu na mengine ambayo yatainua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lugha mbalimbali zitumike kutangaza utalii kuititia *channel* yetu ya utalii, lugha kama Kichina, Kiarabu, Kijerumanji, Kifaransa, Kihindi, Kirusi na kadhalika ili dunia yote iweze kuona na kuifahamu Tanzania kuwa ina vivutio na ni eneo zuri duniani na ni ya pili duniani kwa vivutio vya asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, makapuni ya utalii ya ndani na nje yashirikiane kuitangaza nchi yetu kiutalii. Tuna upungufu katika sekta nyngi hasa zinazohusika na kutoa huduma mbalimbali ikiwemo eneo la hoteli. Huduma kwa mteja (*customer care*) mafunzo zaidi yatolewe kwa wafanyakazi wetu ili tuendane na ushindani wa kibiashara kwa nchi zilizotuzunguka kama Kenya, Rwanda na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampeni kwa utalii wa ndani. Timu maalum ya Wizara na taasisi zake zifanye ziara maalum nje ya nchi na hasa maeneo ya Ulaya, Asia na Amerika kutangaza na kujifunza mbinu nzuri za kuongeza watalii kuja kwa wingi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha nami kuwepo mahali hapa na kuweza kuchangia hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii ya mwaka 2019/2020. Aidha, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na wataalam wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri, halikadhalika hotuba hii inakwenda kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa kuhakikisha Sekta nzima ya Maliasili na Utalii inaendelea kuimarika na kuliingizia pato Taifa letu kwa maendeleo ya watu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kuendelea kufanya kazi kubwa ya Kiuboreshaji hasa katika Sekta ya Utalii, imeendelea kuimarika na kutoa mchango mkubwa katika ukuaji wa pato la Taifa na kuongeza ajira. Mathalan, idadi ya watalii kuongezeka mara dufu na kupelekea watalii walioingia nchini mwaka 2018 kuongezeka na kufikia watalii milioni 1.49 ikilinganishwa na watalii milioni 1.33 walioingia nchini mwaka 2017. Aidha, hapo hapo pia mapato yatokanayo na utalii yameongezeka na kufikia Dola za Marekani bilioni 2.43 mwaka 2018 ikilinganishwa na Dola za Marekani bilioni 2.19 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 7.13, ni mwanzo mzuri wa kimkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuendelea na jitihada hizi ili takwimu hizi ziendelee kukua, halikadhalika Serikali imetuambia katika kutangaza vivutio vya utalii, mwaka 2018/2019 Serikali imeanzisha Chaneli ya Utalii (*Tanzania Safari Channel*) ili kuvutia Watanzania na wageni

kutoka Mataifa mbalimbali kutembelea vivutio vyetu. Hatua hii itasaidia sana kuendelea kukuza hali ya kiuchumi kuitia Sekta hii ya Utalii. Kuanzishwa kwa chaneli hii pia, Serikali imetueleza kuwa inaendelea kuimarisha chaneli hiyo kwa kuipatia wataalam, vifaa na vitendea kazi stahiki. Chaneli hii itaendeleza taswira na sifa nzuri ya Tanzania kimataifa sambamba na kuongeza thamani katika mnyororo mzima wa biashara ya utalii nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo pongezi zangu zinakwenda kwa Serikali kuwa na mpango katika mwaka 2019/2020, kuendelea kuimarisha Sekta ya Utalii kwa kuihamasisha na kuiwezesha sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika kuendeleza sekta hiyo. Aidha, sanjari na kutangaza utalii, Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya usafirishaji ikiwemo usafiri wa anga ili kuvutia watalii wengi zaldi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuchukua hatua mbalimbali za kimkakati katika kuendelea kupambana na uharibifu wa maliasili kama misitu na kadhalika. Hatua hii imesaidia sana pia hata katika utunzaji wa mazingira yetu na kuepukana na ukame ambao athari zake ni kubwa, kama nchi ikikumbwa na tatizo hilo. Napenda kuishauri Serikali kuendelea na jitihada hizo kimkakati, na kuendelea kupambana na wahalifu wote wanaojaribu kuharibu mazingira yetu kwa kukata miti hovyo, hata hivyo sasa ni wakati wa kutambulisha utalii wa misitu kwani tunayo misitu mingi yenye vivutio kadhaa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja

MHE. RISALA S. KABONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia kuhusiana na Wakala wa Misitu Tanzania (*TFS*). *TFS* imepewa dhamana ya kusimamia maeneo ya misitu 461 nchini. Maeneo haya yanahifadhiwa kwa malengo makuu matatu:-

(1) Ikolojia; hakuna anayefahamu umuhimu wa maji nchini, kwa binadamu, wanyama na mimea. Mfano, Jiji la Tanga wanategemea maji yake kutoka chanzo cha Msitu wa *Amani Nature Reserve*, Mkao wa Kilimanjaro wanategemea maji kutoka chanzo cha Msitu wa Chome na Jiji la Dar es Salaam wanategemea maji kutoka Mto Ruvu – Msitu wa Uluguru ukiwa ndiyo chanzo chake.

(2) Lengo la pili ni kuhifadhi viumbe hai. Misitu hii inahifadhi viumbe adimu duniani. Mfano, vyura wa Kihansi na vinyonga wa pembe tatu.

(3) Lengo lingine ni kwa ajili ya utalii. Mfano Msitu wa Asili wa Amani, Chome, Maporomoko ya Kalambo na Msitu wa Rondo. Kwa siku za karibuni misitu hii imekuwa ikivutia watalii kutoka nchi za Asia kwa ajili ya utalii wa *forest bathing* kuondoa stress.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utalii wa Kupiga Picha. Wasanii wa kizazi kipyaa wameonekana kuvutiwa sana na misitu yetu na wanakwenda kurekodi filamu katika misitu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utalii wa Kuangalia Ndege wa Aina Mbalimbali Katika Msitu wa Rondo mkoani Lindi. Ndege hawa wanatoka mabara mbalimbali ya Ulaya na kuweka makazi yao katika Msitu wa Rondo. Msitu huu unashika nafasi ya 43 duniani kwa kuwa na ndege wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mazuri haya lakini misitu hii imekuwa na changamoto mbalimbali. Changamoto ya miundombinu ya barabara kabla na baada ya mvua. Mfano, Maporomoko ya Kalambo, barabara ya lami Sumbawanga kuelekea Makao Makuu ya Wilaya ya Kalambo kuelekea Bandari ya Kasanga mpaka wa Kongo na Tanzania kipande cha kilometra nane kuingia kwenye Maporomoko ya Kalambo, barabara ni mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri Serikali kuitia Wizara ya Maliasili na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuitia *TARURA* kuiangalia barabara hii ili

kusaidia watalii wanaotembelea Maporomoko ya Kalambo pamoja na kuvutia wawekezaji wanaowekeza katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze *TFS*, Kamishna Prof. Silayo kwa kujenga ngazi zenyne Urefu wa mita 270 kwa ajili ya kutembea kwenye maporomoko hayo na lengo ni kukamilisha ngazi zenyne urefu wa mita 570 kwa mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imetembelea *Amani N. Reserve* – hali ya miundombinu ni mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu za idadi ya watalii wa misitu 2015/2016 ni 2,200, mwaka 2016/2017 walikuwa 3,000 na mwaka 2017/2018 walikuwa 3,500. Kwa takwimu hizi kama wangewekeza kwenye miundombinu tungepata watalii wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado mapato yanayotokana na misitu ni kidogo sana. Mwa 2015/2016 ni 245,000,000, mwaka 2016/2017 ni 310,000,000 na mwaka 2017/2018 ni 370,000,000. Pamoja na idadi kubwa ya maeneo ya misitu 461, ni maeneo 13 tu ndiyo yanayojiendesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Mapato Ghafi kwa Serikali iangaliwe upya ili kusaidia hizi taasisi kujiendesha; asilimia 30 *corporate tax*, asilimia 18 *VAT*, asilimia 15 gawio la Serikali na asilimia 3 *SDL*; jumla ni asilimia 66. Mashirika haya hayawezi kumudu kujiendesha, tuwekeze kwenye miundombinu ili kuongeza wawekezaji na idadi ya watalii na mapato yataongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango wangu kwenye Wizara hii nichukue fursa hii kuwapongeza sana Wizara ya Maliasili na taasisi zake zilizochangia gawio kubwa Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto nilizozionesha kwenye mchango wangu Wizara hii imechangia kwa mwaka mmoja *in order of priority, Tanzania*

Telecommunication Regulatory Authority, Tanzania National Park, Ngorongoro Area Conservation Authority, Tanzania Forestry Services. Taasisi tatu kati ya hizi ni Wizara ya Maliasili na Utalii, hii inaonesha umuhimu wa maliasili kwenye uchumi wa nchi, ni lazima tulinde maliasili zetu. Naomba kuwasilisha.

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri Serikali kutoa elimu kwa vyombo vya habari na meseji kwenye simu kwa kuwa wananchi wengi wana simu ilikuwaelimisha faida za kupanda miti kwa matumizi ya kuni na mkaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitalu vile ambavyo vingi vilikuwa kwenye halmashauri zetu vinakufa kwa kukosa fedha za kuviedhesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri Serikali kutafuta njia mbadala wa mkaa kwani ukataji wa miti hautasimama mpaka njia mbadala; mfano gesi kuwa bei ya chini ndipo tutaweza kuokoa misitu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kushauri Serikali kuboresha barabara zinazoingia hifadhini kuliko ilivyo sasa, barabara ni mbovu inatia aibu watalii wanapokuja kudembelea mbuga zetu mfano njia inayoingia mbugani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotel zetu nyingi zilizoko kwenye mbuga zetu haziko katika hali nzuri pia huduma zake si nzuri, Serikali ifuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri Serikali kufuatilia au kuhakikisha inapunguza utitiri wa tozo uliopo tangu mtalii anapoingia nchini na kuelekea kwenye mbuga zetu ili kuwezesha watalii wetu kuvutiwa kuja nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri vyuo vyetu vya utalii vipitiwe, vingi havina sifa hivyo kutoa wahudumu ambaao hawakidhi vigezo vya kimataifa, wengi hawawezi hata

kuwasiliana kwa kushindwa lugha ya kiingereza hivyo kushindwa kuhudumia kulingana na mahitaji ya wageni.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia Wizara hii nyeti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kupotea kwa ndugu zetu kumi katika Hifadhi ya Mikumi. Wananchi wa Mikumi hususan wananchi wa Kata ya Ruhembe Kata ya Kidodi na Kata ya Ruaha bado wana masikitiko makubwa sana ya kupotelewa na ndugu zao wapatao kumi tangu siku ya tarehe 02, Aprili, mwaka huu wa 2019; mpaka leo bado hawajapatikana wala hakuna taarifa wala dalili yoyote ya kuwaona tena ndugu zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii imekuwa ni tabia ya muda mrefu sana ya ndugu zetu kupotea kwenye Hifadhi ya Mikumi. Kwa taarifa ambazo si rasmi zinasema watu hao huwa wanauliwa na askari wa wanyamapori, hasa wakiwakamata wananchi wanaookota kuni au shughuli yoyote ya kijamii pembezoni au ndani ya hifadhi hii. Tunajiuliza askari hawa wanatumia sheria gani kuwa watu wetu hata kama wamewakamata kwa makosa yoyote? Je, wana haki ya kuwaua binadamu wenza bila kuchukuliwa hatua yoyote?

Mheshimiwa Naibu Spika, Tembo Waharibifu wa Mashamba. Kumekuwa na ongezeko kubwa sana la tembo ambaao wanatoka ndani ya mipaka ya hifadhi na kwenda kuharibu mashamba ya wakulima wetu na pia kuwajeruhi wananchi wetu. Hivi karibuni kumekuwa na tembo wengi sana wanaoharibu mashamba ya wakulima kwenye maeneo ya Kata ya Tindiga, Kata ya Kilangali, Kijiji cha Doma (Mvomero) na kuharibu sana mazao ya wananchi na kusababisha hasara kubwa sana kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejitahidi kutoa taarifa kwa Afisa Maliasili wa Wilaya ya Kilosa lakini wilaya nzima kuna askari mmoja tu, tunaomba sana Serikali iwasaidie sana wananchi wa maeneo haya hasa Kata ya Tindiga na Kilangali ambaao wana kila dalili ya kukumbwa na baa la njaa kama

hawatapata msaada wa mapema ili kuzuia hawa tembo wasiendelee kuharibu mashamba yao ili baadaye waweze kuvuna kile walichopanda na kuwaepusha na baa la njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifuta Jasho kwa Wananchi wa Jimbo la Mikumi. Wananchi wa Jimbo la Mikumi ambao mashamba yao yalivamiwa na tembo bado wamekuwa hawalipwi kifuta jasho chao.

Namuomba Mheshimiwa Waziri akija kuhitimisha atuambie katika Jimbo la Mikumi na Wilaya ya Kilosa kwa ujumla, je, ni wananchi wangapi wamelipwa kifutajasho kwa mwaka huu na wangapi hawajalipwa na lini watalipwa? Pia ninataka kupata majina ya wahanga wote walilipwa na ambao bado hawajalipwa kifuta jasho ili tuweze kufuatilia zaidi haki hii ya wanachi wetu kwa Wilaya ya Kilosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Migogoro ya Mipaka Kati ya Vijiji Vinavyopakana na Hifadhi ya Mikumi. Bado kuna migogoro mingi sana katika Jimbo la Mikumi kati ya vijiji vya Mikumi vinavyopakana na hifadhi yenyewe. Namuomba sana Mheshimiwa Waziri afanye ziara ya kikazi Jimboni Mikumi ili aweze kutusaidia kuhusu changamoto hii ya muda mrefu kati ya wananchi na Hifadhi ya Mikumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana muda unavyozidi kwenda wananchi wanaona kama wanaonewa na wanaona kama kuwa na neema ya kuwa na hifadhi kwao imekuwa laana, maana badala ya kujivunia kuwa na hifadhi sasa wamekuwa wakiuliwa, wakiteswa na kunyang'anywa maeneo yao ya kilimo na shughuli mbalimbali za kujiletea maendeleo, kitu ambacho wanaona kama wanaonewa, kunyanyaswa na hawatendewi haki ilhali wao walistahili kuwa ni wanufaika wa kwanza na muhimu wa Hifadhi hii ya Mikumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali iliangalie hili la mahusiano ya wananchi na hifadhi kwa jicho pevu ili kuwafanya wananchi wajivunie kuwa na neema ya kuwa na hifadhi, wailinde Hifadhi yetu ya Mikumi na wanyama wake na pia waweze kushirikiana na watu wa

hifadhi kuwatambua na kuwataja majangili na watu wenye nia ovu na mbaya kwa Hifadhi yetu ya Mikumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo yote yanawezekana tu kama tutakuwa na ujirani mwema kati ya wananchi na askari wanyamapori ili kuweza kujenga jamii inayopendana, kuheshimiana na kushirkiana ili kuilinda Hifadhi yetu ya Mikumi na kuifanya Mikumi sehemu salama ya kuishi na kuchangia pato zaidi la utalii katika taifa letu. Ahsante.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali yetu ya Awamu ya Tano kuanzia kwa Mheshimiwa Dkt. John Joseph Magufuli, Rais wetu, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Naibu Waziri na watendaji wetu wote wa Wizara na mashirika yote ya umma na wadau wote. Shukrani hizi ni kwa ajili ya utendaji wake wenye dira kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nitoe mchango wangu wa ushauri kwa Serikali yetu.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ione umuhimu wa kutupatia mtumishi (afisa wanyamapori) kwa Halmashauri ya Mji wa Mbulu. Mnamo mwaka 2017 nilimuumba Mheshimiwa Waziri, Prof. Jumanne Maghembe kuhusu hali tete ya wanyama wakali waliopoteza maisha ya wananchi nane ndani ya miezi mitatu mwaka 2015. Nami niliandika barua Wizarani kuomba mtumishi walau mmoja, hata hivyo Halmashauri ya Mji wa Mbulu inapakana na Hifadhi ya Marang', Manyara na Msitu wa Hifadhi ya NOWU, eneo lote hili lina wanyama wakali.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iharakishe fidia kwa wananchi walioharibiwa mazao yao kwa miaka ya 2016, 2017 na 2018 ambayo taarifa ya tathmini yao iko Wizarani (*TANAPA*).

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, sheria itazamwe kuhusu viwango vyta fidia na kifuta machozi kulingana na viwango vyta sasa.

(d) Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali itoe fedha zinazoombwa na Wizara kwa asilimia 100 ili kuwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja asilimia 100, naomba kuwasilisha.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, maliasili na utalii ni muhimu sana katika kukuza Pato la Taifa. Ili kukuza utalii Serikali inabidi kupunguza migogoro kati ya wananchi na Wizara. Kuna maeneo ya wananchi yamechukuliwa na Wizara, kwa mfano eneo la lyegeya Kata ya Luhunga. Eneo hili limechukuliwa na hifadhi ilhali hakuna kitu chochote pale, wananchi hawana eneo la kulima na kufugia wanyama wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali kuwarudishia wananchi maeneo ya Kitasengwa, Kata ya Mkangu, Ihomasa Kilolo, Kata ya Kasanga na lyegeya Kata ya Luhunga. Maeneo hayo ni maeneo ambayo yapo ndani ya vijiji hivyo, wananchi wanakosa maeneo ya kulima ili kupata chakula na maeneo ya kufugia mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mufindi tulikuwa na *center* ambayo ilikuwa kama chuo cha misitu ikiwa chini ya Wizara ya Misitu, sasa chuo hicho hakipo na mafunzo ambayo yalikuwa yakitolewa na Idara ya Misitu hayatolewi katika chuo hicho. Naomba Serikali kufufua Chuo cha Misitu Mufindi ambapo kuna shamba kubwa sana la misitu katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naiomba Serikali kuendeleza kutoa misaada kwa vijiji ambavyo vinazunguka Msitu wa *Sao Hill*. Vijiji hivyo ni; Kata za Nyololo, Igowole, Mninga, Mtwango, Mninga, Luhunga na Mkungu. Kata saba, vijiji 42 ambavyo viro katika Wizara ya Maliasili na walitoa ardhi kwa Wizara hii ili kupata miti ya mbao, sasa wananchi wakosa misaada ya kijamii kama ukosefu wa maji, vituo vyaa afya kwa Kata ya Mninga na Kata ya Mtwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Wizara kuendelea kusaidia shughuli za kijamii. Napendekeza kuwajengea majengo ya kituo cha afya au zahanati na si kutoa fedha. Pia, kuwakarabatia miundombinu ya maji pamoja na barabara ili wananchi waweze kukuza uchumi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Naibu Spika, kuwekeza katika Utalii katika Jiji la Dar es Salam. Jiji hili bado halijatumika vizuri katika sekta hii, hasa utalii wa mji na maeneo ya kipekee. Mfano nyumba ya makazi ya zamani ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, jengo la Salamander, fukwe za bahari nakadhalika. Hii ni muhimu hasa kwa wageni wajapo Jiji la Dar es Salaam kutokea nchi za nje; mfano Jiji la Berlin Ujerumani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutengeneza ramani ndogo na mahsusini kwa maeneo ya kutembelea watalii, kwa mfano ramani mahususi ya Jiji la Dar es Salaam, kuonesha maeno na vivutio vya utalii. Kuongeza na kuboresha vivutio vya utalii Jijini Dar es Salaam, mfano Mto Msimbazi ukitengenezwa vizuri kuruhusu maji kupita wakati wote kwa kuboresha kingo na kuondoa takataka itawezesha matumizi ya boti na watalii watawenza kuzunguka kupita eneo hilo tutapata fedha lakini na mazingira yataboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yote yanayopita kwenye maeneo ya hifadhi yaye na matuta kwa ajili ya kuwakinga wanyama pori dhidi ya kugongwa na gari, kama inavyoendelea kwa sasa katika barabara ya Morogoro-Mikumi na Kitengule-Karagwe. Sheria na kanuni kali kwa watakaogonga wanyama katika maeneo ya hifadhi ya wanyama. Kuendelea kutangaza vivutio vya Utalii katika vyombo mbalimbali vya kimataifa kama CNN, BBC na hata kudhamini matukio muhimu duniani kama Olympic hata kwa kiwango kidogo kama Rwanda na PL League ya Uingereza.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Misitu. Kwa dhati ya moyo wangu nawapongeza sana mmejtitahidi sana kuiinua sekta na kuleta utulivu katika sekta na hasa suala zima la upatikanaji wa malighafi katika Shamba la *Sao Hill*. TFS na uongozi wa Shamba la *Sao Hill* wamekuwa na ushirikiano mzuri na Halmashauri ya Mji wa Mafinga hasa katika *Corporate Social Responsibility* na suala la ushirikishwaji wa wadau. Naomba suala hili la kushirikiana wadau na sisi viongozi wa kuchaguliwa liwe *sustainable*, na ni vizuri kila mara kabla ya mgao kuanza vikao viwepo ili wadau na sisi viongozi wao tuwe na uelewa mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pamoja na hayo nina hoja kadhaa; Kuhusu Kuruhusu Mazao ya Misitu Kusafirishwa Masaa 24. Hili suala tumeshalileta na wakati wa kujibu swali langu la msingi na nyongeza tarehe 04 Aprili, 2019 Serikali Waziri na Naibu Waziri wallieleza Bunge kwamba jambo hilo liko katika hatua ya mwisho, nilitarajia suala hilo liwemo kwenye hotuba yako. Ombi langu ni kuwa tusikie kuhusu jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Mikataba kwa Wavunaji. Pamoja na mchango wangu wa maelezo ya mdomo bado ninawasilisha suala hili na pia natahadharisha badhi ya viongozi wa vyama vya wavunaji wanatumia fursa vibaya kwa kuendelea kujilimbikizia vibali. Yapo malalamiko mengi, ni muhimu kadiri tunavyoingia kwenye uwazi hali na ujanja ujanja huu umalizwe ili sekta iendelee kuwa na utulivu. Hata mtakapofikia hatua ya kuwapa wavunaji mikataba iwe ni wale ambao ni *genuine* na wavipate kwa uhakika na uwazi. Suala hili litafanikisha na kuongeza mapato kwa kuwa itawapa uhakika wa kukopa na kuajiri ipasavyo wafanyakazi ambao watachangia kupitia *PAYE, SDL* nakadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Single Entry. Katika zama hizi za *eGovernment – TEHAMA* ni muhimu sasa kuliangaia suala hili kwa umakini ili kuziwezesha jamii zinazozunguka mbuga zetu kunufaika na utalii. Vilevile pia kuwapa uhakika wa kipato wananchi ambao ni sehemu ya ulinzi dhidi ya ujangiri. Mimi ni mdau wa utalii na familia inaendesha *VAMOs Hotel* Mikumi na Mafinga, pale Mikumi,

Tungamalenga na maeneo ya aina hiyo uchumi umelala kwa sababu watalii wanapita juu kwa juu na hivyo kuondoa fursa ya kipato cha wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Chuo cha Misitu – Olmotonyi Kuwa na Campus ndogo Mafinga. Naomba kuwasilisha tena ombi hili ambalo mkirejea michango yangu ya nyuma, nilishawasilisha; naomba mlitafakari.

MHE. SILAFU J. MAIFI: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi nzuri yenye tija kwa taifa letu. Mheshimiwa Waziri ninakuombea Mungu aendelee kukupa afya, nguvu na wepesi ndani ya utekelezaji wa majukumu yako kwani chini ya uongozi wako Wizara imetulia na unawajibika kwa maslahi ya kuachia urithi watoto wetu na kusababisha kuongeza gawio kwa Pato la Taifa. Tumeweza kubainisha maeneo kadhaa ya vivutio hapa nchini kwa nia ya kupanuwa wigo wa utalii. Tatizo ni kuhakikisha tunaweka mazingira madhubuti ya kuweka miundombinu yote kwa kuanzia kabla ya kutangaza ili wakiingia watalii wasiwe na kigugumizi tena cha kurudi au hata kushawishi wengi kutokana na kukuta ubovu wa miundombinu. Mfano Rukwa kuna Kalambo *falls*, ni kivutio kikubwa ndani ya Afrika Mashariki na Kati lakini hakuna barabara na hoteli, vyoo na maeneo ya kupumzika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi wa kilimo Rukwa ni Oktoba – Novemba mvua zinachanganya na kwa wananchi wetu kilimo ndio mradi mkuu kwa kuzalisha chakula na mazao ya ziada kwa biashara. Wanapojoitokeza wanyama waharibifu kunakuwa na hasara kubwa kwa wananchi wetu na maafisa kuwa na uvivu wa kuyatembelea mashamba yaliyoathirika kwa wakati na kwa eneo zima, wamekuwa wanawahadaa wakulima na hatimaye kuwa na chuki na Serikali yao. Mfano kijiji cha Kisumba – Katanga Kisumba, Wilaya ya Kakumbo – Rukwa. Wakulima wa alizeti walioingiliwa na wanyama ni 140 lakini waliolipwa ni wakulima 60, wengine hadi leo hawajalipwa. Tunaomba Wizara na kitengo husika kufuatilia malalamiko ya wakulima na kuwa shughulikia malipo ya fidia

zao ili zitoke; ni kero kubwa sana huko vijijini, maafisa waachane na rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu wote tunakubaliana kuwa asali kwa sasa ina soko ndani na nje kwa matumizi ya kakwaida kwa afya zetu. Maadamu misitu tunayo nashauri wale mabwana nyuki tulionao wawe na kazi ya kutoa elimu, uelewa na kushauri makundi mbalimbali na kuunda makundi ya ujasiriamali kwa vijana na akina mama ili kuweza kuifanya shughuli hiyo. Kwani ni mradi ambao unajizalisha wenyewe na maafisa wanafahamu maeneo yenye tija hiyo. Mikoa, wilaya, kata na vijiji ambavyo vina mwelekeo huo kwa uzalishaji wa asali kuwa na viwanda nya kuchuja na kufungasha kuingiza sokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ziwa Rukwa kuna mambo mengi sana lakini kutokana na uharibifu wa mazingira na shughuli za kibinadamu na mito kuporomosha maji kwa wingi na udongo moja kwa moja kwenye Ziwa sasa kina cha maji katika Ziwa Rukwa kinapungua na mamba kutawanyika na kuathiri wananchi wetu. Ushauri, mamba waweze kuvunwa, washirikiane na Wizara ya Maji, Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Tuweze kuvuna maji kwa umwagiliaji, mabwawa nakadhalika. Tuliokoe Ziwa na usalama wa wananchi wetu upatikane kwao dhidi ya mamba. Tunaomba Hazina kuitoa pesa iliyopendekezwa ya maendeleo ya Bilioni 48.889 yenye ongezeko la asilimia 66, tunahitaji matokeo chanya yajioneshe kwenye gawio la Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. GIMBI D. MASABA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mchango wangu niuelekeze kwenye Sheria ya Fidia kwa Wananchi kipindi anapopata madhara ya kujeruhiwa na wanyama hususani mnyama aina ya tembo. Kwamba mwananchi akijeruhiwa na tembo analipwa fidia shilingi laki tano mpaka milioni na fidia hizo zinatolewa kwa wakati, jambo ambalo linasababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi hawa. Hali kadhalika fidia ya mazao kwa wananchi kipindi mazao yao yanapoharibiwa wanarudishiwa

fidia kidogo, ekari moja shilingi laki moja ilhali ekari moja ya kulima inakadirwa kuwa laki moja, jambo ambalo si sawa, tunawapunja sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ninaomba hii sheria ya fidia ibadilishwe kwani si rafiki tena kwa mazingira ya sasa kwani gharama za kilimo zinaongezeka kila siku na pia binadamu wanaongezeka lakini pia kutokana na kuwa na changamoto ya uharibifu wa tembo kuwa umekithiri, ni vizuri Serikali ikalitazama suala hili kwa undani zaidi ikiwa ni pamoja na kuchukua tahadhali zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, inasadikiwa miti ya pareto ni adui wa tembo , sasa kwa nini Serikali isianzishe kampeni ya upandaji wa miti ya pareto kwenye maeneo ya pembezoni mwa hifadhi ikiwemo na upandaji wa pilipili kwani pia pilipili ni adui wa tembo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha, ahsante.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Naibu Spika, hongera sana kwa kazi kubwa mnayofanya, tunaona mabadiliko makubwa katika kusimamia maliasili za nchi yetu, kazi mnaifanya, hongereni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi, wananchi wa Kata za Nsenda, Uyumbu, Ugaila na Ukondamoyo zilizo Urambo zina malalamiko mengi kuhusu kupunguzwa kwa maeneo yao ambayo kabla ya mpaka mpya maeneo yalikuwa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafadhari sana Serikali itatue migogoro ya mipaka na ikiwezekana warudi kwenye uhalali wa kuishi kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri, matangazo vivutio vyetu yaongezwe hasa nje ya nchi.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Naibu Spika, sababu kuu zinazosababisha uharibifu katika misitu/ uvunaji wa kupitiliza na usio endelevuni;

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji usio endelevu wa mkaa; Shughuli za kilimo; Biashara haramu ya mbao (*illegal timber trading*) na mkanganyiko katika sheria zinazosababisha *degradation* ya misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Serikali ikajipanga na kuja na mikakati mahususi na kuja na *time plan* itakayotumika kuboresha na kurekebisha changamoto hizi ili kuleta tija katika nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maridhiano/Mikataba ya Kimataifa. Tanzania imeingia mikataba ya kimataifa kama, *UN-CCD, Bonn Challenge, African Forest Landscape restoration*, na *Zanzibar Declaration* kwa lengo mahususi la kuboresha soko la mazao ya misitu nje na ndani ya nchi, na kuhakilisha hali ya misitu nchini inaboreshwani. Ni nini *status* katika kutekeleza matakwa ya mikataba hii hapa nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, *TFS Kuwa Regulatory Authority* Kutoka Kuwa *Agency*. Kutekeleza hili kwa wakati itasaidia *TFS* na hivyo kujenga ufanisi katika kusimamia misitu yote nchini bila kuleta changamoto za mgongano wa kimamlaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Soko la Mbao Nje na Ndani ya Nchi. Tuna *potential/kubwa* nchini katika sekta hii ila bado tupo nyuma sana kwani tunaendeleza biashara hii *traditionally*. Viwanda vingi nchini havi *maximize recoveryya* mbao na pia tupo nyuma katika *grading* ya mbao na kukosa fursa ya kujipatia fedha za kigeni. Kuna umuhimu wa kuviendoleza/kuvifufua viwanda vya mbao; kwa mfano viwanda vya *Fiber Board-Arusha, Tembo Clipboard-Tanga*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Soko la Mbao. Serikali ijkite katika kuongeza aina za mbao kutoka *traditional types* za mbao mfano, Mvule, Mkongo na Mninga na badala

yake ku-diversity resources nyinginezo za aina za miti/miti mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja kwa Serikali kujitathmini katika suala la soko la mbao nje ya nchi kwani tunapoteza kama nchi mabilioni ya fedha za kigeni kutoka *illegal traded timber* Soko kuu la magendo limekithiri kwa malighafi nchi za Asia na hususan China. Ni nini *status* ya nchi baada ya kusaini *The Zanzibar Declaration on Illegal Trade in Timber and Forest Products?*

Mheshimiwa Naibu Spika, *what is the status of community based forestry management and the commitment of the Government to uphold what it sets out in the forest policy of 1998? We are told there is draft revised policy, what is the current status and how rights of those depending on community forestry are being upheld?*

MHE. ZAINAB M. AMIRI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri na Naibu wake kwa kazi kubwa wanayoifanya ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushauri; Serikali itenye fedha za kutosha, pia ambazo zinapitishwa na Bunge zitolewe kwa wakati ili kuweza kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali iainishe vivutio katika kila Wilaya ili kuweza kujua vivutio mbalimbali vilivyopo kisha kuweza kuzitangaza kama vivutio na sehemu ya utalii. Kwa mfano kuna chemchemi iliyopo maeneo ya Kisaki Mkoani Morogoro, maeneo ya Morogoro Vijiji ambapo Chemchemi hiyo ni ya maajabu maana maji yake ni ya moto kwa *centigrade* 100, lakini eneo hilo bado Serikali hajjalibainisha na kufanya moja ya kivutio. Naishauri Serikali illitangaze eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuwekeza katika miundombinu kwenye vivutio vya utalii kwa kujenga barabara, viwanja vya ndege, mahoteli n.k ili kuvutia watalii kufika kwenye vivutio hivyo kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ipitie upya tozo mbalimbali zinazotozwa katika huduma za utalii na kuziondoa zile ambazo zinalifanya nchi yetu Tanzania kuwa ghali zaidi ukilinganisha na washindani wetu wa nchi jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuajiri askari wa kutosha kwa ajili ya kulinda hifadhi zetu maana kumekuwa na uhaba wa watumishi hususani askari wa kulinda hifadhi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali, ili kuondoa migogoro baina ya wananchi waliovamia hifadhi zetu na Serikali, elimu ya kutosha itolewe kwa wananchi hao. Pia Serikali iweke mipaka inayookeleza kuonekana kiurahisi ili wananchi wasivamie hifadhi za taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali malipo yanayolipwa (kifuta jasho) kwa wananchi walioharibiwa mazao yao, waliojeruhiwa na hata kuuawa na wanyamapori. Kifuta jasho hicho hakiridhishi hivyo Serikali angalau ione haja ya kuongeza ili angalau mwananchi aweze kuona haki imetendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba Mwenyezi Mungu awape afya njema na umri mrefu Mheshimiwa Waziri na Naibu wako ili kuweza kutekeleza majukumu yenu ya kila siku.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Naibu Spika, matukio ya wanyama waharibifu hasa tembo na nyati waliharibu mazao ya wananchi katika Vijiji vya Rhotia, Kilimatembo, Ayalabe, Kitete, Kamba ya Nyoka na Oldeani Wilayani Karatu yamekuwa ya kujirudia rudia na mwaka huu yamekithiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tembo wengi wanashinda mashambani na kula mahindi ambayo bahati mbaya mwaka huu yako kidogo sana; wanyama hao wanatoka Hifadhi ya Ngorongoro. Niishauri Serikali iwaelekeze mamlaka hiyo kuongeza doria ili kuwadhibiti wanyama hao.

Tembo hawasikii lolote, wananchi wanahangaika sana na mazao yao yanaharibiwa sana. Katika ukanda huo wa msitu kuna kambi tatu tu. Kambi hizo hazitoshii na pia askari wawe na mafuta na silaha zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, wako baadhi ya askari wa wanyamaporii ambaao wanaendeleza uonevu na ukatili kwa mifugo inayoingia kwenye hifadhi kwa bahati mbaya. askari hao wamekuwa wakiua au kujeruhi ng'ombe. Hivi majuzi askari wa hifadhi ya Ziwa Manyara waliwaua ng'ombe watatu na kujeruhi wengine watano na pia kumvunja mguu mwananchi kwa kumpiga risasi mguuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ng'ombe hali wanyama wala hashambulii wala kudhuru miti kwanini wapigwe risasi? Askari hao si waadilifu kabisa na wamekuwa wanapokea rushwa ili mtu aingize mifugo. Huo ni unyama dhidi ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku za nyuma *NCAA* na *TANAPA* walikuwa wanasaidia miradi mbalimbali ya maendeleo; tangu mwaka 2016 miradi hiyo imepungua sana. Ili waone kuwa na wao ni sehemu ya hifadhi hizo ni vyema miradi ya maendeleo ya wananchi iweze kutekelezeka, kama vile miradi ya shule, afya, maji na kadhalika.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie katika hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tozo nyingi; kwenye sekta hii ya utalii kuna tozo nyingi mno. Serikali ipunguze kodi hii ili iwe kama kivutio cha kupata watalii wengi ambaao watatuingizia fedha za kigeni za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Migogoro Bainaa ya Serikali na Wananchi. Kwa kuwa kuna migogoro kwa wananchi wanaoishi karibu na hifadhi za wanyama, Serikali ijjitahidi kutatua migogoro hiyo hata kama Wizara imejitahidi kupunguza kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vivutio vya Utalii – Njombe. Ninaomba Serikali ivitambue vivutio vya kiutalii katika Mkoa wa Njombe ili kuliingizia kipato taifa letu. Vivutio hivyo ni Mapango ya asilia yaliyoko katika Halmashauri ya Njombe Mjini eneo la Nyumbanitu. Eneo hilo lina kuku wa ajabu na vivutio vya kale. vilevile Mbuga za Kitulo ambapo kuna maua ya kila aina, jiwe lenye ramani ya Afrika asilia, maporomoko ya Mto Mwihe na Lupali – Njombe. Naomba Serikali ifuatilie mambo hayo na kisha kupeleka watalii.

Mheshimiwa Sika, Bajeti. Kwa kuwa sekta hii ya utalii ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa taifa letu basi Serikali ihakikishe fedha inayoidhinishwa na Bunge itolewe kwa wakati na itolewe yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na ninapenda kupongeza juhudu kubwa za viongozi wote kwa mbinu mbalimbali inazofanya kuongeza ujio wa watalii nchini. Aidha, ninapenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, bado naleta hoja ya kuruhusu vipepeo hai viruhusiwe kwenda nje kibiashara na kitalii hapa nchini. Vipepeo ambaao wanavunwa na kutunzwa na baadhi ya wananchi wangu maeneo ya amani ingewaongezea kipato. Aidha, ni ubunifu wao binafsi; sasa ni ubaya gani wanaofanya wa kupeleka nje ya nchi kwa biashara? Nchi nyiningine wanafanya hiyo biashara. Vipepeo si hao wanyama kama ambaao Serikali imefanya vizuri kuzuia. Nashauri leteni hiyo sheria Bungeni ifanyiwe marekebisho kwenye maeneo kama haya ya vipepeo. Haileti mantiki kulinganisha vipepeo na faru n.k.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru Wizara kwa juhudu kubwa (*TFS*) inazofanya kumaliza tatizo la wananchi wa Derema (1,028) ambaao walihamishwa katika hifadhi. Kwa sasa tunamalizia wachache waliobakia kuwapatia ekari tatu tatu ila bado wanalamikia wapunjo ya fidia ambayo bado

hayajashughulikiwa. Naomba suala hili lishughulikiwe ili kuondoa haya malalamiko. Uhakiki na taarifa nzima ilikwishatumwa hapo Wizarani. Pamoja na Naibu Katibu Mkuu kuja na kufanya kikao na wahusika, bado tatizo hilo halijatatuliwa, naomba lipewe umuhimu tumalize hili tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muheza tuna sehemu nzuri ambayo watalii wameanza kuja kwa wingi sana, sehemu ya Magoroto. Ni muhimu sasa hivi wataalam wa Wizara watembelee eneo hilo washauri namna bora na hatimaye waliingize kitaifa kama ni moja wapo ya vivutio hapa nchini kupata matangazo mengi.

MHE. DKT. HADJI H. MPONDA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Waziri na niwapongeze Mawaziri pamoja na timu yao yote ya Wizara katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara katika kupanua wigo wa mazao ya utalii kwa kutumia Mto wa Kilombero kwa utalii wa kuvua samaki wakubwa aina ya Mjongwa n.k.; yaani *king fish touring* katika Mto Kilombero. Utalii huu ulikuwepo hapo mwanzo lakini hivi sasa umesimama kwa muda mrefu, inahitajika *promotion* kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la utatuzi wa mgogoro wa matumizi ya ardhi kati ya hifadhi/vijiji. Napongeza Serikali katika jitihada zake kwa kukabiliana na migogoro hii; shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Rais kwa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na utoaji wa elimu ya uhifadhi, uhakiki wa mipaka katika Pori Tengefu la Kilombero, nashauri Serikali, katika vijiji 16 ndani ya Wilaya ya Malinyi zoezi hili la uwekaji alama za kudumu/uhakiki wa mipaka irudiwe tena kwa kuwa mashamba mengi ya wanachi wa Malinyi kwa sasa yapo katika ardhi ya Pori Tengefu la Kilombero. Hivyo, kusababisha uendelezaji wa mgogoro wa wananchi wa vijiji hivyo na pori tengefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri tena Serikali, kwamba ingerejea upya zoezi la utambuzi wa mipaka/ uwekaji wa alama za kudumu ili kuyanusuru mashamba ya wananchi kwa maendeleo na ustawi wa wananchi lakini pia uendelezaji wa uhifadhi. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ashatu Kijaji tutamalizia na Mheshimiwa Subira Mgusu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili nami nichangie hoja iliyowekwa mezani na Mhehimiwa Waziri Maliasili na Utalii. Nianze kwa kuunga mkono hoja hii, lakini pia kuwapongeza sana Waheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda ni mchache naomba niseme hili suala kikodi na tozo kama ambavyo nimekuwa nikisisitiza siku zote nashukuru tumelipokea, tumelisikia wamesema, lakini niendelee kuomba tuiswahishe shughuli, tusubiri muda wa shughuli hii ukifika tutaongelea kuhusu tozo na kodi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo ningependa kulitolea maelezo machache ni hili kwamba Serikali ilikataa ofa iliyotolewa na Serikali fulani kwa ajili ya utekelezaji wa mradi mbadala wa mradi wa kuzalisha umeme wa Mto rufiji. Naomba niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na Sheria ya Misaada, Mikopo na Dhamana, ni Wizara ya Fedha pekee inayoshughulikia mikopo, dhamana na msaada kutoka sehemu yoyote ndani ya dunia hii na wanaposimama Mheshimiwa Mbunge kusema kwamba Serikali ilipata *offer* na ikakataa tuwe tunajitathimini, kujitafakari nini tunakisema na lengo letu la kusema jambo hili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapopata taarifa ya aina hiyo sisi kama Wizara rasmi huwa tunapeleka kwenye Kamati

yetu ya Taifa ya Madeni kufanya *analysis* ya huo unaoitwa msaada au *offer*. Tukishamaliza kwenye Kamati ya Madeni, wanamshauri Mheshimiwa wa Fedha. Sasa unapofika kwenye *conclusion*, unasimama kwenye Bunge Tukufu kuwadanganya Watanzania dhamira yako ni ipi? Hilo lazima tulielewe. Sisi kama wenye Wizara yenge mamlaka ya kushughulika na misaada, mikopo na dhamana hatujawahi kupata *formal letter* yoyote kutoka sehemu yoyote ndani ya dunia hii kwa ajili ya utekelezaji wa mradi mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaambie Watanzania weendelee kumpuuza Mheshimiwa Mbunge huyu ambaye amesimama akiwa amepewa dhamana kuja kuwadanganya Watanzania. Dhamira ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ni njema sana. Tunakwenda kwenye Tanzania ya viwanda, tunatekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo, Dira ya Taifa letu 2025, kujenga uchumi wa viwanda utakaoleta mabadiliko kwa wananchi wetu, lazima tuwe na umeme wa bei nafuu, lazima tutekeleze mradi huu na naomba niseme tuko tayari na tumeanza kutenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia amesema Mhehimiwa Mbunge huyu kwamba Serikali haina uwezo, naomba nimwambie tumejipanga, tumejiandaa na tupo tayari kutekeleza mradi huu na utakamilika kwa wakati na Watanzania waweze kufaidi matunda ya Taifa lao. Ni jambo dogo la kawaida la kujiliza amesema vizuri Mheshimiwa Dkt. Mollel. Daktari Mollel alipoulizwa ni wao taifa hilo hilo ambalo walisema miaka hiyo kama ungetekelizwa mradi huo ungekuwa ni chanzo kikubwa cha maendeleo ya Taifa lao. Leo kuna nini Watanzania tunatekeleza wenyewe?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tusikubali kutumika bila kuwa na sababu ya msingi, sisi ni Taifa huru, tumesimama na mradi huu tutautekeleza na naomba niliambie Bunge lako Tukufu tayari tumshapeleka Sh.688,650,898,267 kama fedha ya kuanza utekelezaji wa mradi huu na pesa yake ipo wala hatuhitaji kwenda kukopa au kuomba, ipo kwa ajili ya mradi wa umeme wa Mto Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na narejea kusema naunga mkono hoja hii.

NAIBU SPIKA: Nilikuwa nimekuita Mheshimiwa Subira Mgali kabla hujasimama ili taarifa zetu zikae vizuri ile taarifa ambayo imepelekwa kwenye Kamati ili Mheshimiwa Ruge ulipata fursa ya kuomba utaratibu, tutaweza kuizungumzia wakati huu kwa sababu ukimjibu sasa hivi kuhusu ile taarifa aliyoitoa kwa sababu amesema utafiti atakapodhibitisha kule tutapata hiyo fursa, kwa hiyo karibu Mheshimiwa Subira Mgali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa kuchangia katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Nianze kwa kuunga mkono hoja hii na kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na Naibu wake na viongozi wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayoifanya hususan katika ulinzi wa maliasili zetu na vyanzo mbalimbali nya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kuchangia hoja kwa dakika chache ambazo umenipa, lakini nikirejea hutuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuanzia ukurasa wa 18 ambayo imeelezea muktadha mzima wa Rufiji *hydropower* na nimshukuru Naibu Waziri wa Fedha amesema, sitarejea katika upande lakini nimpongeze sana wake.

Ninachotaka kuwaomba Watanzania na Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa mradi umeanza na tunatarajia mwezi wa Saba kuweka jiwe la msingi na kazi mbalimbli za mazingira wenzeshi, masuala ya *mobilization* tayari, nadhani itakuwa ni kupoteza muda kuanza kuujadili kwa misingi ya kwamba turudi nyuma, haturudi nyuma. Hilo nataka niliseme wazi kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka nirejee kulitaarifu Bunge lako na nilipata kusema, mradi huu mradi huu ulifanyiwa tafiti mbalimbali na kimsingi tafiti zote hakuna tafiti ambayo iliainisha kwamba mradi huu hauna faida yoyote. Kwa sasa tunapotekeleza mradi huu imeshafanyika *environment social impact assessment* imeshafanyika *strategic environment assessment* ambazo wenzetu wa Maliasili wanaweza kulisemea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ninachotaka kusema sisi tumeangalia faida na hasara zake na hususan kwenye kwenye kumpunguzia mtanzania gharama kubwa ya matumizi ya umeme. Tumetathmini vyanzo mbalimbali na kwa kuwa tunatekeleza mpango kabambe wa umeme ambaao umeainisha kila chanzo kinatakiwa kizalishe *megawatt* ngapi ili kufanya ile *energy mix* ya nchi iwe *stable*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nataka nilitaalifu Bunge lako Tukufu kwa kweli kwa namna ambavyo chanzo hiki cha maji kinagharimu shilingi 36, umeme unazalishwa na gesi unagharimu shilingi 147 umeme unazalishwa na mafuta unazalisha Sh.526. Pia ukiangalia gharama za uwekezaji, unapowekeza kwa kutumia imetajwa joto ardhi unatumia Sh. 10,039 kwa *megawatt* moja tofauti na unapowekeza kwa kutumia maji watumia Sh.6,000 kwa *megawatt* moja, kwa hiyo utaona hata gharama za uwekezaji zina nafuu kwenye miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, chanzo cha joto ardhi Serikali ya Awamu ya Tano imewekeza, Wizara ya Fedha imeleta billioni 32 kununua mitambo ya uchongaji wa visima vya majoribio. Kwa hiyo nataka niseme kwa kweli kwa Serikali yetu kwa *energy mix* inayoendelea tuna imani kabisa mradi huu mkubwa wa Rufiji *hydropower* utakaozalisha *megawatt* 2115 ndiyo mkombozi kwenye uchumi wa viwanda, lakini lile lengo la Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ya kupunguza gharama ya umeme kwa watumiaji wa kawaida na viwandani litatimia kwa kuwa itakuwa ndiyo mradi mkubwa wa kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi nchi mbalimbali zilizoweza kujenga mabwabwa makubwa, ikiwemo Ethiopia ikiwemo Unganda, na nchi nyingine zimevezaje na sisi tushindwe kwa ajili tu ya masuala ya mazingira? Kwa hiyo, nikuthibitishie sisi watekelezaji Wizara ya Fedha imetuwezesha, tunaendelea kusimama mradi huu kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge ambao mmepata fursa ya kuchangia kwenye hoja hii.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nilete kwenu matangazo kabla sijasitisha shughuli za Bunge. Kwanza kuna tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote kwamba siku ya Alhamisi tarehe 23 Mei, mlitangaziwa hapa kuhusu kujaza dodoso ambalo linataka taarifa za hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Bunge la Tanzania katika kupambana na unyanyasaji wa kimtandao unaofanywa dhidi ya Wabunge wanawake, dhidi ya Wabunge kwa ujumla, lakini hasa Wabunge wanawake katika kutekeleza majukumu yao mbalimbali. Mnaombwa sana sana, dodoso hizo mjizaze halafu muwakabidhi wahudumu tutakapokutana mchana wa leo.

Waheshimiwa Wabunge, nami nasisitiza naomba tujaze kwa sababu wakijaza watu wachache halafu taarifa itakapotujia tutaanza kusema hapana hii siyo kweli, kumbe waliojaza wale wao wametoa taarifa yao lakini kwa wingi ukipima kwenye haya mambo ya tafiti itaonekana taarifa hiyo ndiyo ipo sahihi ama taarifa hiyo ndiyo haiko sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sisi wenyewe tujaze ili wenzetu wanaofanya utafiti huo waweze kutueleza vizuri kwamba unyanyasaji huu Bunge limechukua hatua zipi, zile tunazozifahamu na kama hakuna tunazozifahamu pia ni nzuri kujua ili sasa Bunge liweze kusonga mbele kwenye kuhakikisha Wabunge wanafanya kazi zao vizuri bila kunyanyaswa Wabunge wanawake na pia Wabunge wanaume.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Kigwangalla alikuwa leo ametualika kwenye futari jioni mara baada ya kuahirisha Bunge lakini zoezi hilo limeahirishwa mpaka tutakapotangaziwa tena kwa sababu siku ya leo baadhi yetu wamealikwa kwenye futari nyingine, sasa akifanya Mheshimiwa Kigwangalla na wale walioalikwa kule na wenyewe walitaka kuja kwenye futari ya Mheshimiwa Kingwangalla.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge futari iliyokuwa iwepo kwenye viwanja vya Bunge jioni ya leo imeahirishwa mpaka mtakapotangaziwa tena.

Tangazo lingine linatoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sport Club* Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, anawatangazia Wabunge wote kwamba siku ya kesho tarehe 25 Mei, 2019, siku ya Jumamosi kutakuwa na mchezo wa kirafiki kwanza ni mpira wa miguu (*Football*) *Bunge Sport Club* itacheza na Dodoma Veteran. Mechi hiyo itachezwa kwenye Uwanja wa Kilimani kuanzia saa kumi jioni Uwanja wa Kilimani, watu wasije wakaelekea Jamhuri kuangalia mpira wa miguu. Mpira wa pete kwa maana ya *netball* kati ya Bunge *Queens* na Dodoma Veteran, mechi hiyo itachezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri kuanzia saa tisa alasiri. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge tunaweza kuanzia Jamhuri saa tisa alasiri, baada ya kumaliza mpira wa pete basi tutaelekeea kilimani kwa ajili ya mpira wa miguu.

Baada ya matangazo hayo Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi kamili jioni leo.

(Saa 7.00 Bunge lilitishwa mpaka saa 10.00 Jioni)

(Saa 10:00 Jioni Bunge Lillrudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Katibu.

NDG. YONA P. KIRUMBI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Maliasili na Utalii

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Majadiliano Waheshimiwa Wabunge yanaendelea, sasa ni saa ya Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Constantine Kanyasu dakika kumi na tano. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii na mimi niweze kuchangia. Kwanza naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili naomba nimshukuru sana Mungu, kwa kunijaalia kufikia nafasi hii, na kwa kweli kwa kupata nafasi ya kushiriki katika Wizara hii, Wizara ya Maliasili na Utalii, lakini kipekee kupata nafasi ya kumsaidia Mheshimiwa Rais Katika juhudzi zake za kuwakomboa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kunipa nafasi, na kufanya kazi hii, naamini sifa ya ziada kuliko watu wengine lakini ilimpendeza niweze kumtumikia katika nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na ili kuyaweka vizuri maneno yangu, naomba wale ambao huwa wanasoma biblia wasoma katika zaburi ya 116 mstari wa 12 na inasema nimtumikie nini Bwana katika mambo yote aliyonijalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana viongozi wote, Makamu wa Rais, na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote ambao nimekuwa nikipata ushirikiano mkubwa. Kipekee naomba nitumie nafasi hii, kumshukuru sana Waziri wangu wa Maliasili na Utalii kwa namna ambavyo ananipa ushirikiano na kwa kweli kwa namna ambavyo

ananipa miongozo mingi katika kufanikisha kazi yake. Ninaishukuru sana ofisi yako na Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla, nimepata ushirikiano mkubwa sana kwenye Kamati na naishukuru sana Kamati kwa namna ambavyo imekuwa ikitusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee niwashukuru pia wapiga kura wangu. Tulizoea siku zote baada ya Bunge nilikuwepo muda wote jimboni lakini sasa hawanioni lakini wameendelea kuwa na imani na mimi. Ninaishukuru pia familia yangu, kwa uvumilivu wote ambao wameupata hasa katika muda huu ambapo muda mwiningi sipati muda wa kufanya kazi na familia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani zote hizo, naomba sasa nitumie nafasi hii kujibu maeneo machache ambayo naweza kupata nafasi kwa dakika hizi kumi na tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, nianze labda na tatizo la udhibiti wa wanyamaporí wakali na waharibifu. Serikali imechukua hatua nyangi za kudhibiti Wanyamaporí wakali na waharibifu wakiwemo tembo, mamba na viboko. Kimsingi pamoja na hatua zote ambazo tulikuwa tunachukua, tulikuwa na tatizo kubwa la kanuni; kwa hiyo tumeanza kuandaa kanuni za shoroba na maeneo ya mtawanyiko ya wanyamaporí kwa lengo la kuhifadhi na kupunguza migongano baina ya wananchi na wanyamaporí.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeendelea kuendesha doria za kawaida za pamoja ili kudhibiti wanyamaporí wakali na waharibifu, kuelimisha wananchi kuhusu matumizi ya mbinu tofauti kama vile kuweka mizinga ya nyuki, kulima pilipili kwenye mipaka ya mashamba, kuweka oil chafu kwenye maeneo ya mashamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kushirikiana na halmashauri kuunda na kuwezesha vikundi vyá kijamii vinavyodhibiti wanyama waharibifu, kufatilia mienendo ya wanyamaporí hususan tembo; na hivi karibuni tulimshuhudia Mheshimiwa Waziri akiwalisha mikanda ya kielektoniki

yaani (*callars*) kwa lengo la kubaini mienendo yao. Pia kuendelea na mipango mikakati ya kitaifa ya namna ya kukabiliana na changamoto za wanyamaporí wakali na waharibifu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakiri kwamba hivi karibu kumekuwepo sana na tatizo kubwa sana wanyamaporí kuzagaa katika maeneo mengi, na hii inatokana kwa kweli na sasa wanyama wamekuwa huru. Mwanzo walikuwa wanawindwa hovyo na kwa sababu hiyo ulikuwa unaweza kufikiri kwamba sasa wanyama wamekwisha Tanzania, lakini baada ya udhibiti mkali, sasa wanyama imekuwa kila unapoamka asubuhi unasikia wanyama wako kila eneo wamezagaa. Kwa hiyo tumeendelea kuweka Mipango Mikakati ya kukabiliana na changamoto hiyo ambayo tunaamini kwamba baada ya mikakati hiyo Wizara yetu itafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika kukabiliana na changamoto ya watu ya kuuwawa na Mamba. Wizara imefanya sensa nchi nzima ambapo mwezi Oktoba mwaka jana mpaka Novemba taarifa ya sensa imeonesha kwamba, mamba wameongezeka katika maeneo yaliyohifadhiwa na mamba wamepungua katika maeneo ambayo hayaku hifadhiwa. Wizara itafanya utaratibu wa kuwavuna hawa mamba na utaratibu huu tayari tunauandaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imefanya sensa ya Viboko katika maeneo ya Mafia na maeneo mengine. Takwimu zinaonesha kwamba katika Kisiwa cha Mafia viboko wako sasa kumi na sita na kuna mabwawa matatu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Changamoto ya wanyama hawa katika kisiwa hiki inaonekana kwamba inapanuka kwa sababu wanashambulia watu na kuvamia mashamba. Wizara itafanya juhudzi za kutoa elimu kwa wananchi lakini pia tutawavuna viboko wakorofí ambao wamekuwa wakishambulia watu na mashamba ili kuwapunguza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yetu inafahamu kwamba ziko changamoto za malipo yanayotokana na shambulio la wanyama waharibifu. Ni kweli kwamba kifuta jasho kimekuwa ni kidogo lakini na kifuta machozi. Wizara inaendelea kufanya mapitio ya Kanuni za kifuta jasho na kifuta machozi na tayari wataalamu wa Wizara wameandaa andiko na mapendelekezo hatua inayofuata ni kupeleka rasimu ya Kanuni ya hizo kwa wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya kanuni hizo yanakwenda sambasamba na mabadiliko ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Namba 5 ya Mwaka 2009. Wizara pia inaendelea kulipa malipo ya kifuta jasho cha machozi kadiri madai yanavyowasilishwa, na kwa mwaka 2018/2019 jumla ya shilingi bilioni moja, milioni mia nne na ishirini sita, laki sita na thelathini na sita na mia tano zimelipwa kwa wananchi 7,320, hawa ni kutoka katika Wilaya 57. Kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019 kiasi cha shilingi milioni arobaini na mbili zimelipwa kwa wananchi 148 kwa wananchi wa Wilaya ya Kilosa. Malipo hayo yamefanyika tarehe 12 Februari.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba madai yako mengi na yanashughulikiwa; na Mheshimiwa Catherine alitaka orodha ya watu waliolipwa Serengeti, namuomba Mheshimiwa Catherine kama hatajari baada ya kikao hiki, tunaweza tukawasiliana tukampatia hiyo orodha kwa sababu ni Waziri Kivuli wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ya kifuta jasho au kifuta machozi yalikuwa yanachelewa kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kuchelewa kwa kuwasilishwa kwa taarifa kutoka kwa waathirika kwa sababu zipo taratibu nyingi ambazo zinatakiwa kupitiwa kabla ya kufikia hatua ya kupata malipo. Wizara kwa kushirikiana na *Giz*, inaboresha mfumo wa kuwasilisha taarifa kwa kuanzisha kanda nne ambazo zitakuwa zinapokea na kufanya tathimini ya athari zinazotokana na shambulio hilo, ambazo tunazipokea Wizarani kwa njia ya elektoniki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zake inaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu taratibu za kuwasilisha madai kwa mujibu wa sheria lakini pia ndani ya wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maeneo machache tu ya Waheshimiwa Wabunge ambayo walisema yalishatolewa maelekezo na Wizara yangu lakini hayajafanyika. Nikianza na Mheshimiwa Dkt. Kikwembe, amezungumza kuhusu suala la watu wetu wa *TANAPA* kugonga mtu na baadaye hawakusimama na hajulikani malipo hayo. Suala hili ni la kisheria linashughulikiwa kisheria na ninaamini pale ambapo mfumo wa kisheria utakapokamilika haki za aliyegongwa zitapatikana kulingana na kheria kwa sababu gari zile ziko insured

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili amezungumzia kuhusu kisima; *TANAPA* tayari wameshatoa maelekezo kwa Mkurugenzi wa Kanda hiyo kukamilisha kisima hicho kama nilivyonitoa maelekezo wakati najibu swali. Kwa hiyo kisima hicho kitakamilika na wananchi watapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Malocha, alizungumzia usumbufu wanaoupata wananchi wa Ziwa Rukwa wanapokwenda kuvua, na akaeleza kwa masikitiko makubwa kwamba wananchi wamekuwa wakinyang'anywa mali zao na mitumbwi yao kubomolewa na afisa wetu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara yangu ilishachukua hatua, Katibu Mkuu wa Wizara alituma ujumbe wa maafisa watatu kwenda kuchunguza malalamiko haya ya kinidhamu, ambayo Mheshimiwa Malocha aliyaleta ofisini, pamoja na Mbunge wa Viti maalum na tayari taratibu za kiofisi zinaendelea. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimuhakikishie Mheshimiwa Malocha, baada ya tu ya Bunge hili nilikuwa nimekuahidi kwamba tutakwenda katika eneo hilo kufanya mukutano na wavuvi na kuwasikiliza, na pale ambapo hatua

italazimika kuchukua pale pale tutachukua kwa mujibu wa sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Getere, amekuwa akilalimikia kuhusu Kituo chake cha afya ambacho kimejengwa na taasisi yetu ya TANAPA, kimekamilika kwa miaka miwili iliyopita lakini hakifanyi kazi. Ni kwamba tayari uongozi wa TANAPA umeshamwelekeza Mkurugenzi wa Kanda hiyo ya Magharibi kukamilisha kituo hicho ili kiweze kufanya kazi haraka, na tayari pesa za Kituo hiki zimekwisha tengwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwepo ahadi ya Mheshimiwa Waziri katika eneo la Kihibu, Waziri alifanya ziara na akaahidi milioni thelathini kwenye jimbo la Mheshimiwa Getere. Tayari aliwaelekeza TANAPA kuhakikisha kwamba pesa hizo zinatolewa na zinatolewa kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwanza kwa pongezi zao ambazo wametupatia katika Wizara, lakini kwa ushirikiano mkubwa ambao wamekuwa wakitupa. Tuwahakikishie kwamba sisi ni watumishi wao; kwa hiyo pale ambapo wanadhani tunahitaji kutoa ushirikiano tuko tayari muda wote masaa yote kufanya kazi hiyo bila kubagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nakushukuru sana, ahsante sana kwa nafasi. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge sasa nimuite mwenye hoja yake, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Dkt. Hamisi Kigwangalla. (*Makofii*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa fursa hii, na nianze kwanza kwa kukushukuru wewe mwenyewe Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wenyeviti wote, na mahsusni Mwenyekiti Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu ambaye, ninyi nyote kwa pamoja mmeshiriki katika

kutuongoza vizuri katika mjadala huu wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Pia kipekee niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kujadili hotuba ya Wizara yetu ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninamshukuru sana Mheshimiwa Kemilembe Julius Lwota, Mbunge ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa kuchambua na kujadili utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020; lakini pia, kwa kutoa maoni kuhusu makadirio na mapato ya matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019. Vilevile ninamshukuru Mheshimiwa Mchungaji Peter Simon Msigwa Mbunge, na Naibu wake Mheshimiwa Catherine Ruge, ambao ni wasemaji kwa upande wa Wizara ya Maliasili na Utalii kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru pia, Waheshimiwa Wabunge wote kwa namna ya kipekee kwa kutoa michango mbalimbali ya kuongea hapa Bungeni lakini pia michango ya maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imepokea na kuchambua michango kutoka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na Waheshimiwa Wabunge. Jumla ya Waheshimiwa Wabunge 68 kwa ujumla wao, wamechangia ambapo 36 wamechangia kwa kuongea hapa Bungeni na 32 wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwahakikisha kuwa maoni na ushauri wote uliotolewa na Wabunge utazingatiwa kwa dhati kabisa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, zimetolewa hoja nyingi mbalimbali na kwa faida ya muda naomba nisizirudie, lakini ninaomba nitoe ufanuzi kwenye maeneo machache, na ninaomba Waheshimiwa Wabunge waniruhusu nifanye hivyo kwa faida ya muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja zote zilizotolewa hapa, hoja ambayo tunaona tuipe uzito sana katika kuitolea ufanuzi kwa sababu inagusa maeneo mengi ya Waheshimiwa Wabunge, lakini pia wananchi kwa ujumla wake ni hoja ya nigogoro ya mipaka baina ya mamlaka za maeneo mbalimbali yaliyohifadhiwa na wananchi wanaozunguka maeneo hayo. Ushauri umetolewa, maombi yametolewa na Waheshimiwa Wabunge kwamba pengine ile Kamati ambayo Mheshimiwa Rais aliyoiumba Januari 15 mwaka 2019, baada ya kukamilisha kazi yake inge-share ripoti ya kazi hiyo na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufanuzi pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu aliutoa hapa juzi, na naona pia jana imejitokeza na leo imejitokeza, naomba tu niwape *comfort* Waheshimiwa Wabunge kwamba mchakato huu kwanza, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu, uliagizwa na Mamlaka ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na hivyo kazi tuliyotumwa mimi pamoja na Mawaziri wenzangu wengine saba ilikamilika na tumeshawasilisha ripoti kwa aliyetutuma, na ndio utaratibu wa kiutendaji. Sasa Mheshimiwa Rais atashauriwa na Baraza lake la Mawaziri na hatua zitakapo anza kuelekezwa kwamba zichukuliwe ni wazi Waheshimiwa Wabunge watapata mrejesho. Hata hivyo niwatoe hofu kwamba tumefanya sample ndogo ya maeneo wamezungumza Waheshimiwa Wabunge wengi, kwa sababu nafahamu wengi wangetamani tufike kila eneo ndipo waone kwamba tunashughulikia migogoro ya maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Naomba niwape *comfort* Waheshimiwa Wabunge kwamba kazi iliyofanyika imefanyika kwa kikamilifu na ni kazi ambayo ilipewa uzito mkubwa sana na Serikali na si kazi ambayo ilianza Januari 15, kuna kazi nyingine zilishafanyika huko nyuma. Kuna Tume mbalimbali zilishaundwa, tumechambua taarifa zote hizo lakini tukaona haitoshi tukaona pia tuchukue maoni kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na tukapata maoni yenu, mapendekezo yenu na maombi sehemu nyingine na yote haya, tumeyafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tukaona haitoshi tukawaita Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Mikoa, wa Wilaya, Wakurugenzi wote wa halmashauri zote hapa nchini wakaja pia wakazungumza na Kamati yetu, nao wakatuelezea migogoro mingine ambayo ipo katika maeneo yao na yote hiyo tumeifanyia kazi na kimsingi kuna migogoro ambayo mahsus i tumeipatia mapendekezo kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kwenye maeneo mengi zaidi, tumeweka tu *principle* ambayo itatumika kufanya maamuzi tunavyoelekea mbele. Kwa hivyo hata kama mgogoro haukuwepo katika migogoro ambayo tumeipitia, na hiyo itakuwa ni bahati mbaya sana, basi itaguswa na hiyo *principle* ambayo tutaitumia katika kufanya utekelezaji; na hii sasa, ni mpaka pale ambapo Mheshimiwa Rais atakubaliana na mapendekezo ambayo tumeyapeleka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini walau linaloleta faraja kubwa kwa Waheshimiwa Wabunge na kwa wananchi ni jambo moja, na hili ni *spirit* ya Mheshimiwa Rais. Azma ya Mheshimiwa Rais ilikuwa ni kupunguza manung'uniko, kero na migogoro kwa upande wa wananchi kuliko hata kwa upande wa hifadhi; japokuwa aliweka angalizo kwamba tuhakikishe tunalinda hifadhi hizi, tuhakikishe pia tunalinda ikolojia hizi ambazo tunazo kwa namna yoyote ile. Kwamba tutatue migogoro lakini tuhakikishe pia uhifadhi unaendelea na shughuli za utalii zinaongezewa tija. Kwa hivyo mambo yote yamezingatiwa katika uchambuzi wetu na mapendekezo yako vizuri. Kwa hivyo *comfort* iliyopo ni kwamba kwenye maeneo yale yenyewe kero, kwa kweli *spirit* na muongozo wa Mheshimiwa Rais ulikuwa ni kwamba wananchi wapate ahueni; na hilo ndilo tulilolizingatia katika mapendekezo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kuwa bado kazi ni mbichi naomba niishie hapo nisije nikajikuta naanza kuelezea baadhi ya migogoro ilhali hatujapewa muongozo na aliyetutuma; lakini walau muwe mna-*comfort* hiyo kwamba migogoro baada ya mapendekezo haya kuitishwa

na Mheshimiwa Rais pengine tutaipunguza kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maelekezo mengine yote ya ushirikishwaji wa wananchi tunayapokea kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na ndivyo ambavyo tumekuwa tukifanya; labda tutaweka msisitizo zaidi kwamba wananchi washirikishwe kwa kiasi kikubwa katika kuitia mipaka na katika zoezi zima la kuweka vizingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna maelezo pia ambayo yalitolewa kwenye ripoti ya Kamati, lakini pia Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, pia Mheshimiwa Sakaya, Mheshimiwa Catherine Magige, Mheshimiwa Yussuph Hussein pia alizungumzia leo na Waheshimiwa wengine wamezungumzia eneo la Ngorongoro. Naomba hapa nielezee tu kwamba, eneo hilli ni katika maeneo ya urithi wa dunia ambao unatambulika na *UNESCO*. Pia ni eneo nyeti kidogo kiuhifadhi ma unyeti wake kwa kiasi kikubwa unajengwa na msingi kwamba ni eneo pekee ambalo matumizi mseto ya ardhii yanaruhusiwa kwamba kuna matumizi ya uhifadhi wa wanyamaporii katika eneo hilo lakini pia shughuli za mwananchi zinaruhusiwa, wananchi wanaishi sambamba na wanyamaporii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na changamoto nyingi ambazo zimejitokeza kutokana na *model* hii na ukweli unazidi kujibainisha pale ambapo tunaona dhahiri kwamba idadi ya watu toka mwaka 1959 inapotangazwa ambapo walikuwepo 8,000 imeongezeka sana leo hii tuna watu takribani 93,000 katika eneo lile lile. Pia idadi ya mifugo imeongezeka, shughuli za utalii pia zimeongezeka kulikuwa kuna *lodge* chini ya sita leo hii tunazo *lodges* zaidi ya 10 katika eneo hilo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo shughuli za utalii zimeongezeka, shughuli za watu zimeongezeka pia wananchi wanaopita katika eneo la Ngorongoro kwenda Serengeti na kwenda Mkoa wa Mara upande wa pili pia wameongezeka. Kwa hivyo kulikuwa kuna haja ya Serikali kwa kweli kukaa

chini kutathmini na hatimaye kuja na mapendekezo kwamba nini kifanyike katika eneo hili nyeti sana la kiuhifadhi la Ngorongoro. pia kwa kuzingatia ukweli kwamba *per square meter* eneo la Ngorongoro ndio hifadhi pekee ambayo inaingiza pesa nyingi zaidi kuliko hifadhi zote Afrika Mashariki na Kati, *per square meter*. Kwa hivyo, ni eneo fulani ambalo kiuchumi ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumefanya kazi hiyo, niliunda Kamati mimi kama Waziri mwaka jana mwezi Machi, Kamati imetuletea ripoti wiki iliopita na ina mapendekezo kadhaa. Mapendekezo tunaona yakikubaliwa na wananchi na wadau wote yatakuwa mazuri yatasaidia ku-*balance* mahitaji ya makundi yote ambayo yanatumia ardhi ya Ngorongoro wakiwemo wananchi pia sisi wahifadhi na shughuli za utalii kwa ujumla wake kwa sababu tunapendekeza na kama Serikali itakubali kwa maana ya kupitia Baraza la Mawaziri, basi sisi tunapendekeza kwamba eneo la Ngorongoro kwa kuwa linazidi kupata athari kubwa ya mazingira ni lazima tuchukue hatua mahususi kama zifuatazo; kwamba katika eneo lile kuna shughuli ambazo zinahusiana na uhifadhi 100%. Eneo kwa mfanola *crater*, kuna *craters* tatu pale *almost*, ya Embakai pamoja na hiyo Ngorongoro *Crater* ni lazima maeneo haya yalindwe. Pia kuna msitu wa Kaskazini ni lazima eneo hili lilindwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunavyoona sisi pengine matumizi katika maeneo haya nyeti na maeneo mengine ambayo yana wanyamapori wengi kama Ndutu pengine yawe *limited* kwa ajili ya wanyamapori.

Vilevile tunaona kwamba mle ndani kuna makazi ya wananchi, wananchi wale hawaruhusiwi kulima, hawaruhusiwi kujenga nyumba za kudumu, kwa hivyo maisha yao yanakuwa magumu sana. Ukitaka kujenga shule alizungumza Mheshimiwa Catherine Magige ni mpaka wapate kibali, wakitaka kujenga zahanati ni mpaka wapate kibali, kwa hiyo yanakuwa wanapata adha kubwa sana kuleta maendeleo katika maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi pia tunaona hii si sawa, jamii ya wananchi wa Ngorongoro ina haki kama jamii ya wananchi wa Iringa, jamii ya wananchi wa Moshi, ya kujiendeleza. Hatuwezi kusema jamii hii itabaki kuwa duni toka enzi na enzi mpaka leo tunaona kwamba lazima tuipe fursa pia ya kujiendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jamii hii hairuhusiwi kulima katika eneo lile tunalazimika kuwapa chakula kidogo ili kuwasaidia, lakini jamii pia nayo imebadili sana, leo hii jamii ya Ngorongoro sio wafugaji 100%, kwa kiasi kikubwa pia kuna watu wanahitaji kulima kuna watu wengine mle zaidi ya asilimia 25, hawana ngombe hata mmoja kwa hivyo siyo wafugaji, hawana mfugo hata mmoja, kwa hivyo siyo wafugaji. Je, hawa watu wanaishije, huwezi kusema wanaishi kwa kutegemea maziwa na nyama peke yake, kwa hivyo tumeona tugawe sehemu kadhaa tutengeneze vijiji *proper* vijiji ambavyo wananchi wataruhusiwa kufanya shughuli zozote zile za uendelezaji, wataruhusiwa kumiliki ardhi, wataruhusiwa kufanya shughuli za kiuchumi nyingine kama sehemu nyingine yoyote ile ya nchi, kwa sababu kwa sasa hivi wanahesabika wako ndani ya hifadhi. Kwa hivyo wamekuwa *limited* kufanya shughuli kadhaa ambazo zinatambulika na lazima zifanyike kwa kibali maalum. Kwa hivyo, tunaona tutaanisha sasa vijiji mahususi katika eneo hili ambavyo vitakuwa haviingiliani sana na uhifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, tutabakisha maeneo ambayo yatatumika kwa ajili ya shughuli za uhifadhi mseto ambapo wanyapori watapita humo na wananchi wataishi katika maisha yale ya kizamani ya kimila ya kiasili ya kimasai kama ambavyo iko sasa. Kwa hivyo tutaweka maeneo hayo matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo tunaona kwamba eneo lile bado ni finyu sana ni lazima tu-*annex* maeneo ya jirani ambayo yana uhifadhi pia yana mila zinazofanana na watu wa pale ili eneo liwe kubwa zaidi ili wananchi tutakapokuwa tunawahamisha kwenye maeneo yale nyeti tuwasogeze pemberi hapo waweze kukaa. Sasa

tutaweka mfumo ambao utatoa motisha kwa watu ambao watakubali kuhama wao wenyewe katika eneo moja kwenda eneo linguine, lakini pia tutaweka masharti magumu kwa watu ambao watataka kuendelea kubaki katika eneo hilo. Lengo letu ni kutotumia nguvu katika kuendelea kuhakikisha hifadhi ya eneo la Ngorongoro inabaki kuwa endelevu kwa vizazi na vizazi vinavyokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda kulitolea ufanuzi ni suala la hifadhi mpya ambazo tumeziongeza kwa Shirika la Hifadhi za Taifa (*TANAPA*) na hizi ni yale yaliyokuwa mapori ya akiba matano na ninayo furaha kiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba mchakato ambao tuliuspisha hapa Bungeni kwenye Bunge lililopita kupitia azimio la kupandisha hadhi mapori ya akiba haya matano kuwa hifadhi za Taifa umekamilika, Mheshimiwa Rais ameshaandika tangazo kwenye gazeti na muda si mrefu litakuwa liko *public*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa mkononi ninayo hati ambayo inatoka kwa Mheshimiwa Rais ambapo akitangaza hifadhi tatu mpya za Taifa ambazo kama Mheshimiwa Bernadetha Kasabago Mushashu alivyopenda tumwambie majina ya hifadhi hizo maana yake anasikasikia tu. Naomba nimpe taarifa rasmi sasa Mheshimiwa Bernadetha Kasabago Mushashu kwamba Mheshimiwa Rais ameamua kutangaza Hifadhi ya Taifa ya Burigi - Chato *National Park*, Hifadhi ya Rumanyika - Karagwe *National Park* na hifadhi ya Taifa ya Ibanda - Kyerwa *National Park*. Kwa hivyo hizo ndio hifadhi mpya tatu ambazo zinaingia katika orodha ya hifadhi za Taifa na zitakuwa chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitamke kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii ilianza mchakato wa kuunda mfumo wa kukusanya takwimu na taarifa mbalimbali kutoka kwa watalii wa kielektroniki, pia mfumo wote wa shughuli zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia wizara yenyewe kama makao makuu lakini pia na taasisi zote zitafanyika kwa njia ya mtandao na tumejenga mfumo mpya

kabisa ambao utakuwa mmoja tu na utakuwa chini ya Wizara na taasisi zote watapewa *windows* kwa ajili ya kufanya shughuli zao ujilikanao kama *MNRT Portal*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo huu umeshaanza kutumika kwenye baadhi ya taasisi na taratibu tunaendelea kusambaza kwenye taasisi nyingine na utakapokamilika changamoto ya takwimu itapungua sana na mfumo huu mwisho wa siku utafika mpaka kwa wadau, watu wanaofanya biashara ya *tour*, wale *tour operators*, watu wa mahoteli, wote watakuwa na huu mfumo na watafanya kazi zao kwa kutumia mfumo huu wa kielektroniki ambapo utakuwa unaoana na mifumo mingine kwenye taasisi zingine zote ambazo zinahusika na kuwachaji tozo wadau mbalimbali wa utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, tutakuwa tuna *link* ya OSHA tutakuwa tuna *link* ya BRELA, tutakuwa tuna *link* ya TRA, utaunganishwa na kufungamanishwa na mifumo yote ya Serikali na hivyo itakuwa ni rahisi kulipa tozo, ni rahisi kuletewa *invoice* na itakuwa ni rahisi kufanya *booking na package* za wageni wanaokuja katika kampuni yako. Kwa hivyo tunaamini mfumo huu utapunguza kwa kiasi kikubwa sana *business process* ambazo zinafanywa na taasisi mbalimbali zilizopo chini ya Wizara yetu pamoja na wadau wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Waheshimiwa Wabunge wa kutoka Kusini ambao wanasesma hii ndio kusini *proper* wamezungumzia sana kuhusu mradi wa *Regrow* kutokuwa na *impact* kubwa sana katika Mikoa ya Ruvuma, Lindi na Mtwara. Wameongea kwa uchungu sana kuhusu Mji Mkongwe wa Mikindani, Mji Mkongwe wa Kilwa Kisiwani, hifadhi ya Selou kwa upande wa Mikoa wa Lindi nami nawaelewa. Naomba niseme nimechukua *concern* yao na nitaifanyia kazi kwa ukaribu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia napenda pia niwape taarifa tu kwamba Mji Mkongwe wa Mikindani pia tumeshausajili kwenye urithi wa dunia na kila mwaka

tunafanya Tamasha la Mji Mkongwe wa Mikindani, pia Mji Mkongwe wa Kilwa nao tuko katika mchakato wa kuusajili ili nao uwe katika orodha ya miji ambayo ni urithi wa dunia. Pia tuko katika mpango wa kuendeleza utalii wa fukwe na kwa sasa tutaanza na fukwe za Kigamboni na Bagamoyo. Kwa kuanzia tumeshaandika andiko, liko tayari na katika hatua ya pili sasa tutazungumzia fukwe za ukanda huu wa kusini hii ya Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu fukwe ya Mnazibay tunafahamu fukwe ya Kisiwa cha Mafia ni katika fukwe bora kabisa duniani na zinapendeza kwa kweli madhari yake na hilo halina mjadala, halibishaniwi, ni ukweli usiopingika, lakini tunakwenda kwa awamu. Katika awamu ya kwanza tunaona kwanza tufanye kazi kubwa ya kuwekeza kwenye utalii wa fukwe katika Jiji la Dar es Salaam na hapa tumeangalia sana uwepo wa miundombinu. Ili uwe na *product* ya utalii ambayo inafanya kazi kimkakati ni lazima uwe karibu na uwanja wa ndege wa Kimataifa. Ili kuwe kuna uwezekano wa zile *long-haul flight* kufika na kushusha wateja na wateja kufika kwenye kivutio kwa haraka zaidi kuliko kuwa na *stop* nyingine tena kwamba achukue *local flight* kwenda kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, tumeona katika kukuza fursa ambayo inakuja na utalii wa fukwe, utalii wa mikutano na utalii wa meli, tuwekeze kwanza katika Jiji la Dar es Salaam. Huu ni mradi mkubwa sana ukianza huu mradi, dunia nzima itatikisika kwa sababu idadi ya watalii itaongezeka kwa kiasi kikubwa sana. Pia ni *concern* ya Waheshimiwa Wabunge kwamba tuongeze idadi ya watalii hapa nchini. Utalii wa Tanzania kwa kiasi kikubwa kwa sasa ni utalii unaoendana na mazingira asilia, utalii wa *nature*, utalii wa wanyamaporì kwa kiasi kikubwa zaidi ya asilimia 80 na utalii huu pia umejikita katika *circuit* moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliona katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa mwaka 2016 – 2021, tufanye *diversification*, tutanue wigo wa vivutio vyta utalii ili tutengeneze mazao mengine ya utalii, mojawapo ni

hili zao la utalii wa utamaduni ndio maana nazungumzia Mji Mkongwe wa Mikindani, Mji Mkongwe wa Kilwa, Mji wa Bagamoyo na vivutio vingine nya malikale kama vile Isimila, Kalenga na historia ya nchi yetu kuititia Machifu na vitu vingine. Sasa hiyo ni aina moja ya zao la utalii ambalo ni lazima sisi kama Serikali tuwekeze.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao lingine kubwa na muhimu la utalii ambalo ni lazima tuwekeze kama tunavyoolekezwa na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambao tuliupitisha hapa Bungeni ni utalii wa fukwe na lingine ni utalii wa mikutano na lingine ni utalii wa *maze yaani cruise ship*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi tumeona tuanze kwa Dar es Salaam tuunganishe haya mazao yote kiurahisi zaidi na pale tayari tuna *advantage* ya uwanja wa ndege wa kimataifa ambao upo pale na sasa hivi unafanyiwa uendelezaji mkubwa na Serikali, ujenzi umevuka asilimia 99. Kwa hivyo muda si mrefu tutakuwa tuna uwanja wa ndege mzuri zaidi, tuna shirika la ndege ambalo linafanya kazi vizuri. Sasa tukiunganisha na vivutio nya fukwe vilivyopo pale Dar es Salaam na vivutio nya utamaduni itakuwa rahisi sana kupata faida na tija ambayo itakuja na hizi *product*. Kwa hivyo sasa hivi wenzetu wa *TPA* ambao tuko nao katika uendelezaji wa mradi wa utalii wa *cruise ship*, utalii wa meli tunajenga gati maalum kwa ajili ya *cruise ship tourism* na hii itatusaidia sana kuongeza watalii. Kwa tathmini niliyofanya na wataalamu tunaweza tukapata zaidi ya trillioni tatu kwa utalii wa *cruise ships*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo utalii wa meli tu peke yake unaweza ukaleta trillioni tatu. Huu utalii tulionao leo unatuletea trillioni sita. Kwa hivyo kwa haraka haraka tu unaona kwamba kama ni matunda yanayoning'inia chini zaidi, *lower hanging fruits* maana yake *cruise ship tourism* ni lazima tuwekeze kwa haraka sana. Kwa hivyo, tunawekeza katika eneo hili na tayari tunarudisha uanachama wa nchi yetu katika yale mashirika ya kimataifa yanayohusika na *cruise ship tourism* ili tuwe katika mikakati ya kupanga,

kufanya *marketing* mapema ili tutakapokamilisha ujenzi wa gati hili maalum kwa ajili ya *cruise ships* watalii waanze kuingia nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni utalii wa mikutano; utalii huu tukiwekeza vizuri kama ambavyo majirani zetu wamefanya tuna uwezo wa kupata zaidi ya trillioni mbili kutokana na mikutano ambayo itavutiwa hapa nchini. Eneo lingine ni huo utalii wa fukwe ambaao kwa ujumla wake tunakusudia kuanzisha eneo maalum la utalii pale Kigamboni na eneo la Bagamoyo ambapo tutajenga kumbi kubwa za mikutano na hapa nazungumzia mikutano ambayo watu zaidi ya 5,000 wanaweza wakaingia na wakafanya mikutano kwa wakati mmoja. Sizungumzii ukumbi kama ule tulionao sasa wa *AICC*, nazungumzia *project* kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuko katika hatua za kufanya andiko la mradi huu, hatua ya awali ya utafiti imekamilika, sasa tuna *proposal* ambayo itakwenda kwa Makatibu Wakuu, baadaye Baraza la Mawaziri na mradi huu ukipitishwa tutaanza kuutekeleza. Uzuri tuna uwezekano mkubwa sana wa kupata fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi huu. Huu ni awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya pili tutakwenda kwenye fukwe za Maziwa pia tutakwenda kwenye fukwe zilizopo Mafia, Kilwa, Mtwara na maeneo ya Tanga mpaka Pangani kuunganisha na hiyo Bagamoyo nilioisema. Kwa hivyo eneo hili kwa kweli tunalipa kipaumbele cha hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyininge ni hoja ya hoteli zilizokuwa chini ya Shirika la Utalii Tanzania (*Tanzania Tourist Corporation*) ambalo lilivunjwa na baadaye mahotelii 17 yakauzwa kwenye sekta binafsi. Katika hoteli hizi kuna hoteli, nilipoteuliwa kwa kweli nilipewa maelekezo ya namna ya kuzifanyia tathmini hoteli hizi zote ili tuweze kuona ni zipi bado ziko *viable* na zipi ambazo haziko *viable* ili tuweze kuvunja mikataba, tuzirudishe ndani ya umiliki wa Serikali na hatimaye tuweze kuzikodisha kwa waendeshaji wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika tathmini iliyo fanyika takribani hoteli 10 zilione kana zina changamoto mbalimbali za kimkataba na katika hizi 10 ilione kana hoteli nne tayari zimekiuka moja kwa moja masharti ya mikataba ya mauziano baina yake na Serikali. Hizi ziko chini ya kampuni moja inaitwa *Hotels and Lodges Limited* na hizi nazungumzia hoteli kama Seronera *Wildlife Lodge*, Ngorongoro *Wildlife Lodge* na Kilimanjaro *Wildlife Lodge* na ile ya Mafia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tuko katika hatua mbalimbali ndani ya Serikali ili kufanya uchambuzi wa nyaraka ambazo zipo, tukishirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wizara ya Fedha na wiki ijayo tutakaa kikao cha mwisho ili kufikia maamuzi ya nini itakuwa hatma ya hoteli hizi nne ambazo moja kwa moja zimeshakiuka masharti ya mkataba ili tuweze kuchukua hatua ya kuzirejesha Serikallini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo lilizungumziwa hapa na limezungumziwa na wachangiaji wengi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Peter Msigwa, Mheshimiwa Grace Kiwelu na wachangiaji wengine lilihusu biashara ya wanyamapori hai nje ya nchi. Biashara hii kwa ndani ya nchi bado inaruhusiwa na *actually* tunahamasisha iweze kufanyika pia tunawahamasisha wadau mbalimbali waanzishe *ranch* kwa ajili ya kufuga wanyamapori kwa sababu kuna uhitaji mkubwa wa wanyamapori. Pia nyara ambazo zinaweza zikatumika kwa ajili ya shughuli mbalimbali hapa ndani ya nchi pia kuvutia wawekezaji kutoka nje waje hapa ndani ya nchi wawekeze kwenye viwanda vya Nyara pia ufugaji wa wanyamapori na hatimaye tuweze kuindeleza biashara hii na iweze kuleta tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili sasa ni biashara hii ya wanyamapori nje ya nchi. Kwa sehemu ya kwanza kwa sasa hivi tunafanya mabadiliko ya Kanuni ambapo tutaruhusu hata mabucha ya nyamapori katika maeneo mbalimbali ya nchi kwa ajili ya matumizi ya wananchi. Kwa sababu tunafahamu wananchi kimila lakini

pia hata wengine tu kwa upenzi tu wanapenda kutumia nyamapori kwa matumizi ya chakula ili kupata *protein* na tumeamua kuanzisha mabucha kwa ajili ya kutoa fursa hiyo kwa wananchi. Kwa hivyo hii inapaswa iende sambamba na wananchi kuanzisha mashamba (*ranch*) kwa ajili ya kufuga wanyama pori. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni lile la kupeleka nje ya nchi. Kwa nje nchi kwa kweli mimi huwa sipendi kumung'unya maneno, biashara hii imekoma. Mheshimiwa Peter Msigwa ananiangalia vizuri, naomba uniangularie vizuri na usome midomo yangu; biashara ya wanyama pori hai nje ya nchi haitofanyika mimi nikiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Sababu ziko wazi tu, nilipokuwa Mbunge hapa tulikuwa naye Mheshimiwa kaka yangu Mchungaji Peter Msigwa, kaka zetu waliokuwa Mawaziri wa Wizara hii walishambuliwa sana kuhusu wanyamapori hai. Mara twiga ameenda, mara pundamilia, mara nyani, mara nini! Kwa hivyo Mheshimiwa tulikuwa tunasema na mimi nilikuwa mmojawapo nikirusha mawe na hata rafiki zangu nao walikuwa moja wapo ya watu waliokuwa wakilalamikia sana jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi nilipoteuliwa nikakuta wameshazua na mimi nikasema hii haitofunguliwa mimi nikiwa Waziri. Kwa hivyo hii tumeifunga hatutosafirisha. Mapendekezo ya Mheshimiwa Msigwa ni kwamba pengine kuna mijusi, kuna ngedere kwenye mashamba ya watu, kuna kwereakwerea; na pia hata Mheshimiwa Adadi Rajab naye analalamikia vipepeo kwamba tungeweza kuwaruhusu wananchi wanaofuga wanyama hawa wao wenyewe wasafirishe nje ya nje, ama walipo kwenye maeneo ya wazi wachukuliwe wasafirishwe nje ya nchi. Tungeweza kufanya hiyo, lakini hatutaki kuweka hiyo *principle*, kwamba tunaruhusu baadhi ya wanyamapori na tunakataza baadhi ya wanyamapori. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tumeamua tu kufunga milango ya wanyamapori ambao ni urithi wa kiasili wa Watanzania kutoka nje ya nchi, hawatatoka. Hata chawa hatatoka, hata kunguni hatatoka, kwa hivyo *size* ya mnyama

haita-matter. Hakuna myamapori hai atatoka mipaka ya Tanzania kihalali, kwa njia ya biashara kwenda nje ya nchi eti kwa sababu tunataka kipato, hapana. Nimesema anayetaka kufanya biashara ya nyara afuge, aendeleze hizo nyara zake hapa, azitengeneze hapa, atengeneze hizo bidhaa hapa, auze bidhaa hizo nje ya nchi. Anayetaka kufuga ili waje watazamwe, aanzishe *zoo* yake hapa na sisi tutamuunga mkono, afanye hiyo biashara ya *Zoo*hapa, kana ana wageni awatoe huko kwao awalete hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini biashara hii ya watu kununua wanyama hapa kwenda kuweka kwenye ma-zoo huko; kwa mfano vipepeo, kule Marekani kuna *zoo* kubwa sana wamejaza mle vipepeo ambao wanatoka *Amani Nature Reserve* hapa Muheza kwa kaka yangu Mheshimiwa Adadi, na watu wanaingia kwa gharama kubwa kwenda kuwaona pale. Sisi wazo letu ni kwamba, hawa vipepeo kwa sababu ni mahsus na ni pekee kwa hapo tu *Amani Nature Reserve* hawapatikana sehemu nyingine yoyote ile duniani, vipepeo wa aina ile, basi ni bora na nilishaagiza Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania ashirikiane na wale wananchi ambao wanafuga vipepeo pale tujenge *Museum* ya kwetu pale. Tujenge *Zoo* tuwaweke wale vipepeo pale kiwe kivutio kimojawapo cha utalii katika eneo lile, kwa sababu tayari watu wanapenda kwenda kutembea kwenye Msitu wa Amani na kwenda kuoga kwenye yale maporomoko yaliyoko pale kwenye mito ile iliyoko pale. Watalii wengi wanaenda pale na wengine wanaenda kutembea kwenye ule msitu, ni kivutio tayari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tuongeze tu *product* nyingine ya utalii kwa kuanzisha *zoo* pale tuweke hao vipepeo na watu waende wakawaone pale. Kwa hivyo wale wananchi ambao wanafuga na maisha yao wanayaendesha kwa kupata kipato kutokana na vipepeo, basi watakuwa wanawapeleka pale kwenye *museum* kila baada ya muda wanawapeleka pale na watu wanakuja kuwaona na wananchi wale wanapata faida inayotokana na vipepeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu wale wafanya biashara wakati zui o linatolewa mwaka 2016 mwezi Mei, walikuwa wameshalipa fedha kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali kutoka Serikalini. Tayari tathmini hii imefanyika, uhakiki umefanywa na Wizara ya Fedha na hao wananchi watarejeshewa fedha zao ambazo walikuwa wameshalipa ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kulitolea ufanuzi ni eneo la uwindaji wa kitalii. Biashara ya uwindaji wa kitalii kwa kweli ilikuwa inafanya vizuri mpaka mwaka 2008/2009 na baadaye biashara hii ikaanza kuanguka. Sababu za kuanguka ni nyngi lakini tatu mahsusimba ambazo napenda kuzisema hapa ni pamoja na kuvamiwa kwa maeneo yanayotumika kwa ajili ya uwindaji wa kitalii na wananchi kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kibindamu, zikiwemo killimo, ufugaji pamoja na makazi. Hyo imekuwa iki-*discourage* sana wawekezaji katika sekta hiyo lakini pia hata wawindaji wanaokuja kuwinda katika maeneo hayo; kwa sababu wawindaji hawa ni watu wanapenda wayakute haya maeneo katika uasilia wake. Sasa wakikuta mle ndani kuna ng'ombe anaona sasa hili tena siyo pori hiki tayari kimeshakuwa kijiji siyo tena pori kwa ajili ya uwindaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu nyngine ilikuwa ni zui o ambalo liliifanywa na nchi za nje, huko ambako ni masoko yetu makubwa kama Marekani kuititia ile *U.S Fish and Wildlife Service* ya Marekani pamoja na *Scientific Review Group* ya Umoja wa Ulaya; kwamba nyara za simba na tembo zisiingizwe katika nchi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kama wawindaji wanakuja huku kuwinda halafu kiu yao ni kupata hizo nyara za wanyamaporu kama nyara za simba na tembo; nchini kwao kule kama haziruhusiwi kuingia maana yake hata wao kuja kuwinda huku haina maana tena kwa sababu kinachowafanya waje kuwinda ni wao kupata hizo nyara. Kwa hivyo lile zui o kule limetusumbua sana katika biashara hii. Kingine ni wanaharakati ambao wanapinga uwindaji wa wanyamaporu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo haya mambo makubwa matatu yalisababisha kwa kiasi kikubwa sana biashara hii kuanguka hapa duniani na si Tanzania peke yake. Kwa hivyo mapato yalishuka lakini pia changamoto zikawa nyingi kwa hawa waendeshaji wa biashara hii, kwa maana ya zile kampuni za *Hunting Operators*, matokeo yake sasa wakarudisha maeneo mengi Serikalini; na wakati mimi nateuliwa kuwa Waziri kwenye Wizara hii nilikuta vitalu takribani 81 viko wazi. Kwa hivyo biashara kwa kweli ilikuwa imeanguka kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumefanya jitihada kama Serikali kwa kushirikiana na wadau hao kufanya mageuzi mbalimbali katika *sub sector* hii. Mojawapo likiwa ni kuzungumza na *United States Fish and Wildlife Service* pamoja na hii Taasisi ya Nchi za Ulaya inayojulikana kama *Scientific Review Group* ili waweze kuruhusu nyara ziingizwe katika nchi zao kutoka nchi za Afrika na kwa sababu *lobbying* iliyofanywa na Serikali za nchi za Afrika imekuwa kubwa, zaidi ni kuwaelimisha kwamba uwindaji si kitu ambacho kinapunguza *population* ya wanyama huku Afrika lakini ni kitu ambacho kinasaidia kupata mapato ambayo yanatuwezesha kulinda maeneo haya. Kwa sababu gharama ya kuyahifadhi na kuyalinda ni kubwa mno, haya maeneo ni makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania 1/3 ya maeneo yetu ni hifadhi, kwa maana ya asilimia takribani 33 ni hifadhi. Kuyalinda maeneo haya halafu kama hayaingizi fedha ni mzigo mzito sana kwa Serikali, lakini tumeyalinda kwa faida yetu, kwa faida mbalimbali ya kiikolojia lakini pia kwa faida za vizazi kutoka nchi mbalimbali ambavyo vinakuja kutumia maliasili hizi. Sasa jukumu la kuzilinda haliwezi kuwa la kwetu peke yake, kwa hivyo kuwaomba watusaidie tupate fedha kwa ajili ya kulinda na yenyewe inakuwa *too much* kuombaomba. Kwa hivyo ni bora tufanye biashara kwenye maeneo haya ili mapato yatumike kurudi kuendelea kuyahifadhi maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo elimu ya namna hii imezunguka sana huko Ulaya, huko Marekani na baadhi

ya *states* za kule Marekani wameweza kuruhusu nyara ziingizwe katika hizo *states* zao. Baadhi ya nchi za Ulaya wametuelewa na wenyewe wameweza kufungulia nyara ziweze kuingia katika hizo nchi zao, kwa hivyo mafanikio tumeanza kuyapata kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tumepitia kwa ujumla wake; niliunda Kamati mwaka jana mwezi Machi; ambayo imepitia sekta yote hii ya uwindaji wa kitalii na imetuletea ushauri. Kamati ilikuwa ndani yake ina wadau na hatimyae wameleta ushauri kwamba kuna mambo kadhaa ambayo tuyafanyie mojawapo likiwa ni hilo la *lobbying* lingine likiwa ni eneo la kufanya *marketing* vizuri zaidi, lakini pia lingine likiwa ni kuvutia *professional hunters* ambao hawa ni wawindaji bingwa ambao wana elimu na ujuzi mahsus kwa ajili ya kuwindisha wageni waje Tanzania ili kufanya kazi ya uwindaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo walipendekeza tupunguze tozo ambayo tunawachaji hao wawindaji bingwa kutoka nchi nyagine, wengi wanatoka nchi ya Afrika ya Kusini na nchi ya Zimbabwe na wachache kidogo Botswana pale. Kwa hiyo tumeefanya mabadiliko hayo kwenye kanuni, tumerekebisha hizo tozo mbalimbali, tumerekebisha tozo za wanyama, za kuuza nyara, *top fees, game fees* na kwa kiasi kikubwa haya mabadiliko kwa kweli tuliyaita *hunt more for less*; gharama za kuja kuwinda Tanzania zimepungua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hata vitalu vyenyewe tumeona tuvibadilishe *category*. Tulikuwa tuna *category* tano, sasa tumezishusha zimebaki *category* tatu, lakini pia tumeona tuongeze muda wa kumiliki kitalu badala ya kuwa na miaka mitano tunapeleka kitalu daraja la kwanza na kwa daraja la pili mtu atawenza kuwinda kwa miaka kumi katika eneo lile. Pia kwa daraja la tatu tumesogeza muda badala ya miaka mitano tumepeleka mpaka miaka 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo kwa mtu ambaye atashiriki kwenye biashara hii akapata kitalu atakuwa na uhakika ile tunayoizungumza kila siku, akina Mheshimiwa

Msigwa anazungumzia hapa, *stability* ndiyo hiyo tunayoizungumza. Kwamba mtu atakuwa na kitalu kwa miaka 10 ama kwa miaka 15 bila kuingiliwa na Serikali *as long as* analipa tozo mbalimbali ambazo anapaswa kulipa. Kwa hivyo ataweza hata kuendeleza kujenga kambi nzuri, kambi za kudumu kwa muda wote huo akiwa na uhakika kwamba kwa miaka 10 ata- *operate* kitalu chake bila shida yoyote ile, kwa hivyo anaweza hata akapanga safari za miaka 10 za wageni wake. Kwa hivyo hayo ndiyo mageuzi ya *hunt more for less* ambayo tumeyafanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na mageuzi hayo, inakuja *issue* ya kuanzisha utaratibu wa kugawa vitalu kwa njia ya mnada. Tumeona tuweke utaratibu wa kugawa vitalu kwa njia ya mnada wa kielektroniki, mnada ambaao utawafaidisha watu wa ndani ya nchi lakini pia hata wa nje ya nchi. Lengo ni kuongeza ushindani ili tupate bei kubwa zaidi kwa kila kitalu ambacho tutakuza, lakini pia lengo ni kuweka uwazi zaidi, kuongeza *more transparency* ambayo ilikuwa ikilalamikwa sana. Ilikuwa ukiwa Waziri wa Maliasili na Utalii siku ya kwanza ukipiga hodi Wizarani, basi kuna makampuni mawili yatakutembelea hapo na yatakapoondoka yatakuachia *briefcase* zenye *dollar* za kutosha. Sasa huo utamaduni tulikuwa tunasikia hizo hadidhi, kwa hiyo mimi nilipoingia pale nikasema hapana, mimi sitaki kukutana na wafanya biashara tutaweka utaratibu ambaao ni wazi, utaratibu ambaao utatoa haki kwa kila mtu na mimi sitaki kuwa na *contact* na mfanya biashara. Wao wakutane na mnada kwenye mtandao wa-*bid* na atakayeshinda ndiyo ameshinda, hakuna haja ya kumjua Waziri ili uweze kupata kitalu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo huo uwazi pia tunaamini utavutia sana wawekezaji kwa sababu watakuwa na uhakika wa kupata kitalu kama amefika ile bei ambayo tunaitarajia. Kwa hivyo haya ni mageuzi ambayo nilipenda kuyasema, na kwamba si kwamba matamko ya Waziri yameweza kutikisa biashara hii. Leo hii nafikiri mmeona bajeti yetu inavyoenda vizuri hakuna malalamiko sana kutoka kwa wadau, wadau wameridhika na wadau wenyewe

wanatusifia. Ukienda kuangalia kwenye mitandao hotuba zao wanazotoa wanasifia, wanasemwa Wizara sasa iko *stable*, biashara imekuwa nzuri zaidi kuliko kipindi chochote kile katika historia ya Wizara ya Maliasili na Utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ninyi wenyewe ni mashahidi, bajeti yetu imefika hapa Wabunge wengi wamechangia, wametupa pongozi tunawashukuru, tunazipokea lakini kiukweli *credits* hizi ziende pia kwa wadau wetu kwa sababu wamekuwa wakitupa ushauri na sisi tulikuwa tunatega masikio vizuri, tunajaribu kuilewa biashara na tunajaribu kufanya maamuzi ambayo yana faida kwa Serikali na faida pia kwenye sekta yenye kwa ujumla wake. Hiyo imesaidia sana hata migogoro humu na Waheshimiwa Wabunge imekuwa midogo kwa sababu tumejifunza sana kusikiliza na kufanya maamuzi ambayo yanakubalika na wadau wote. (*Mkofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uhifadhi na ulinzi wa maeneo ya wanyamapori tumeuimarisha sana. Nilisema jana katika hotuba yangu hapa, kwamba tumeunda Jeshi Usu, tumefanya *transformation* kubwa sana katika eneo hili sasa tuna Jeshi Usu imebakia tu Mheshimiwa Rais kuwavisha vyeo wale Makamishna. Kwa hivyo leo hii sisi kwa mfano *TANAPA* mmezoea kumuita Mkurugenzi Mkuu Kijazi, leo hii yule ni Kamishna wa Uhifadhi ni *Conservation Commissioner (CC)*, ndiyo cheo chake si tena Mkurugenzi Mkuu. Hivyo hivyo kwa *TAWA*, *TFS*, kwa Ngorongoro, wale ni Makamishna wa Uhifadhi ni *Conservation Commissioners*. Kwa hivyo hii ni matokeo ya mabadiliko makubwa tuliyyafanya ya kuji-*transform* kutoka kwanye mfumo wa kiraia kwenda kwenye mfumo wa Jeshi Usu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Majenerali ambao ni Wenyeviti wetu wa Bodi za Taasisi hizi, lakini pia *Major General/Milanzi* ambaye alikuwa Katibu Mkuu wetu wakati mimi nateuliwa kuwa Waziri kwa sababu walitupa sana *inputs* za kuweza kutufikisha kukamilisha mchakato wa kuwa Jeshi Usu na wanaendelea kulilea jeshi hili mpaka litapokuwa imara. Tunatoa mafunzo kwa watu

wetu, tunaimarisha Kikosi Kazi cha Taifa dhidi ya ujangili ambacho kinafanya kazi kubwa na nzuri sana ya kizalendo ya kuimarisha ulinzi lakini pia kufanya ufuatiliaji wa majangili. Sasa hivi kwa kweli ukitembea, alisema jana Mheshimiwa Catherine Magige, ukitembea huko utakutana na wanyamapori wanazunguka kila kona. Wanyamapori juzi wamezunguka pale Mvomero, mara mwezi uliopita tulisikia wako pale Morogoro Mjini kabisa, wamekuwa kila sehemu wanaenda wana amani hakuna mtu anayeweza kuwa-*shoot* na kuweza kupata nyama kwa sababu tunafuatilia kwa ukaribu sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwa jangili ukikutwa na nyara ya Serikali utapata kifungo tu, hakuna namna utakwepa. Vitendo vyta rushwa tumevidhibiti kwa kiasi kikubwa kwa sababu kikosi kazi kina watu kutoka vyombo mbalimbali vya ulinzi na usalama. Kila mmoja anamwogopa mwenzake, hakuna mtu anayeweza kuthubutu kuchezacheza na kesi ya ujangili hata kidogo. Ujangili wa misitu tumeudhibiti kwa kiasi kikubwa; alizungumza Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi, kwa kweli tuko vizuri sana. Hata kwenye eneo la biashara ya mbao naona muda umeniishia ningefafanua zaidi lakini tuko vizuri sana, tumedhibiti sana ujangili wa mazao ya misitu na tunafanya mabadiliko makubwa sana kwenye sekta ya misitu kwenda kwenye hiyo mamlaka ambayo umezungumzia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kubadilisha mfumo mzima wa kupata mkaa kwa ajili ya matumizi kwenye majiji makubwa, namna ya kuufungasha mkaa, namna ya ku-*cross check*, namna ya kuvuna, namna ya matanuri yale yatakayokuwa yote haya tumeshafanya kazi na tumeshatunga Kanuni. Kimsingi tuko katika hatua sasa za utekelezaji tu wa mageuzi haya. Tumefanya mabadiliko makubwa sana kwenye eneo hilo nilipenda nigosie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa kweli uhifadhi na ulinzi wa maeneo haya umeimarika sana na nadhani kuliko kipindi chochote kile katika historia ya nchi yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tuna uhakika kwamba tembo akifa ataoza hapo na tutakuta meno ya tembo yako pale pale. Imejitokeza mara kadhaa, imejitokeza kule Loliondo tembo walipata ugonjwa karibu tembo sita walipata kamlipuko fulani nafikiri ilikuwa ni *bacillus anthracis* na wote wakafa pale na meno ya tembo yote tuliyakuta *intact* kwenye mizoga ya tembo. Hakuna mtu aliyeenda kuyaokota ili afanye biashara. Kwa hivyo leo hii kesi ambazo tunahangaika nazo ni za meno ya tembo ya zamani, hakuna kesi mpya, *fresh cases* za mtu ambaye emeenda ame-shoot tembo leo ama ame-shoot faru leo ni za kuhesabu. Yaani sjapata repoti ya hizo kesi zaidi ya mwaka; kwa hiyo ninaweza nikasema ni *negligible*, kwa hivyo kazi ya ulinzi imeimarika sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Eneo la Masoko. Tumejiimarisha sana katika kutangaza vivutio vya utalii hapa nchini na mkakati wetu wa kwanza ni kama nilivyosema ni kuongeza mazao ya utalii, kufanya *geographical diversification* kwenda kwenye maeneo mengine zaidi ya utalii, lakini pia kutumia mbinu za kisasa zaidi kujitangaza ikiwemo kutumia mitandao na kutumia watu mashuhuri. Tumeanzisha *Tanzania Safari Channel* na itakwenda kimataifa Waheshimiwa Wabunge msifikirie itakuwa *local*, na *productions* zake zita-improve. Mheshimiwa Sugu alitupiga mawe hapa asubuhi, *productions* zake zita-improve sana, tutafanya *production* tofauti na hizo unazoziona leo. Haya ni *material* ya zamani lakini ni *material/tutakayoyatoa baadaye* na hususan tutakapoanza kwenda *global* yatakuwa mazuri zaidi, yako kimkakati zaidi na yatakidhi matakwa ya ulichokuwa unakisema. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kutumia watu mashuhuri, Mbwana Samatta ni balozi wetu wa utalii alizungumza Mheshimiwa Molel. Ni balozi wa utalii tumeshamteua na hiyo kazi anayofanya ni sisi ambao tunashirikiana naye kumwelekeza namna ya kutumika vizuri. Kwamba Bendera ya Tanzania ioneokane, ataje Tanzania mara nydingi, azungumze Kiswahili mara nydingi, awaalike wachezaji wenzake mashuhuri kuja Tanzania lakini pia hata

Timu yenyewe ya *KRC Genk* tupo katika mazungumzo nao ili kuwaalika waje wacheze mechi hapa kama ambavyo Simba jana imecheza na Sevilla na mitandao yote ya kula Spain inazungumzia inataja neno Simba, inataja neno Tanzania. Ndicho tunachokitaka, *more visibility*, tuonekane zaidi, ndicho tunachokitaka kwa kutumia michezo. Tumefadhili *AFCON*, tumeshiriki *AFCON*, tume-*brand* uwanja wa Taifa, ni mambo mengi tumeyafanya katika eneo hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hizo kuna *roadshows* ambazo ziko *targeted* ambazo tunazifanya katika nchi mbalimbali za kimkakati kama China, Australia, Russia, India, pamoja na Israel na ndiyo maana mnaona wageni hawa wanakuja kwa China peke yake mwaka huu tutafanya *roadshows* takriban tatu, tumefanya *roadshow* moja hiyo illyofanyika mwaka jana October, tutafanya nyngine mwezi Juni, tutafanya nyngine mwezi Novemba. Lengo letu kwa China peke yake tuweze kupata watalii wasiopungua 500,000 ndani ya miaka miwili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunivumilia, naomba nihitimishe tu kwanza kwa kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunivumilia, lakini pia kwa kunipa fursa hii na naomba nimalizie tu kwa kutoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Kwa hivyo tutaendelea na utaratibu wetu.

Katibu.

NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii

Kif. 1001- *Administration and Human Resources Management* Sh. 4,526,711,080

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki ndicho chenyeh mshahara wa Waziri kwa hivyo kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 101 nimeletewa majina hapa na vyama vyenye uwakilishi hapa Bungeni ya Wabunge wanaohitaji ufanuzi.

Waheshimiwa Wabunge, jana Mheshimiwa Spika, alitukumbusha masharti ya Kanuni hii na kwamba ni jambo gani unaweza ukaomba ufanuzi kwenye kutumia hii kanuni ambayo inazungumzia mshahara wa Waziri. Jambo linakuwa ni moja na linahusu ufanuzi wa kisera. Tutaanza na Mheshimiwa Richard Mbogo.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Tunajua chini ya Wizara hii ya Maliasili na Utalii ina taasisi ambazo ziko chini yake tukiwa tuna *TAWA, TFS, TANAPA* na wote wako kwa mujibu wa sheria na wanasmamia sheria. Tuna Sheria ya Misitu Na. 14 ya 2002 na pia tuna Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Na.5 ya 2009 zote hizi ni katika kulinda hizi hifadhi zetu za wanyama. Hata hivyo, tuna kundi la wafugaji na hususan wafugaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo ambao katika nchi hii wamekuwa wanahangaika sana kuhusu malisho na wakati mwiningine inasababisha wanaingia kwenye hifadhi na wanaanza kulisha mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kabisa mifugo haikati miti, haiangushi, inakula tu majani, lakini hoja hapa ni kwamba faini wanazopigwa kwa taasisi hizi zilizoko chini ya hii Wizara, *TANAPA, TFS*na *TAWA* zinatofautiana kati ya sheria na sheria. Sasa ningeomba Waziri atuambie, je, yuko tayari

ku-harmonize hizi faini wanazopigwa wafugaji hususan wa ng'ombe zikawa na kiwango kimoja katika sheria zote na kiwango hicho chini ya 100,000 tofauti na sasa hivi kilivyo kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo yasipojitosheleza, basi nitashika mshahara wa Waziri.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ufanuzi.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nianze tu kutoa ufanuzi kwamba ni kweli mifugo inakula tu majani na inapita, lakini mifugo inaharibu uoto ulioko pale chini. Pale chini ambapo mifugo inapita na kwato zake kuna mbegu za miti, nyasi pia kuna viumbe ambavyo vinaishi katika maeneo hayo. Kwa hiyo tunapohifadhi ikolojia tunaihifadhi ili ibaki kama ilivyo na uhalisia wake ili kupekana na madhara ambayo yanaweza yakajitokeza endapo tutaruhusu mifugo ikaingia mle na ndiyo maana kwenye nchi hii, asilimia 10 ya ardhi ilitengwa kwa ajili ya maeneo ya malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika ile ardhi asilimia takriban 67 iliyopo kwenye nchi yetu ambayo ni *general land* kwa ajili ya matumizi mengine pia inaweza ikatumika kwa malisho, asilimia ambayo tumeamua kuihifadhi kwa ajili ya kupata mahitaji ya kiikolojia ikiwemo maji kwa ajili yetu sisi lakini pia kwa ajili hata ya hiyo mifugo yenyewe, ikiwemo mvua, huduma ya kuondoa hewa ya ukaa kwenye mazingira ambayo tunatumia sisi na hata hiyo mifugo inatumia, tulisema hii asilimia 33 ibaki kama ilivyo na kuwa eneo la hifadhi, hatuwezi kuruhusu mwingiliano tena na matumizi mengine ambayo ni ya ufugaji ama ya makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutoa maelezo hayo naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbogo kwamba hizi faini zina msingi wake kwenye kila sheria kunawekwa msingi tofauti. Tunachokusudia kufanya marekebisho huko mbele ni kwenye faini ya mifugo ikikutwa kwenye Mapori ya

Akiba, Hifadhi za Taifa, maeneo ya WMA's, maeneo ya *Game Controlled Areas*, huko tunaweza tukafanya sheria zikawa kidogo zinakaribiana na haziwezi kuwa sawa kwa sababu haya maeneo yanatofautiana hadhi za uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maeneo ya misitu pia kutakuwa kuna sheria yake. Kwa kuwa sheria zote hizi kama nilivyosema kwenye hotuba yangu hapo jana tunazifanyia mapitio tusubiri wakati muafaka ukifika hayo mapendelekezo ya mapitio yatakuwemo humo *accordingly* kwa jinsi ambavyo Serikali itaona inafaa. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbogo.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo ya Waziri, lakini changamoto iliyo po kwa wafugaji sasahivi ni kiwango wanacholipa sasa hivi kutokana na hizo *offence* zinazowakuta na ukiangalia *control* ya hizi fedha pia bado iko chini. Mtu anakamatwa porini huko anamalizana na mfugaji...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Richard Mbogo kwa wakati huu aidha unakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, kama hukubaliani nayo unaenda moja kwa moja kwenye kutoa hoja kwa sababu hupewi muda wa kueleza mara tatu. Unapewa mara mbili na mwishoni utafunga wewe kama hujamwelewa maelezo Waziri tunaendelea yaani utoe hoja ili watu wakuunge mkono tujadili.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hii ilivyo naomba kutoa hoja ili Wabunge tuweze kuijadili.

MWENYEKITI: Hoja haijaungwa mkono.

Tunaendelea. Mheshimiwa Dkt. Mponda.

MHE. DKT. HADJI H. MPONDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Waziri katika hotuba yake ukurasa wa 71 ameelezea uhifadhi na ulinzi wa hifadhi, lakini

amefafanua zaidi kwamba kutakuwa na ushirikishwaji wa wadau pamoja na kutoa elimu na uhamasishaji na ameeleza zaidi namna gani *TANAPA* watakapotekeleza hilo na *TFS*, lakini upande wa *TAWA* ambao wana maeneo makubwa, *TAWA* hawa wana mapori tengefu na mapori ya akiba, sasa wengine tunaishi maeneo yale ambayo kama hakutakuwa na ushirikishwaji, uhamasishaji na elimu, maeneo yale ndiyo yanafuga wale wanyama, baadae wakipanda *grade* yanakuwa kama hifadhi. Sasa nini utaratibu na mkakati kupitia *TAWA*, ushirikishaji na elimu na uhamasishaji hasa wananchi katika maeneo yale ya mapori tengefu na mapori ya akiba.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyeekiti, ni kweli kwamba Mheshimiwa Waziri nadhani amezungumza zaidi kuhusu *TANAPA* na *TFS* lakini hakumaanisha kwamba *TAWA* wao hawawezi kushirikisha jamii wala hawawezi kutoa elimu kwa jamii namna ya kushiriki kwenye uhifadhi. Ninachotaka kumhakikishia tu Dkt. Mponda ni kwamba *TAWA* pamoja na *TFS* pamoja na *TANAPA* wote kwa pamoja kwa nia ya kujenga mahusiano na jamii lakini kwa ajili ya matumizi endelevu ya maliasili hizi, wanao wajibu wa kutoa elimu na kushirikisha jamii zote ambazo zinazunguka maeneo haya yenye hifadhi. Kwa hiyo nimhakikishie Dkt. Mponda kwamba wote wanawajibika. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Naona Mheshimiwa Mponda ameridhika na majibu.

MHE. DKT. HADJI H. MPONDA: Mheshimiwa Mwenyeekiti, ndio nimeridhika.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Cosato Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyeekiti, kuelekea uchumi wa viwanda, viwnada kati ya vitu ambavyo

vinahitaji ni kufikishiwa malighafi kwa wakati. Wakati wa mchango wangu kati ya mambo ambayo nilichangia ni kuhusu kuiomba Serikali iweze kuruhusu usafirishaji wa mazao ya misitu kwa muda wa saa 24, kama tunavyosema kuelekea uchumi wa viwanda, ili kuvizezesha viwanda kufikishiwa malighafi kwa wakati na hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata maelezo kutoka kwa Serikali, jambo hili ambalo tumekuwa tukiliomba kwa muda mrefu na ninakumbuka Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wakati wakijibu swali langu tarehe 4, Machi wakati tunaanza Bunge hili, Mheshimiwa Waziri alilielea Bunge lako Tukufu kwamba yeche pia sio muumini wa kufanya kazi saa chache, angependa ili kukuza uchumi watu ikiwezekana wafanye kazi saa 24. Kwa hiyo ningependa kupata maelezo ya Serikali, jambo hili limefikia wapi ili wananchi wale ambao wanafanya biashara hizi lakini ambao wangependa kufikisha malighafi viwandani kwa wakati waweze kupata ahueni kutokana na kauli ambayo watakuwa wameisikia kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ufanuzi.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba nilisema hapa Bungeni tarehe ambayo anaizungumzia Mheshimiwa Cosato Chumi *colleague* wangu kutokea *DARUSO* kwamba mimi siamini kwamba tunapaswa kufanya kazi saa 24 tu, natamani hata yangekuwa 26 ili tuweze kukimbia kuweza kupambana na umaskini katika nchi yetu. Kwa hivyo nikiona kuna sheria ambayo inazuia watu wasifanye kazi usiku mimi ni mtu ambaye naumia sana na ndiyo maana nilisema hapa Bungeni kwamba nilikwishaanza mchakato kwa kupata ushauri wa kitaalam kwamba hivi tunawezaje walau kuruhusu hizi *exotic species* ambazo zinalimwa maeneo ya kule Mafinga na Mikoa yote ya Njombe na Iringa ziweze kusafirishwa hata usiku. Tayari Kamati ilikuwa inafanyia kazi suala hilo na iliniletea ushauri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijakamilisha kutunga Kanuni Mheshimiwa Chumi tena akanishtaki kwa bosi wangu kwenye mkutano kule Jimboni kwake, lakini hiyo haikunikatisha tamaa, ilinipa moyo wa kufanya kazi kwa bidii zaidi na hapa leo ninayo furaha kwamba leo hii hii tarehe 24 Mei, 2019 Kanuni ambazo tumezitunga zimetangazwa kwenye gazeti rasmi la Serikali. Gazeti namba 417 la tarehe 24 Mei. Kwa hivyo ninayo kanuni hapa, anaweza ukaja akachukua *copyili* uwe na uhakika kwamba kuanzia leo sasa inaruhusiwa kusafirisha mazao ya misitu. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipende kabisa kuishukuru Serikali...

MWENYEKITI: Kama umeelewa unaachia tunasonga mbele. *List iko* ndefu hapa Mheshimiwa.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, *in fact* sikuwa nimeshika, naishukuru Serikali. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nimwite sasa Mheshimiwa Peter Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Katika majibu ya Mheshimiwa Waziri alizungumzia kuhusu biashara ya wanyamapor (viumbe hai). Natambua kwamba Sheria Na.5 ya Wanyamapor na Kanuni zake za mwaka 2009 zimeruhusu biashara ya wanyamapor lakini zimeweka *class*. Sasa nilichokwu nazungumza, mimi sizungumzii wale twiga na tembo ambaa amewazungumza na kimsingi twiga na tembo katika nchi hii hawakutoroshwa, walisafirishwa kihalali na Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninachokizungumza ambacho naomba watu wote waelewe vizuri, nazungumza ile *class* kama sijaikosea vizuri ni *class* namba 12 ya wale watu wanaokamata *spiders*, nyoka, wanahangaika na sumu na hivyo vipepeo, *fine!* Mheshimiwa

Waziri amesema kwamba biashara hizi kwa sababu ya tija zibaki nchini hazitasafirishwa, *that's fine* lakini wale watu wakati biashara hii inastishwa mwaka 2016 walikuwa ni wafanyabiashara, walikuwa *wana-contract* mbalimbali, wengine walikopa mikopo benki, wengine walikuwa wamechukua hela za wateja nchi za nje, wengine walikuwa wameshakamata wanyama. Amezungumza hapa kwamba kuna fidia ambazo pesa walileta Serikalini watalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipate *commitment* ya Mheshimiwa Waziri, je, watawalipa hasara yote waliyoipata kwa sababu walikuwa wanafanya biashara yao kihalali ili tuwarudishe pale walipokuwepo. Kama sitapata majibu mazuri nitakamata shilingi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, ufanuzi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba taarifa ya Kamati lakini Taarifa ya Msemaji wa Upinzani ilionesha kwamba kuna hao wananchi ambao walikuwa wanafanya biashara ya viumbe hai na Mheshimiwa Waziri amejibu vizuri kwamba biashara hiyo hapo awali ilikuwa inafanyika kisheria lakini nyakati zinabadilika. Serikali yetu sasa ya Awamu ya Tano imeona hakuna sababu ya kuendelea kuuza wanyama hai nje na nashukuru kwamba Mheshimiwa Msigwa amekubaliana na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala ambalo anazungumza ni kuhusu fidia ambalo pia Mheshimiwa Waziri ameliweka vizuri kwamba Wizara yetu iko katika hatua za mwisho za malipo ya hao wananchi ambao walikuwa wamelipia tayari na kimsingi naomba tu niseme ukweli kwamba sisi hatujandai kulipa fidia, tunajiandaa kuwarejeshea pesa zao ambazo walikuwa wamelipia kwenye Serikali kwa ajili ya kufanya biashara. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka hivi tunavyosimama, sheria bado inaruhusu na wale watu walifanya baishara yao kihalali. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri anaposema kwamba watawalipa zile pesa walizoipa Serikali ni kwamba Serikali imenyamg'anya hela, imedhulumu, imevuruga biashara za wale watu. Kwa hiyo, naomba Bunge lijadili kwa sababu sijapata *commitment* naomba kutoa shilingi ili Wabunge wenzangu waniunge, natoa hoja ili Wabunge tujadili kuhusiana na suala hili kwa sababu Serikali haijajibu vizuri.

MWENYEKITI: Sawa. Sasa Waheshimiwa Wabunge tukae kwanza kabla ya kuunga mkono hoja. Mheshimiwa Msigwa, nakupa dakika moja, tunyooshee hoja ipi itakayosababisha Bunge kufanya maamuzi, dakika moja, hoja ipi unataka uungwe mkono ili Bunge lijadili.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu nimesema hawa watu walikuwa wanafanya biashara kihalali, waliingia kama unavyojuwa wafanyabiashara wanakuwa na mikataba ya kibenki, wanakuwa na mahusiano mbalimbali duniani, hii ni biashara ya Kimataifa. Sasa Serikali hapa inasema fidia zile pesa zilizoingia Serikalini, lakini hawa watu walikuwa wanafanya biashara kihalali kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa ni Serikali yenyewe imesimamisha tena imewasimamishia kinyume cha sheria, sheria bado ipo. Sasa ninachotaka hasara na gharama zote walizoingia hao wafanyabiashara, nataka Serikali iwalipe fidia gharama zote *including* hizo za Serikali na zile zingine ambazo waliingia kwa sababu ni Serikali ambayo iliwaingiza kwenye shida hiyo.

MWENYEKITI: Sasa hiyo ni sera gani? Sera ya Fidia? Yaani hiyo ni sera gani ambayo unataka hoja yake Bunge mwishoni liamue.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sera inatokana na biashara ya wanyamapori, ni kwenye biashara ya wanyamapori, kwa sababu walikuwa wanafanya baishara ya wanyamapori kisheria, sheria namba

tano inaruhusu kusafirisha viumbe hai, inarihusu mpaka sasa hivi *as we speak*.

MWENYEKITI: Haya, toa hoja uungwe mkono, nione wanaojadili, labda nitawaelewa vizuri.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashikuru sana, naomba nitoe hoja niungwe mkono ili tujadili suala hili ni la muhimu.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono, wabaki wale wanaotaka kuchangia hoja hii. Mheshimiwa Japhary, leo wote waliosimama wameongea ongea, Mheshimiwa Gimbi, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa! A'a', watu lazima wapate fursa ya kuzungumza, nimfute nani kati ya wale wawili niliyowataja, a'a', nimfute mmoja kwa sababu siwezi kuwapa wote, Mheshimiwa Mshashu, Mheshimiwa Getere na Mheshimiwa Kakunda. Hawa waliotajwa wanatosha. Siyo jina lake Mheshimiwa Japhary Michael?

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Aaa, hapana, Mheshimiwa Japhary Michael.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Msigwa. Biashara katika nchi hii zinaendeshwa kwa mujibu wa sharia; wafanyabiashara hawa ambao walikuwa wanafanya hiyo biashara walitimiza taratibu zote za kisheria. Kwa hiyo, nilitegemea kwamba, la kwanza, Serikali ingeleta utaratibu wa kubadilisha sheria hapa Bungeni ndipo ifanye uamuzi mwengine. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, wafanyabishara hawa wamekatiwa utaratibu wa biashara yao kwa ghafula

sana wakiwa tayari wameshatimiza taratibu zote za biashara zao. Sasa leo tunapoamua kuwalipa fidia, hatuwezi kuwalipa *party* ya fidia, lazima tuwalipe fidia ya hasara zote walizopata, ili kuwatendea haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna muda mrefu wamekaa bila kufanya hizo biashara, wana hasara zaidi hata ya muda waliokaa bila kufanya hizo biashara, kwa hiyo, ni vizuri Serikali ifikiri kwa maana zaidi, inawalipa kwa kiasi gani hawa wafanyabiashara ili kwa kiwango fulani hata iwafute machozi kulingana na hasara waliyoipata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na bahati nzuri Serikali ya awamu ya tano inajinasibu kwamba ni Serikali ya kuhakikisha watu wanaishi vizuri, wana...

(Hapa kengele lilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa, kengele imegonga. Mhehimiwa Gimbi Masaba. (*Makofi*)

MHE. GIMBI D. MASABA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, moja kwa moja naunga hoja mkono ya Mheshimiwa Msigwa, kwa namna ambavyo ametetea hoja yake. Kwamba wakati watu wanafanyabiashara ya kusafirisha wanyama kwenda nje walikuwa wanafanikisha matumizi yao ya familia na mambo mengine. Licha tu ya kusafirisha hao wanyama sisi wenyewe walikuwa wanatisaidia kwa sababu hao wanyama wanazaliana, kwa hiyo kadiri ambavyo wanapelekwa nje inatusaidia sisi kuondoa pia hata msongamano wa namna ambavyo wanyama hao wanaendekea kuzaliana hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine, hawa watu wamekuwa wakifanya biashara, si tu ya kusafirisha nje, wamekuwa wakifanya tena biashara ya kutusaidia kupeleka kwenye maonesho kama ya Sabasaba, Nanenane, hao hao wanyama ambao ndiyo wanakwenda kuapeleka kule. Sasa kitendo cha kuwasitishia moja kwa moja si jambo jema.

Kwa hiyo mimi nilikuwa naomba Serikali kabla haijafanya maamuzi haya ni vizuri tuwe tunatafakari ni namna gani tunaweza kuwasaidia hawa watu, watoe muda zaidi ili watu waweze kujijandaa kuliko kila siku tunawaingizia hasara Watanzania. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Benardetha Mushashu.

MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siungi mkono hoja ya Mheshimiwa Peter Msigwa kwa sababu Mheshimiwa Peter Msingwa na mimi hapa na Wabunge wengine watatu tuliwekwa kwenye Tume ya kwenda kuchunguza utoroshwaji wa wanyamapori hai. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo hali ilikuwa mbaya sana, wanyama walikuwa wanatoroshwa, ye ye na mimi tukagundua, kwamba wale waliokuwa wamepewa vibali, unakuta mtu amepewa vibali vya kusafirisha mijusi tumekuta wana wanyama kama kobe. Kuna mahali tumeigia tunamkuta katika *compound* ana wanyama zaidi ya elfu tano, tumeingia kwenye *bedroom* tumekuta kuna nyoka, kuna kobe, kwenye *bathtub* tumekuta aina moja ya mnyama ambaye hatapikani mahali popote duniani, anapatikana Tanzania tu, lakini tulikuta wanao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukaja sisi wenye wene tukaleta mapendekezo humu ndani ya Bunge, sisi ndio tuliopendekeza kwamba hiyo biashara sasa inawafanya wanyama wetu watoroshwe, watalii wataacha kuja Tanzania kwa sababu watakuwa wameshaa-*accumulate* wanyama wa kutosha katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wenye ndiyo tuliotoa hayo mapendekezo, Mheshimiwa Peter Msigwa rafiki yangu *holding ground* tuliyatotoa wote, tukaishauri Serikali ikatekeleza. Kwa hiyo naomba, wanaweza kwenda kutumia mwanya huo vibaya, basi mrudishie Mheshimiwa Waziri kusudi tusonge mbele aweze kwenda kutekeleza bajeti yake. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere!

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja ya Mheshimiwa Msigwa kwa sababu moja tu. Kuna tofauti kubwa sana kama rafiki yangu Msigwa angekuwa anaendelea na pointi yake ile, kwamba wale watu wanaouza mijusi, koleakolea, konokono, mende tutafute kila namna tuwaruhusu; lakini sasa anachokitaka hapa ye ye ni fidia, na hili suala ni la kisheria. Kama kuna mtu anadai madai yake, hakuna Bunge linaloweza kukaa mahali likasema fulani alipwe. Kama mtu anadai kwa sababu ana listi ana kila kiltu. Kama anaona kwamba alionewa kwa wakati muafaka, lazima atakwenda mahakamani kudai. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tujuu kitu kimoja hapa, kwamba Tanzania ilishatunga sheria kuu ya kulinda mallasili za nchi yetu, kwa hiyo sheria zote zinafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho, mikataba iliyokuwa inafanywa na watu wanaouza wanyama ilikuwa inafanywa kwa mikataba, na mikataba hiyo ilishakwisha, haipo mpaka sasa hivi. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEITI: Mheshimiwa Kemilembe Lwota!

MHE. KEMILEMBE J. LWOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nianzde kwa kumuomba Mheshimiwa Msigwa, Waziri Kivuli, arudishe shilingi ya Mheshimiwa Waziri. Jambo la kwanza, kwanza nimesikitishwa na maoni haya kutoka wa Waziri Kivuli na vilevile kama Mjumbe wa Kamati ya Maliasili na Utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili tumeshajidili kwenye Kamati yetu na tulichotaka ni *commitment* ya Serikali ni lini watu hawa watapata fidia na katika majibu ya Mheshimiwa Waziri, ameeleza vizuri kabisa hawa watu watapata fidia. Sasa sijui Mheshimiwa Msigwa unataka kitu gani kifanyike ilhali jambo hili tumeshali-*discuss* na kuliamua

kwenye kamati na Mheshimiwa Waziri ametupa majibu? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Joseph Kakunda!

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa Mheshimiwa Msigwa anafahamu kwamba hoja ambayo ameitoa hapa bahati mbaya sana wafanyabiashara wenyewe hawajaiunga mkono, kwa hiyo ni vigumu sana kuungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge. Kwa mujibu wa taarifa zilizoko Serikalini ni kwamba wafanyabiashara hao waliomba warejeshewe fedha walizolipa, hawaajaleta fidia, kwa hiyo hawana madai ya fidia, wao walidai kulipa hasara walizoingia. Hii kaileta mwenyewe ambayo ni hoja ya kwake, siyo ya wafanyabishara. Kwa hiyo, mimi nilikuwa namuomba Mheshimiwa Msigwa asituotезee muda arudishe hiyo shillingi ili tuendelee na blashara. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa mtoa hoja, Mheshimiwa Peter Msigwa, funga hoja yako.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashindwa kuwaelewa Wabunge wenzangu. Kwanza Mheshimiwa Waziri anasema hapa nisiwapotезee muda, mimi nipo kufanya kazi ya wananchi hapa, hapa hatupotezi muda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba hebu tuwe *sober*, tuwe na *sober mind* tusishabikie tu, nimemshangaa hata Mwenyekiti wangu wa kamati, anasema hili suala tumelijadili. Hawa watu wamemwandikia barua Rais haya ninayoyasema hata kwenye barua waliyompelekeea Rais wameyazunguza haya mambo; lakini haya mambo Waziri mwenyewe umezipata kopi. Hawa watu walikuwa wana *contract*, hapa kuna mambo ya *contract breaching*, *wame-bleach* na *contract* waliyokuwa wanafanya nje, wamefanya biashara ya kimataifa, lakini kuna mambo ya *opportunity cost*, kuna mambo ya *value for money*, ni muda mrefu toka mwaka 2016; halifu leo hapa tunasema tunawatetea wananchi wanyonge, hawa siyo kama wawindaji wale

wenye fedha nyingi, ni watu wa chini kabisa hawa wanafanya biashara ya mijusi, ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine walikuwa wamekamata wanyama walikuwa nao ndani ya nyumba walikuwa wamehifadhi kwenye *holding grounds* anazozisema mama Mushashu na mama Mushashu anaongea *out of context*. Mimi sizungumzii akina Kamlani hawa tuliokuwa tunawachunguza wakati ule, Mheshimiwa Waziri unalielewa ninalolisema. Kwa hiyo ninachotaka kukisema, tutakuwa hatuwatendei haki hawa wanyonge ambao kwanza hivi vitu hawaindi kwenye mbuga za wanyama kama mnavyosema, ni *class* ya 12, ni ndogo, wanawinda huku mitaani, mijusi na konokono, leo tunawapotezea fedha zao halafu leo hapa tunasema, eti tunapoteza muda. Mimi niwaombe Waheshimiwa Wabunge, hebu tusifanye siasa kwenye uchumi wa watu. Wengine wameuziwa nyumba, jana nimezungumza, wengine wamekufa, sasa kama tusipowatetea atawasemea nani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachotaka hawa watu walipwe fidia ya hasara waliyoipata kwa sababu Serikali imewapa umaskini, na *as we speak* sheria ya wanyamaporii inawaruhusu kufanya biashara, maana yake wakieda hata mahakani Government ita-*loose* kwa sababu wamefanya biashara kisheria.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Muda umekwisha, kengele imeshagonga, kwa hiyo, tunakushukuru kwa maelezo uliyoyatoa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hoja hii haiwezi kuamriwa na Bunge kwa sababu, umeshazungumza kwamba

wale watu wana mikataba, Bunge haliwezi kuingia hapo katikakati likaanza kuamua juu ya mikataba kwamba ndiyo walipwe ama wasilipwe, kwa sababu mikataba, hatujaiona sisi. Huko huko nje ndiko ambako hatujaiona, Bunge litaamuaje kuhusu mikataba ya watu binafsi huko nje? (*Makofi*)

Haiwezekani, ndiyo maama tunataka la sera ambalo Bunge linaweza kuimauru Serikali au kuiamurisha Serikali ikafanye jambo, sasa hili tunawaamrishu Serikali ikazungumzie mikataba ambayo wao wanapajua pa kwenda? Siyo....

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti,...

MWENYEKITI: Aa, siwezi kuitoa hoja Mheshimiwa Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba ya nchi za nje na hawa wafanyabiashara haihusiani na Bunge?

MWENYEKITI: Hiyo, mikataba, siyo mikataba ya nchi na nchi, Bunge linaingiaje kati ya mkataba wako wewe na kampuni yako na nchi nyingine, Bunge linaingiaje hapo Mheshimiwa?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nazungumza mkataba na Serikali, hawa waliingga mkataba na Serikali...

MWENYEKITI: Ehe! Umeeleza vizuri, hapo hapo ukiwa umesimama, mkataba wameingia kati yao na Serikali.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Yes.

MWENYEKITI: Waende mahakmani! Bunge linaingiaje hapo Mheshimiwa Msigwa!

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, waende mahakani!

MWENYEKITI: Ndiko wanakotakiwa kwenda! Haliwezi kuingia Bunge hapo katikati. (*Makofi*)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: *Okay!*

MWENYEKITI: Bunge haliwezi kuingia kuamua juu ya mkataba wa mtu na Serikali,

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: (*Alizungumza bila kutumia kipaza sauti*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa, huu mjadala ni wa kuendelea siku nyingine, hata tukikutana pale nje, nitakuelezea sheria za mikataba zinavyofanya kazi, siyo kazi ya Bunge hiyo. (*Makofi*)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo...

MWENYEKITI: Hapana, siyo kazi ya Bunge, Bunge haliwezi kufanya hiyo kazi. Mheshimiwa Msigwa tunaendelea naomba ukae, inabidi tuendelee Mheshimiwa Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti....

MWENYEKITI: Naomba ukae Bunge haliwezi kuingia hapoa Mheshimiwa....

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *that's un fair, its real un fair!*

MWENYEKITI: Haiwezi kuingia hasa kwa kutumia kifungu cha mshahara wa Waziri, haiwezekani....

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani *it is unfair kwa sababu*, kazi ya Bunge ni kuishauri Serikali na kuismamia.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa tusikilizane.

Waheshimiwa Wabunge tuelewane vizuri. Kanuni inayotumika kwenye mshahara wa Waziri ni 101. Chukueni kanuni zenu muisome inaweka masharti gani tunapozungumzia mshahara wa Waziri. Isomeni hiyo kanuni kwa sababu ndiyo tunayoitumia kwenye huu mjadala sasa hivi. Kwa hiyo chukueni nakala zenu Waheshimiwa Wabunge kila mtu anazo hizi nakala, 101 masharti yake yanatutaka tutumi hivyo. Hapana hiyo miaka yote basi bahati mbaya sikuwa nimekaa hapa mimi ambaye nafahamu sheria za mikataba, hiyo ndiyo bahati mbaya. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, nimwite sasa Mheshimiwa Jitu Soni.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi katika ngo wangu wa maandishi na pia nilishawahi kupeleka kwenye kamati, kuna sheria nyingi ambazo zinakinzana na ambazo zinaleta mgongano mkubwa baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi.

Sasa ningependa kujua baadhi ya mifano ya sheria hizo, kwa mfano hii Sheria ya *Wild Life Corridor Disposal Buffer Zone and Migratory Roots Regulations*, 2018, inakinzana na sheria ya Wizara hiyo ya Sheria ya Wanyamapori, kwa mfano namba tano ambapo sheria namba tano imeweke makatazo kwamba shughuli hizi zote zinaweka makatazo tu na ndani ya siku 90 Waziri anaweza kutoa *order* kwamba shughuli zote zile za kibinadamu zisimame katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na Sheria ya Ardhi lakini pia tofauti na ile Sheria ya Wanyamapori ya 2009; na kwenye ile sheria ya 2009 Waziri alipewa mamlaka na ndani ya miezi 12 alitakiwa aweze kusema maeneo yote ambayo ni 43 ya *game controlled areas* ili zippi zitakazobaki ambazo zinakidhi matakwa ya kisheria na zippi ambazo bado. Ya 2009

imekataza baada ya hapo kwamba maeneo yote ambayo ni *game controlled areas*, shughuli yoyote ya kibinadamu iendelee. Leo hii...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele imeshagonga Mheshimiwa Jitu Soni, kwa hiyo nadhani Mheshimiwa Waziri atakuwa ameusikia atoe ufanuzi juu ya jambo lako.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, na kama maelezo yake hayatakuwa mazuribasi niomba wenzangu wachangie.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Amezungumza mambo mawili, la kwanza linahusu migogoro ya kisheria kati ya sheria moja na sheria nyingine, ya kwanza amezungumzia, *actually* siyo sheria ni kanuni, ambazo zinatokana na Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori ya Mwaka 2009 na hizo kanuni zinazohusika na mambo ya *corridor*, maeneo ya mazalia ya wanyamapori, maeneo ya mitawanyiko ya wanyamapori, ni kanuni ambazo zinatungwa na Waziri kutokana na sheria mama, Sheria Na.5 ya Mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia amezungumzia pengine mgogoro ambao unauja kati ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori hiyo Namba 5 ya Mwaka 2009, na Sheria Namba 4 ya Vijiji ya Mwaka 1999, ambayo yenyewe inatambua maeneo ya vijiji na inaweka mipaka, lakini mgogoro unaokuja kwenye sheria ni kwamba Sheria ya Mwaka 1974 ya Uhifadhi wa Wanyamapori iliruhusu mapori tengefu kuanzishwa kwenye vijiji ama vijiji kuanzishwa kwenye mapori tengefu. Hata hivyo ilipokuja sheria ya mwaka 2009 ikakataza kitu hicho kufanyika na Waziri akapewa mamlaka na sheria kwamba ndani ya miezi 12 awe amefanya tathmini na kisha kubaini ni mapori tengefu yapi yabaki kuwa mapori tengefu na ni mapori tengefu yapi yaondoke katika orodha ya mapori tengefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini hiyo, bahati mbaya haikuwa kukamilika, ilianza kufanyika eneo la Loliondo, Waziri aliyejukwepo alifanya tathmini hiyo na akaamua kukata eneo la *square* kilomita 1,500 ili ibaki kuwa pori tengefu na eneo lingine libaki kuwa vijiji ikazua mtafaruku haikukamilika. Pia eneo la Kilombero hapakukamilika, eneo la *Speak* kule Serengeti pia hapakukamilika, kwa hiyo ni kwamba sheria ile haikukamilika utekelezaji wake, kile kifungu cha Waziri kutoa tamko la mapori tengefu yapi yabaki kwenye orodha na yapi yaondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mgogoro wa kisheria pengine ungekuwa huo lakini siyo mgogoro kutokana na tafsri ambayo sisi ndani ya Serikali; tulikuwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali; kwamba mapori tengefu yatabaki kuwa mapori tengefu na vijiji vitabaki kuwa vijiji mpaka hapo Waziri mwenye dhamana ya Maliasili na Utalii atakapoamua kutoa hilo tangazo ambalo anapaswa kulitoa kwa mujibu wa sheria.

Kwa hiyo, mpaka sasa bado tunaendelea kutumia sheria hiyo kutangaza mapori tengefu na kutangaza maeneo ambayo tunayaachia kwenye vijiji, na faraja inakuja kwenye hili agizo la Mheshimiwa Rais la Januari, 15 kwamba kuna maeneo ambayo tutatumia kifungu hicho kuyatangaza kwamba yabaki kuwa mapori tengefu na kuna maeneo ambayo yatabaki kuwa vijiji, kwa hiyo tutaweka ule mstari ambao unazungumziwa. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jitu Soni nadhani ameridhika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jitu Soni nadhani ameridhika, hapana, Mheshimiwa Jitu Soni.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba Waziri ameisema vizuri, na kwamba bado hawakutekeleza yale ambayo walistahili kutekeleza 2009 na hiyo inaleta mgongano katika maeneo mbalimbali..

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jitu Soni orodha ya majina ni ndefu hapa aidha umemwelewa Waziri kama hujamuelewa toa hoja watu waijadili, hatuna muda mrefu.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwelewa na naomba waifanyie kazi vizuri.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Amina Mollel.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba kupata ufanuzi, mwezi Februari tulipitisha azimio la kuyafanya mapori matano kuwa Hifadhi za Taifa, lakini pamoja na kuyapitisha hayo mapori matano, tunafahamu kwamba baadhi ya hifadhi kwa kweli bado hazijiendeshi. Hii pia ni kutokana na kwamba hata zile zinazojiendesha kwa mfano *TANAPA* wana kodi nyingi ambazo kodi pamoja na tozo wanazokatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda tu kupata ufanuzi kutoka kwa Serikali, Wizara husika kwamba ni lini sasa tutaleta kama ni Sheria au Muswada hapa ili basi uweze kubadilishwa hizo na hatimaye kuipunguzia mzigo mkubwa *TANAPA*, kodi ambazo wanatozwa. Naomba tu kupata ufanuzi sina haja ya kukamata mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, ufanuzi.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa hii na nimshukuru Mheshimiwa Amina kwa kulirejesha tena suala ili apate ufanuzi. Kama nilivyosema mchana masuala ya kikodi huwa yana utaratibu wake wa kufanyiwa marekebisho na kipindi hiki Serikali iko kwenye mchakato wa kuandaa Sheria ya Fedha ya mwaka 2019 na katika Taasisi ambazo zimewasilisha maombi yao mojawapo ni Wizara ya Maliasili na Utalii, wamewasilisha maombi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa unafahamu mchakato huu taratibu zake zikoje, naomba nisiseme ni zipi ambazo waliwasilisha, lakini kama nilivyosema mchana tuiswahishe shughuli, shughuli yake haiko mbali ndani ya mwezi Juni tutajadili mambo haya ndani ya Bunge lako Tukufu na nimwombe sana Mheshimiwa Amina avute subira na kipindi hicho tutatoa maelezo zaidi. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake yote kwa kweli kwa kipindi hiki tunaanza kuona dira nzuri ya Wizara hii katika kuchangia kwenye mapato ya Taifa. Hoja yangu hapa leo nataka tu kupata ufanuzi wa Mheshimiwa Waziri ni kwamba tatizo la wanyama waharibifu wakiwemo tembo na hawa viboko, wanasumbua sana wananchi wanaoishi kandokando ya hifadhi au ya mapori tengefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kupata *commitment* ya Serikali, kumekuwa na kauli kwamba tunashughulikia, tunasaidia kuna vile vikundi vya kuweza kuwarudisha wanyama hawa wanapojitokeza, lakini ongezeko la hasa tembo linatishia sana uhai wa maisha ya wananchi na limesababisha wananchi kupoteza maisha na kuharibiwa mali zao. Sasa ningependa kupata *commitment* ya Serikali kwamba tunafanyakaje ili kuwasaidia wananchi hawa sasa wasiweze kuhangainka na tatizo la hawa tembo pamoja na viboko.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ufanuzi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maelezo yangu wakati nachangia hoja nimeleza, pia Mheshimiwa Waziri ameleeza wakati anajibu hoja. Ni kweli kwamba kuna shida ambayo sasa hivi tunaona inajitokeza baada ya udhibiti ambao tumezungumza,

pamekuwa na tatizo la wanyama wengi waharibifu, wanyama wakali kuzagaa kwenye maeneo ya makazi ya watu hasa tembo na wanyama kama viboko na wengine kama nyani na tumbili wameongezeka. Nimeleza hapa kwenye majibu yangu wakati najibu kwamba tatizo hili kwa sababu tumeliona limeongezeka Wizara imeweuka mkakati, lakini mkakati wa kwanza kwa wanyama kama boko, tumefanya utafiti na pale ambapo tumeona kwamba wafanya hawa wameongezeka wamekuwa wengi watavunwa, nafikiri hili nimelieleza vizuri watavunwa na kubakiza kiwango ambacho hakina madhara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanyama kama tembo tunatumia kuelimisha jamii zinazozunguka maeneo ya hifadhi, kwa mfano tunesema ziko njia mbalimbali za kuwadhibiti ikiwa ni pamoja na kupanda pilipili kwenye mashamba, kufuga nyuki karibu na makazi ya watu. Pia tumezilekeza Halmashauri zetu hapa mara zote nilipojibu swalii nimezilekeza halmashauri kuhakikisha kwamba zinapotaka kuajiri watumishi wapya ziweke Maafisa Wanyamaporii ambaao watatumika kwanza kama watu wa *ku-respond* haraka wakati watu wa Wizara wanakuja kwenye maeneo husika. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Chegeni naona amesharidhika. Mheshimiwa Saed Kubenea.

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru. Hoja yangu ni ndogo kidogo, nataka kufahamu kwamba kumekuwa na utaratibu wa watu wanaoshambuliwa na wanyama katika maeneo ambayo mbuga za wanyama ziko karibu na makazi ya wananchi. Wanyama wale wanaposhambulia wananchi Serikali inatoa fidia ndogo sana, ukilinganisha na kiwango ambacho mtu anatozwa anapoua mnyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, wanasesma tembo mmoja analipiwa mpaka milioni 30 na ushee, lakini tembo anapoua binadamu, binadamu analipwa fidia ndogo sana na binadamu ana thamani kubwa kuliko mnyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka Serikali ituambie ni lini italeta Bungeni mabadiliko ya sheria au kanuni zake ambazo zitawafanya watu wanaoathiriwa na wanyama katika maeneo ambapo wanyama hao wanaishi karibu na binadamu kulipa fidia inayolingana na hadhi ya binadamu badala ya utaratibu wa sasa wa kulipa fedha ambayo haitoshi hata kununua sanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama majibu hayataridhisha, nitatoa shilingi ya kuzuia mshahara wa Waziri. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ufanuzi.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza Mheshimiwa Shehe Saed Kubenea anatakiwa afahamu kabisa kwamba hakuna fidia ambayo inaendana na kiwango cha thamani ya binadamu, hakuna. Yeye Muislamu kama mimi Mungu alipoiumba dunia, akamuumba mwanadamu akamteua kuwa kiongozi katika hii dunia, aliweka ile thamani ya binadamu kuwa juu ya kitu chochote kile hapa duniani. Sasa hakuna fidia ambayo utalipa itaendana na usawa wa uzito wa thamani aliyonayo bindamu. Kwa hivyo ndiyo maana Serikali haiwezi kuzungumzia kulipa fidia ya mtu kupotea na kutokana na kujeruhija na wanyamapori. Tunachozungumzia ni kifuta machozi kwamba ni jambo baya limetokea, watu wamelia, watu wamesononeka, basi Serikali inawafuta machozi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na mazao kwa upande wa pili ama mali ambazo zinaharibiwa na wanyama waharibifu, tunalipa kifuta jasho kwamba walau tunamfuta mtu jasho kwa hasara iliyosababishwa na wanyamapori, lakini hatuwezi kusema tutalipa fidia ya mazao yote ambayo yataharibiwa na wanyamapori, maana yake ni kwamba tutashindwa kulipa hizo fidia na kutakuwa hakuna maana ya kuwahifadhi hawa wafanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro hii ni mipana sana, siyo kwamba wanyama ndiyo wanafuata wananchi, sasa hivi ni wananchi ndiyo wanaowafuata wanyama kwenye maeneo yao. Wananchi wengi kwa kiasi kikubwa wanavamia *corridors*, wanavamia maeneo ya mitawanyiko wa wanyama, wanavamia *breeding sites* za wanyama. Kwa hivyo kwa vyovoyote vile wanyama wakifika kwenye yale maeneo ambayo walizoea kuyatumia watakuta watu wameshavamia pale *eitherwanalima* ama wanafuga ama wanaishi na matokeo yake madhara yanajitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, kusema tutaweza kama Serikali kuji-*commit* kulipa fidia ya mazao ama mali zinazoharibiwa hatuwezi na kwa sasa tunachokifanya kwa kweli ni kuboresha kifuta machozi na kifuta jasho ili walau kiendane na mazingira ya sasa, lakini hatuzungumzii fidia hata kidogo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kubenea nakupa tu dakika moja ili utoe maelezo, lakini muda wetu umekwisha tayari, Mheshimiwa Kubenea.

MHE. SAED A. KUBENA: Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Waziri hayardhishi kabisa, sijazungumzia juu ya mazao, nimezungumza juu ya binadamu wanaouawa na wanyamapori na siyo binadamu wote wanawafuata wanyamapori. Kwa hiyo natoa hoja kwamba Bunge hili liweze kujadili jambo hili na utolewe uamuzi. Nakushukuru.

MWENYEKITI: Hoja haijaungwa mkono, lakini pia muda wetu umekwisha. Tumefika muda wa kupitisha mafungu Waheshimiwa Wabunge majina yalikuwepo hapa mengine ambayo hatujaweza kuyafikia kwa sababu ya muda wetu, Waheshimiwa Wabunge tumefika kwenye kusoma mafungu yote kwa pamoja, Katibu.

Fungu 69- Wizara ya Maliasili na Utalii

Kif. 1001- *Administration and Human Resources Management*.....Sh.4,526, 711,080

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Kif. 1002 – <i>Finance and Account Unit</i>	Sh.1,106,080,820
Kif. 1003 – <i>Policy and Planning Unit</i>	Sh.1,430,667,487
Kif. 1004 – <i>Government Communication Unit</i> ..	Sh.323,164,152
Kif. 1005 – <i>Internal Audit Unit</i>	Sh.428,940,166
Kif. 1006 – <i>Procurement Management Unit</i>	Sh. 652,088,742
Kif. 1007 – <i>Legal Services Unit</i>	Sh.369,000, 255
Kif. 1008 – <i>Management Information Systems Unit</i>	Sh.616,077,318
Kif. 1009 – <i>Research and Training Unit</i>	Sh.11, 824,642,727
Kif. 2001 – <i>Wildlife Development</i>	Sh.17,756, 295,632
Kif. 3001 – <i>Forestry And Beekeeping</i>	Sh.21,782,508,388
Kif. 4001 – <i>Tourism</i>	Sh.5, 530,745,787
Kif. 4002- <i>Antiquities Unit</i>	Sh.4,965,726,446

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 69– Wizara ya Maliasili na Utalii

Kif. 1003- <i>Policy And Planning Unit</i>	Sh.0
Kif. 2001- <i>Wildlife</i>	Sh.15,059,140,734
Kif. 3001- <i>Forest And Beekeeping</i>	Sh.13,530,848,000
Kif. 4001- <i>Tourism</i>	Sh.20,300,000,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

(Bunge lilitrudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae, mtoa hoja taarifa.

TAARIFA

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake, hivyo, naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(Makofii)

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge sasa nitawahoji kwa utaratibu wetu kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

*(Hoja ilitolewa na iamuliwe)
(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)*

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka 2019/2020 yalipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kwa niaba yenu nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa hoja yao ambayo walikuwa wameileta hapa, pamoja na watendaji wao kwa maana ya Makatibu Wakuu na Viongozi wote wa Taasisi zilizo chini yao, kwa pongezi nydingi walizopewa na Bunge hili ni dhahiri kwamba wanafanya kazi nzuri. Kwa hiyo nami niwape pongezi za dhati kabisa kwa kazi nzuri wanayoifanya, pia niwatakie kila la kheri katika utekelezaji wa yale ambayo mmeliambia Bunge hili mnaenda kutekeleza katika Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Tunaamini kwamba yale yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyatoa kama mawazo yao mtaenda kuyafanya kazi. Pia na yale ambayo Kamati imetoea kwa niaba ya Bunge nayo mtaenda kuyafanya kazi ili sekta hii iedelee kuwa bora zaidi na kuleta tija zaidi kwa Watanzania;

maana kama mlivyotupa takwimu maana yake ni kwamba kama mkiongeza bidii katika hiyo kazi nzuri mnayoifanya, basi tutafika sehemu nzuri. Kwa hiyo tunawapongeza sana na tunawatakia kila kheri kwenye utekelezaji wa hii bajeti ambayo mmeiomba kwa Bunge na Bunge limeidhinisha.

Waheshimiwa Wabunge, pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana Wanakamati ambao wamefanya kazi kwa niaba yetu sote. Kimsingi tunapoisisia Serikali katika maeneo kama haya maana yake Kamati ambayo inafanya kwa niaba yetu sisi sote inaisimamia vizuri sekta hii. Kwa hiyo tuwapongeze wenzetu wa Kamati hii kwa kuisimamia vizuri Wizara hii, kwa hiyo inafanya vizuri na sisi tuwaombe muendelee kufanya hivyo ili tuendelee kuona matunda mazuri ya hii sekta muhimu kabisa katika Taifa letu. (*Makofi*)

Pia niwashukuru Wabunge wote ambao wamepata fursa ya kuchangia kwenye hoja hii na naamini hayo yataboresha utendaji kazi wa Wizara, Waziri yuko hapa Naibu wake wamewasikia na pia Watendaji wao Wakuu wote wako hapa wamewasikia. Kwa hiyo kila mtu atakuwa amechukua yale yanayomhusu katika sekta yame na kwa namna mlivyo sema Waziri anawasikiliza wataalam wake na wataalam wako hapa, basi naamini Mheshimiwa Waziri ataweza kufanya kazi nzuri zaidi huko tunakokwenda. .(*Makofi*)

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa ninalo tangazo; la kwanza, ni kwa kuwakumbusha wengine walikuwa wametoka wakati tangazo la kuahirisha futari ambayo ilikuwa tumealikwa na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwamba imeahirishwa mpaka itakapotangazwa tena kwa sababu siku ya leo kuna futari nyiningine mahali kwingine ambako Waheshimiwa Wabunge wamealikwa huko, usiulize wapi kama hukupata mwaliko maana yake leo huendi huko, wanaoenda huko wameshapata mialiko.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo pia la wageni ambao tuko nao hapa Bungeni, tunao wanafunzi 85

kutoka Taasisi ya Uhasibu Tanzania (*TIA*) ya Jijini Dar es Salam, karibuni sana wageni wetu, karibuni sana. Hawa wamekuja kwa ajili ya mafunzo kuona namna Bunge linavyofanya kazi na tunaamini wamepata fursa ya kuona namna tunavyofanya kazi. (*Makofi*)

Wageni nawaona wengi lakini nataka kuamini kwamba wengine walishatambulishwa asubuhi ndiyo maana orodha yao sipo nayo hapa, lakini kama kuna wageni ambao wameingia na hatujawatambulisha basi tunawashukuru kwa kuja na karibuni sana tumefurahi kuwaona wote kwa pamoja.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.00 Jioni Bunge lillahirishwa hadi Siku ya Jumatatu,
Tarehe 27 Mei, 2019, Saa Tatu Asubuhi)*